ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Mbili - Tarehe 02 Machi, 2017

(Kikao kilianza saa 3:00 asuuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mhe. Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

UTARATIBU

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, nimesimama kwa Kanuni ya 37 lakini nakazia kwenye Kanuni ya 72(1). Kiwango cha vikao vya Baraza la Wawakilishi ni nusu ya Wajumbe. Nashangaa sasa hivi tunaanza Kikao cha Baraza hata nusu ya Wajumbe hatujafika.

Naomba Mhe. Mwenyekiti, kwa nguvu zako tuahirishe kikao mpaka tutakapotimia tuendelee.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Katibu hebu chukua idadi ya Wajumbe waliomo angalia.

(Baada ya kuhesabiwa Waheshimiwa Wajumbe walitimia kutokana na kuingia ukumbini kwa haraka haraka kwa muda wa dakika kama tatu hivi)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa *quorum* imetimia, kwa hivyo madhali imetimia tunaendelea.

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa sana na taadhima naomba kuweka mezani Hoja kuhusu Ongezeko na Uingizaji wa Utumiaji wa Madawa ya Kulevya Zanzibar.

Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako, naomba kuweka hati mezani kuhusu Hoja ya kuhusu kutoa Maazimio Kuhusiana na Uimarishaji wa Mfumo mzima wa Sheria unaohusiana na Uendeshwaji wa Kesi za Udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 55

Kuwekwa Nguzo za Umeme za Kudumu katika Viwanja vya Michezo

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:-

Pamoja na jitihada nzuri za kusambaza umeme katika sehemu mbali mbali za nchi kwa kuimarisha miundombunu ya umeme, lakini yametokea matukio ya kuweka umeme huo hadi katika sehemu ambazo hazina mahitaji ya kawaida ya umeme.

a) Je, ni lini shirika lako litaziondosha nguzo za umeme ambazo zimewekwa kwenye viwanja vya mpira vya Mnazi Mmoja.

b) Je, huoni kuwa tunaondosha haiba na malengo ya viwanja vile vya mpira kwa kuwekwa nguzo za umeme kwa muda mrefu.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 55 lenye vipengele (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, viwanja vya Mnazi Mmoja pamoja na kutumika kwa shughuli za kimichezo, pia huwa vinatumika kwa shughuli mbali mbali za kitaifa na kijamii ambapo huduma ya umeme huhitajika. Katika upelekaji wa huduma hiyo ya umeme uchomekaji wa nguzo ni jambo la lazima. Hivyo wizara yangu kupitia Shirika la Umeme linahakikisha kuwa uchomekaji wa nguzo hizo hauathiri matumizi ya viwanja hivyo kwa shughuli za kimichezo na ndio maana zinaendelea kuwepo.

Malengo ya viwanja hapo pale pale kwa ajili ya michezo na shughuli za kijamii, hivyo haiba ya viwanja hivyo itaendelea kuwepo.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya kibabe ya wizara, nathubutu kusema kwamba nguzo za umeme miaka ya nyuma katika viwanja vile ilikuwa hapana na zinapohitajika zinachomekwa. Iweje, kuna ugumu gani kwamba nguzo zile zisiondoshwe ili zinapohitajika

zikawekwa, kulikoni sasa hivi imekuwa muda mwingi umepita lakini bado unaambiwa nguzo hizo haziondoki. Mimi nakumbuka viwanja vile tumevitumia huko nyuma.

Je, serikali ina maana ndio imeshaamua nguzo zile kuziacha maisha pale.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nimesema kuwa viwanja vinatumika sio tu kwa michezo bali pia kwenye shughuli nyengine za kitaifa kama Mikutano, Maulidi na mambo mengine ambapo pia umeme huhitajika.

Sasa katika hali ya kawaida isingekuwa vyema tukakosa nguzo au nyaya wakati wa shughuli hizo zinapohitajika pale. Kwa sababu tukichukua tukipeleka katika eneo lakini inapotokea *emergency* ya kutaka nguzo au *wire* katika matumizi mengine na huku ikitakikana hatimaye ikiwa havipatikani vile vitu katika kuja kurejesha itakuwa tatizo. Lakini pia chukua, ondosha, chukua, ondosha; ni gharama ambazo si za lazima, lakini wakati hakuna athari haipunguzi haiba ni vyema basi Mhe. Mwakilishi akakubaliana nasi kwamba zile nguzo ziendelee kubakia pale kwa matumizi hayo ambayo yamekusudiwa. Ahsante sana.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru nataka kuuliza swali dogo la nyongeza Mhe. Naibu Waziri .

Katika jawabu zake amesema kwamba suala la kuondosha, weka, ondosha linawapa gharama Shirika la Umeme. Nataka nimuulize kwa kuwa umeme ule wanaotumia wote wanalipia. Jee, hizo gharama zinazojitokeza zinatokea wapi wakati wahudumu wa utumiaji wa umeme katika maeneo ya viwanja wanatoa wananchi wenyewe.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli wananchi wanalipia lakini wanalipia ile huduma ya umeme. Naomba sana tujielekeze zaidi katika labda kuonesha kama kuna athari ya zile nguzo, kwa sababu kuweko pale tumesema kwamba kusije kukawa kuna shida siku moja zinahitajika nguzo ziwekwe pale ikawa hatunazo tushazitumia

katika matumizi mengine kwa wananchi. Sasa tuweke pale ni vizuri kuhakikisha eneo lile kwamba linapata huduma hiyo wakati wowote inapohitajika ahsante sana.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana mimi swali langu la ziada lina (a) na (b).

(a) Kwa kuwa wizara yake ina masuala ya mazingira. Je, haioni kwamba kuweka nguzo zile ndani ya viwanja vya mpira ni kuchafua mazingira na haiba ya viwanja.
(b) Tuna taarifa kwamba Waheshimiwa Wabunge mnawapatia nguzo za umeme bure wanapata kutoka *ZECO*. Je hili suala atuhakikishie lipo kweli au vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lenye (a) na (b) ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mimi nahusiana na mazingira lakini uchomekaji ule pale ume-*observe* yote hayo, na ndio hilo tunahofia pia chomoa, chomeka, chomoa, chomeka, tutakuwa tunaharibu; lakini ikikaa pale ndio imekaa maana yake tume-*save* mazingira yenyewe. Kwa hivyo, katika ku-*save* mazingira tunaomba mutuunge mkono kwamba zile nguzo ziendelee kuwepo pale.

(b) Ni kwamba hilo sio kweli kuwa Mbunge anapewa nguzo tu, lakini shirika lipo kwa niaba yetu kama kuna haja maalum unaweza kwenda kuonana na uongozi wa shirika namna ya kufanya basi itajulikana kule. Kwa sababu tupo katika kusaidia wananchi wetu wapate nafuu ahsante sana.

Nam. 66

Hatua Zilizochukuliwa kwa Waharibifu wa Mazingira

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis - Aliuliza:-

Uharibifu wa mazingira ni suala lililoathiri katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar hasa Wilaya ya Magharibi na Wilaya ya Kati. Uharibifu huo husababisha madhara makubwa kwa jamii na pia kutia hasara serikali kwa kuharibu miundombinu mbali mbali iliyowekwa.

Je, ni matukio mangapi ya uharibifu wa mazingira yaliyoripotiwa na hatua gani za kisheria zilizochukuliwa kwa wale waliothibitishwa kufanya makosa hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 66 kama ifuatavyo:-

Lakini kabla ya kumjibu naomba niungane na Mhe. Mwakilishi huyo kuwa, uharibifu wa mazingira ni tatizo liliopo katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar na limekuwa likiathiri ustawi wa maisha na maendeleo endelevu ya Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, ndio maana serikali imekuwa ikichukua hatua mbali mbali za kisera, kisheria na kimkakati za kukabiliana ha hali hiyo. Baada ya utangulizi huo sasa naomba nimjibu Mheshimiwa kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, mwaka 2013/2014, Serikali kupitia Idara ya Mazingira, Idara ya Misitu, pamoja na taasisi nyengine husika ilianzisha programu maalum ya kudhibiti uchimbaji mchanga na ukataji miti ovyo katika maeneo mbali mbali ya Unguja na Pemba.

Katika kutekeleza programu hiyo, hadi kufikia Novemba, 2016 jumla ya magari 13 ya mchanga, magari ya ng'ombe 40 na misumeno 51 ilikamatwa kwa upande wa Unguja na kwa Upande wa Pemba magari 2 ya mchanga, magari ya ng'ombe 7 na misumeno 32 ilikamatwa na kuchomwa moto. Aidha, jumla ya watu 207 wamekamatwa Unguja na Pemba kutokana na matumikio mbali mbali ya uharibifu wa mazingira na kuchukuliwa hatua za kisheria. Jumla ya shilingi 177,032,600/= zililipwa na watuhumiwa hao katika kipindi hicho kutokana na matukio hayo.

Aidha, kwa ajili ya kuongeza kasi ya kudhibiti uharibifu wa mazingira katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar, serikali imezitaka taasisi husika kutumia Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa husika. Kwa hivi sasa mkazo zaidi umewekwa katika Mkoa wa Mjini/Magharibi hasa Wilaya ya Magharibi kwa kuwa ndiko kwenye wimbi kubwa la uharibifu wa mazingira.

Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis: Mhe. Mwenyekiti ahsante, napenda nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri, lakini katika majibu yake Mhe. Naibu Waziri alisema kuwa kuna hatua mbali mbali za kisera,

kisheria na kimkakati ambazo zinachukuliwa. Lakini kutokana na hatua hizo napenda nimuulize swali dogo tu la nyongeza.

Jee, ni mikakati gani iliyowekwa na wizara ili kudhibiti hali hiyo isiendelee kwa sababu tunaona bado uharibifu wa mazingira unaendelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba tumejipangia kufanya *patrol* katika maeneo mbali mbali na imekuwa tunaendana kutokana na mazingira yalivyo yale husika. Lakini chengine tumekuwa tukishirikisha ama tunaomba taarifa kupitia watu tofauti katika maeneo husika. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti ahsante sana, nami niulize maswali madogo sana ya nyongeza.

Kitengo cha Mazingira Mhe. Naibu Waziri kiko kwake na *Alhamdulillahi* kimepata Mkurugenzi msomi ambaye hauyumbi na mtendaji. Lakini ni sababu gani za Katibu Mtendaji wa Kamisheni na Mkurugenzi Mipango Miji wakati Mkurugenzi ameshatoa ripoti ya mazingira *EIA* na baadae mwekezaji anayumbishwa. Hawaoni kurudisha nyuma wawekezaji.

La pili pametajwa habari ya ng'ombe 40 waliokamatwa. Jee, kuna utaratibu gani wa kuwakomboa ng'ombe wale mtu ili apate ng'ombe wake.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, naomba arudie swali lake la pili kabla ya kumjibu huku.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, swali la pili alitaja kama ng'ombe 40 wamekamatwa, ili mwananchi mnyonge anataka kugomboa ng'ombe wake yule kuna utaratibu gani ili apate na kama amezaa atalipia wote wawili au vipi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kabla sijamjibu hilo swali hili la (a) nahisi kama ni swali jipya kabisa, hapa nitahitaji muongozi wako Mwenyekiti kama lijibiwe au vipi.

Lakini la (b) ni kwamba sheria zipo aliyekuwa kakamatwa basi kuna *fine* na mambo mengine. Kwa mujibu wa sheria atapata haki yake kwa yeyote ambaye kakamatwa ng'ombe wake aende katika taasisi husika ili sheria ichukue mkondo wake, ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni zetu kama kukataa swali ni wewe, sio Mjumbe na mimi sikuuliza sokoni wala Mwanakwerekwe.

Utaratibu nimeuliza hapa kwenye chombo cha wananchi, naomba ajibu swali kama nilivyomuuliza.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea kujibu na swali la pili.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba taasisi zote zinaongozwa na sheria. Mazingira wakiona hapa wanaweza kutoa *EIA* wanatoa, lakini ardhi pia kuna sheria na sheria moja haiwezi kuilazimisha taasisi nyengine. Lakini naomba nilichukue na tukaangalie kikwazo ni nini, kama ni sheria au kuna nini. Nakuahidi kama si sheria basi kila kitu kitakwenda sawa lakini kama sheria maana yake tufuate sheria.

Mwenyekiti ahsante sana.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Hakunifahamu Mhe. Waziri swali jepesi sana. namwambia Mkurugenzi ...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim, sijakuruhusu uendelee. Katibu endelea.

Nam. 9

Malipo kwa Madeni ya Wakulima

Mhe. Jaku Hashim Ayoub - Aliuliza:-

Wakulima wa Wilaya ya Mkoani katika Bonde la Darajani lilioko Makombeni kwa muda mrefu wanaidai serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili,Mifugo na Uvuvi.

a) Je, ni kiasi gani wanachodai wakulima hao na ni wakulima wangapi wanasubiri malipo hayo mpaka sasa.

b) Je, ni sababu gani za msingi zilizopelekea kutolipwa kwa wakati wakulima hao wakati wizara ina wataalamu wa mipango ambao wanatakiwa kupanga na kuamua kabla ya utekelezaji wake kufanyika.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi- Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake nambari 9 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na idadi ya wakulima wanachodai malipo kwa kazi ya kuweka taa Konde na kujenga matuta ni wakulima 71, fedha wanazodai ni Tanzania shilingi ni milioni kumi na tano.

b) Mhe. Mwenyekiti, naomba nikiri kwamba kitendo cha kuchelewa kuwalipa wakulima hao kimeathiri maendeleo ya sekta ya kilimo na kubadilisha hali ya maisha kwa wakulima hawa. Iwapo wangelipata mapema malipo ya fedha wanazodai wangeliweza kununua pembejeo ikiwemo mbolea, dawa na mambo mengine ya kufanikisha ukulima huo pamoja na suala zima la kuongeza kipato na tija kwa sekta ya kilimo.

Wizara huwa haina lengo wala dhamira ya kucheleweshe madeni ya wakulima lakini wakati mwengine upatikanaji wa fedha unakuwa mgumu. Jambo ambalo linatukwanza aidha Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi itaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba madeni yanalipwa mapema kwa kadri inavyowezekana.

Mhe. Mwenyekiti, sababu za msingi za wakulima hawa kutolipwa kwa wakati ingawa wizara ina wataalamu wa mipango ambayo wanatakiwa kupanga na

kuamua kabla ya utekelezaji wake kufanyika. Ifahamike kwamba kupanga ni jambo moja na kuingiziwa fedha ni jambo jengine. Tatizo liliopo ni kutolewa kwa fedha hizo kwa kiasi kidogo sana ukilinganisha na madai ya wakulima katika maeneo tofauti ya mradi iliyotelekezwa katika mabonde ya umwagiliaji.

Aidha, fedha hizo hutengwa kupitia *capital* ambacho kwa kipindi hiki fedha hizi zimepatikana kiasi kidogo kulingana na mahitaji. Hata hivyo, wizara yangu inaahidi kufanya malipo hayo japo kwa kutumia fedha za matumizi ya kawaida *OC* katika kipindi kifupi kijacho.

Kwa niaba ya Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi nawaomba radhi wakulima wote walioathirika na kadhia hii. Ahsante.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na swali hili toka kuingia Barazani kuleta maswali Afisi ya Spika haijawi kuniita imeniita mara nne kwa suala hili. Lakini itakuwa nitakuwa sijamfanyia haki Mhe. Naibu Waziri kama sikumpongeza kwa kukiri suala hili, nikupongeze sana Mhe. Naibu Waziri kuwa umekiri.

Baada ya kukiri naomba nikuulize maswali madogo sana ya nyongeza.

(a) Kwa kuwa pesa thamani yake inashuka shilingi mwaka jana tofauti na mwaka huu. Jee, kuna fidia gani mtawalipa wananchi kwa kiasi hicho.

Vile vile nikueleze tu taarifa nilizokuwanazo kutoka kule Darajani Makombeni ni milioni kumi na mbili laki moja, hebu fuatilia vizuri isije kuwa milioni kumi na tano ikawa pana njia kidogo ya kutoka kutoka. Taarifa niliokuwa nayo ni kama milioni kumi na mbili laki moja.

(b) Mpango wa utekelezaji kipi kinaanza mwanzo mpaka mtumie vifungu vya bajeti nyengine, hamuoni kwamba huu ni uzembe munaofanya hivi sasa wizara.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Waziri jibu namba moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako ninapenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayou swali lake la nyongeza ifuatavyo.

(a) Fidia kwa wananchi ni kweli shilingi inashuka lakini vile vile wakumbuke kwamba hii ilikuwa ni kazi nguvu yao ambayo wao walipaswa

wafanye hii na bila ya malipo. Kutokana na huruma za serikali hii kazi walisema hawaiwezi na baada yake wakaambiwa basi tutakulipeni ndipo waliweza kuifanya kazi hii na serikali ikakubali kubebea deni hili. Kwa hivyo, naomba tu wananchi wakubali kile ambacho watakacholipwa na serikali.

Kuhusiana kwamba umesema umefanya utafiti kwamba milioni kumi na mbili hili sawa nachukua tutakwenda kulifanyia kazi kama ni milioni kumi na mbili ama milioni kumi na tano. Nashukuru.

Nam 97

Kurejeshwa Mashamba ya Mikarafuu kwa Wananchi Pemba

Mhe. Omar Seif Abeid -Aliuliza**:-**

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba marehemu Salim Nassor Juma aliruhusu wananchi wanaotaka mashamba ya mikarafuu ya Serikali wayafyekee na kupanda mikarafuu mipya hata hivyo, badala ya kufanya hivyo, wananchi hao sasa wameondoshwa kwa maelezo kuwa hawana nyaraka za mashamba hayo na kusababisha manung'uniko makubwa.

a. Je, ni lini Serikali itawarudishia wananchi mashamba hayo ili waweze kupanda mikarafuu zaidi.

b. Je, Serikali haioni kwamba kutowaachia wananchi kuyatumia mashamba hayo yaliokuwa ya eka tatu hasa ya mikarafuu kumepunguza ari ya kutimiza azma ya Serikali ya kuongeza kupanda mikarafuu

c. Je, Wizara ya Kilimo, kupitia Idara ya mashamba tangu ilipoyarithi mashamba hayo kutoka Idara ya Ardhi imeshapanda mikarafuu mingapi katika mashamba hayo wanayoyakodisha.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi- Alijibu

Mhe. Mwenyekiti, Kwa ruhusu yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Namba 97 lenye (a) (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mheshimiwa naomba kutoa maelezo mafupi kuhusiana na swali lake.

Serikali ilitoa mashamba ya eka tatu kwa wananchi mara tu baada ya Mapinduzi Matukufu ya mwaka 1964, kwa nia ya kuyaendeleza kwa kupanda mazao ya chakula na miti ya kudumu. Ugawaji huo ulikuwa na lengo la kuwapatia wananchi hao ardhi ili waondokane na unyonge na umaskini wa kipato lakini pia na kuongeza pato la taifa.

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumfahamisha Mhe Mwakilishi kwamba Mkuu wa Mkoa hana mamlaka wakugawa mashamba, hii ni kazi ya Wizara ya Ardhi na Mkuu wa Mkoa anapaswa kusimamia shughuli za mashamba hayo.

Baada ya maelezo hayo machache naomba kumjibu Mhe mwakilishi swali lake lenye kipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, **k**wanza hakuna mtu yeyote aliyenyang'anywa shamba isipokuwa kwa sasa Wizara ya Kilimo iko katika kazi ya utafutaji wa mashamba hayo na kuyapangia utaratibu mpya.

Mhe. Mwenyekiti, **k**wa wale wananchi wenye mikataba halali ya mashamba hayo wanaendelea kuyatumia bila tatizo lolote na kwa wale ambao hawana umiliki halali, baada ya kukamilika kwa upatikanaji wa mashamba hayo watatakiwa kufuata utaratibu wa kuyaomba upya ili waweze kupata umiliki halali na kuyaendeleza kwa kilimo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, haina utaratibu na wala haikutakiwa kupanda mikarafuu katika mashamba ya eka yaliyogawiwa kwa wananchi isipokuwa wizara hii ina jukumu la kuwahamasisha na kuwaelimisha wananchi kupanda miti mbalimbali ikiwemo mikarafuu katika mashamba hayo ya eka tatu pamoja na mashamba yao ya urithi.

Aidha, Wizara ya Kilimo ina jukumu la kuotesha miche ya mikarafuu kwenye vitalu na kuigawa kwa wananchi bila ya malipo kwa ajili ya kupanda katika mashamba yao yakiwemo ya eka tatu.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri lakini swali langu limejikita zaidi kwenye miaka ya nyuma sio leo kwenye miaka ya tisini na nilieza hivyo, na kwa kuwa hili jambo ninalolizungumza mimi lipo.

(a) Je, Waziri atanithibitia vipi iwapo watatokea wale watu waliyoyapanda mashamba yale wakayaendeleza yaliokuwa mapori matupu wakenda wakafyeka wakayapanda na leo wamezuiwa kuyatumia. Unasemaje

Mheshimiwa juu wa suala hili kama utatokea ushahidi wa mtu kama kafanyia hivyo, serikali itatoa jibu gani.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hii ardhi au mashamba serikali imeyapa mashamba haya. Lakini vile vile sasa hivi tunafanya upya kujua haya mashamba yana uhalali mtu ama anamiliki tu kwa kupeana kwa kurithi. Ndio maana nikasema tutakapomaliza kuyayafuta mashamba haya basi watatakiwa waombe upya, kama ni wao wahusika kweli kweli basi wasione tabu kuomba upya tena halafu wataendelea kuyatumia mashamba hayo. Nashukuru.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuongezea majibu ya Mhe. Omar Seif Abeid kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni hivi karibuni tuna serikali imeunda kamati maalum inayoongozwa na Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya kwenda Pemba kuangalia kwa undani mashamba ya mikarafuu ambayo awali yake yalimilikiwa na serikali na yale mashamba mengine ambayo yana utata wa umiliki.

Kwa hivyo, niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi kuvuta subra kuona hatua zinazochuliwa na serikali katika kuhakikisha kwamba kila mmoja anapata haki yake kwa mujibu wa sheria na hakuna wajanja wanaohodhi mashamba ya serikali kwa kuyafanya yao binafsi.(*Makofi*).

Kwa msingi huo basi hatua mbali mbali zinaendelea kuchukuliwa na serikali kama alivyokwisha eleza Mhe. Naibu Waziri, lakini kila hatua zitachukuliwa kuhakikisha kila mwenye haki anapata haki yake na wananchi wanaendelea kufanya shughuli zao za kilimo bila ya matatizo ili kila mmoja aweze kupata haki yake ya msingi katika nchi yetu.

Nam. 43

Matumizi mabaya ya Mitandao

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:**

Katika siku za karibuni kumekuwa na matumizi mabaya ya mitandao ikiwemo kusambazwa picha za ngono.

Jee, hatua gani zimechukuliwa dhidi ya watu wanaofanya vitendo hivyo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 43 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, makosa ya matumizi mabaya ya mtandao ni makosa yanayoshirikisha miundombinu ya mawasiliano ya ndani na nje ya nchi. Kitengo cha Makosa ya Mtandao kipo kwenye Jeshi la Polisi na kina mashirikiano na mataifa mbali mbali katika kushughulikia makosa ya aina hiyo.

Hivi karibuni kumekuwa na aina tofauti za makosa ya mitandao ambayo yameripotiwa katika kitengo hicho. Makosa hayo hufanyiwa uchunguzi na inapobainika kuwepo na uvunjwaji wa Sheria za Mtandao, muhusika huchukuliwa hatua zinazostahiki ikiwa ni pamoja na kupandishwa Mahakamani.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri, naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, tukumbuke kwamba suala la utumiaji mbaya wa mitandao kwa Zanzibar limekithiri hata kupelekea kuchafuliwa kwa hali ya ushwari ndani ya nchii hii usalama uliokuwepo, kumekuwa na mitandao mbali mbali, *Mzalendo Network* wanaandika mambo ambayo hayastahiki na sheria zipo za kudhibiti.

(a) Je, wizara yako imejipanga vipi kuyadhibi ili tusione tena mitandao ile kumuandika vibaya Rais wa Zanzibar kusema uongo na kuhatarisha usalama wa nchi hii.

(b) Umesema kwamba watumiaji makosa wamebainika. Je, ni kesi ngapi ambazo zimepandishwa Mahakamani na zimetolewa hukumu kwa hao watumiaji mitandao vibaya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani maswali yake ya nyongeza yenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, wizara yetu baada ya kuileta hapa Barazani Sheria ile ya Makosa ya Mtandao na kuridhiwa tarehe 28 Septemba 2016, Sheria Namba 14 ya 2015 Makosa ya Mtandao wa Jinai tumeanza kutoa elimu na vile vile tumekaa na wahusika, yaani Jeshi la Polisi kuwaelezea kuhusu ile sheria ilivyo na kwa mujibu wa sheria ile wao Polisi wanatakiwa wazipeleke zile kesi Mahakamani baada ya watu wale ambao wametendewa yale makosa kwenda kutoa ushirikiano na Jeshi la Polisi.

b) Mpaka sasa hivi kuna kesi mbili ziko kwa Mkuu wa Mashtaka wa Serikali (*DDP).* Kesi moja wapo ni kesi iliyotokea karibuni Jang'ombe na nyengine ile iliyotumika ya kumkashifu Mtume Muhammad (SAW). Kwa hivyo, kezi bado hazijapelekwa Mahakamani.

Lakini kama nilivyosema watu wengi hii sheria hawaijui vizuri. Kwa hivyo, sisi tutakaa na wadau ili kutoa mafunzo kama tulivyoanza ili waelewe. Lakini Sheria hii ina adhabu nyingi sana kwa wale wote wanaokwenda kinyume na Sheria hii ambayo vile vile inakiuka maadili yetu ya Wazanzibari basi hatua kali zinachukuliwa kwa mujibu wa hii Sheria.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi swali langu la ziada lenye (a) na (b).

Kwa kuwa nchi nyingi zilizoendelea kwenye kudhibiti masuala ya mtandao, wana watendaji maalum wa ku- *search engine* ambao wataangalia zile *web-site* au zile programu ambazo watu wanatukana na kufanya mambo ambayo yaliokuwa hayana maana.

(a) Naomba utwambie ni *web-site* ngapi au mitandao wanaotumia watu binafsi ni wangapi ambao tayari mmeshawakamata kwa *list* ambao wanatukana Serikali au wanatukana nchi pamoja na kuhatarisha nchi yetu.

(b) Ni lini sasa hizi *web-site* mtaweza kuzi-*block* kwenye hii mitandao ambayo ni za *Zanlik* na *Zanzinet* na waliokuwepo kuzungumza nao ili kuhakikisha mnazi-*block* kabisa zisifanye kazi katika *Network* zao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye Kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kuna mitandao mingine yaani *web-site* wamefungua mfano wa nje ya nchi. Mitandao aliotaja moja wapo umefungua *web-site* yake Uingereza. Sasa kama nilivyojibu katika swali langu la mwanzo kwamba ni wajibu wa vyombo vya Polisi kushirikiana na Polisi wa Kimataifa katika kuhakikisha kwamba pale tatizo linapotokea sisi tuwape taarifa na wao wafanye uchunguzi. Sasa hili jambo ambalo kama mtandao umechukuwa ruhusa nje ya nchi inakuwa kazi kidogo.

Lakini Jeshi la Polisi hivi sasa liko makini na ni karibuni tu kama alivyozungumza Mhe. Abdalla Maulid Diwani wanaendelea kufuatiliwa wale watu waliotoa ile hotuba feki ya Mhe. Rais na tunasema kwamba iwapo kama watapatikana tutawafikisha Mahakamani na kwa mujibu wa sheria yetu hii basi kuna adhabu kali dhidi yao.

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

UTARATIBU

Mhe. Nadir Abdul- latif Yussuf: Niliuliza swali la (b) kwamba hizi *web-site* ambazo ziko ndani ya Zanzibar ambazo haziko nje ya Zanzibar ni lini sasa mtakaa na mashirika ambayo yapo ndani ya Tanzania mtazi-*block* ili zisiweze kufanya kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyomuarifu kwamba mambo ya ku-*block* au kuto-*block* yanaenda kwa mujibu wa sheria ile Namba 14 ya 2015 ya Makosa ya Mtandao.

Sasa pale tutakaporidhika na ushahidi kamili basi wakati wowote tunastahiki kuzi-*block* zile *Network* ambazo zinafanyakazi kinyume na maadili na vile vile

kuzifikisha Mahakamani. Na zinapofikishwa Mahakamani kama nilivyosema iwapo itabainika basi adhabu kwa mujibu wa sheria zitachukuliwa dhidi yao.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, napenda kukuzia majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwamba ukisoma ile Sheria Namba 14 ya mwaka 2015, Sheria ya *Cybercrime*, imetaja utaratibu mzuri sana na namna gani chombo chetu kinachoratibu mawasiliano nchi yaani *TCRA* kinavyoweza kushughulikia na kusimamia suala zima la mawasiliano. Kwa mujibu wa Sheria ile nadhani kifungu namba 50 ukisoma ile *section* ya pili ya ile sheria husika imeeleza vizuri sana nini jukumu la *TCCRA* katika kuchuja, kudhibiti lakini pia kuweza kwenda kutoa ushahidi Mahakamani.

Kwa hivyo, kama kuna mitandao ambayo inafanya makosa ni wajibu wa chombo cha *TCCRA*, Jeshi la Polisi kwenda kukaa pamoja wakapitia tukajiridhisha na tabwaan kutakuwa na watu watabainika kabisa kwamba haya makosa wameyafanya na ni wajibu wetu sasa kama Serikali kuiomba rasmi *TCCRA* isitende kazi upande mmoja tu katika usimamizi mzuri wa makosa haya ya kimtandao.

Sheria inaruhusu pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano kuweza kusimamia na kuweza kuwabaini na wale ambao wanabainika ni wajibu wao sasa *TCCRA* kuhakikisha kwamba wanachukua hatua za kushirikiana na Jeshi la Polisi kumshtaki ili hatua za stahiki za sheria ziweze kutolewa dhidi yao.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana kwa kunipa fursa asubuhi wa leo. Mhe. Mwenyekiti, swali ni kwamba sote tumeshuhudia Rais wetu wa Serikali na Zanzibar anatukanwa kupitia mitandao.

Je, wizara yake lini itawachukulia hatua wale wanaomtukana kupitia mitandao, aidha ndani ya nchi au nje ya nchi, na anajua sheria zinakubali mtu kuchukuliwa hatua ndani ya nchi na nje ya nchi. Lini itamchukulia hatua wanaomtukana Rais wetu kupitia mitandano, *that's the question.*

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Mwenyekiti, masuala haya ni Masuala ya Makosa ya Jinai na Kosa la Jinai haliharibiki, kwa maana kwamba halina *expiring date*, hata kama ulitenda mwaka juzi, mwaka jana madhali ulipotenda kosa Sheria ilikuwepo, maana yake ni wajibu wa serikali sasa hata ikiwa sasa kuweza

kuona watu hao wanakamatwa vielelezo vipo, wanashtakiwa na wanafikishwa mahakamani ili mkondo wa sheria uchukuwe hatua zake.

Nam. 89

Kuvunjwa kwa Sheria ya Hifadhi ya Barabara

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza:-

Serikali ya Zanzibar kwa nia safi ya kuendeleza wananchi wake na miji yake katika maeneo takribani yote ya miji na yenye barabara, imeweka Sheria kwamba barabara kubwa (*main road*) ziwe na hifadhi ya barabara kwa mita 15 na barabara ndogondogo mita 8, lakini barabara hizo kwa sasa zinaachiwa na wananchi wanajenga bila kuzuiwa na wapimaji wa viwanja hivyo wamepima mpaka maeneo ya barabara.

(a) Je, mpimaji eneo na mwananchi ni nani mwenye kosa.

(b) Je, serikali ni lini itaonesha mipaka ya barabara zake kwa vipimo ili wananchi wasiisogelee barabara na kuleta usumbufu wakati serikali inataka kujenga barabara zake.

(c) Je, serikali haioni kuwa gharama za kupima barabara zake zote hivi sasa ni ndogo kuliko kusubiri mpaka mwaka ambao serikali itaamua kujenga barabara hizo na itakuwa zimeshajaa nyumba na kuzivunja ni gharama kubwa na kupelekea uhasama na wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji – Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na napenda kuchukua nafasi hii kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 89 lenye vifungu (a), (b) na (c).
Kwanza napenda kutoa maelezo mafupi kabla ya kumjibu.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwa mujibu wa Marekebisho ya Sheria ya Barabara Nambari 17 ya mwaka 2013 kifungu Nambari 17 (1) hadi (2) kimeeleza juu ya maeneo ya hifadhi ya barabara kama ifuatavyo:-

- Mita 15 kwa barabara kuu
- Mita 12 kwa barabara zinazounganisha barabara kuu na Wilaya
- Mita 10 kwa barabara za vijijini

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kwa mwananchi anayetaka kujenga pembezoni mwa barabara, anatakiwa apeleke maombi yake kwenye Manispaa na Halmashauri, ambapo wizara yangu tayari imeshawapatia maelekezo.

Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa naomba kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, kutokana na Sheria ya Barabara Nambari 17 ya mwaka 2013 nambari 17 kifungu nambari 17 (1) hadi (2), watu wote hawa wana makosa.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali tayari imeanza kuweka viguzo kwa baadhi ya barabara na itaendelea kuziwekea viguzo barabara nyengine kadri hali ya fedha itakavyoruhusu.

(c) Ni kweli kabisa gharama za kupima barabara ni ndogo, lakini kwa wale wote watakaoamua kuvamia maeneo ya hifadhi ya barabara basi wanakuwa hawalipwi fidia. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kumuuliza Mhe. Naibu Waziri kwamba kwa sababu wananchi wetu wengi hawana taaluma, hasa usomi wetu ni mdogo kuelewa mambo ya sheria. Lakini hizi taratibu za kuvamia barabara serikali imekuwa ni kitendawili, kila siku ikitaka kujenga barabara basi lazima tuwe tuna mashaka makubwa.

(a) Je, serikali itaamua lini kuipima Zanzibar yote katika sehemu zake za barabara ili kuondoa kadhia hii.

(b) Sasa hivi Sheria ya Barabara imechanganyika kati ya Serikali za Mitaa na Mawasiliano. Je, Sheria hii itatumika mpaka Serikali za Mitaa au Serikali za Mitaa wana sheria yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi maswali yake yenye Kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

Mhe. Mjumbe ameuliza ni lini serikali itapima maeneo yote. Serikali kwa kupitia mipango miji na vijiji, tayari imeshaonesha maeneo yote ambayo yanahusu hifadhi ya barabara.

(a) Kwa hivyo, kama nilivyosema mtu yeyote hata kama hajui hii sheria, lakini kufanya kosa moja kwa moja anatakiwa aadhibiwe. Kwa hivyo, kutojua sheria maana yake sio kwamba usichukuliwe hatua.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema hii Sheria ni Sheria ambayo iko katika barabara isipokuwa tumekasimu madaraka kwa Serikali za Mitaa. Sasa wao wanafuata hii Sheria Kuu ya kuhusiana na mambo ya barabara. Ahsante Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaomba kuuliza swali moja la nyongeza kwa Mhe. Naibu Waziri, swali langu ni la (a) na (b).

(a) Ni lini sasa wizara yako itafikiria kuweka *plan* ya *future* ya barabara ambazo zitakuwa mbili katika kila njia za Zanzibar. Kwa sababu sasa hivi tumegundua kwamba mipaka yenu mnayoweka ni mipaka ile ile ya barabara moja na kipande kidogo. Ukiangalia nchi nyengine nyingi zinaweka *future plans* ambazo zitakwenda barabara mbili au tatu hapa Zanzibar bado hili suala hatujaliona.

(b) Ni lini sasa wizara yako itaweka *speed limit*, yale mabango katika barabara ili ioneshe mtu atembee *speed* gani kwa sababu tumegundua kuna matatizo Polisi hukaa na zile kamera hupeana, wanawapiga watu halafu wanawaambia unatakiwa uende *speed* sita wakati hakuna bango mwanzo mpaka mwisho wa barabara.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lenye Kifungu (a) na (b) kwa pamoja.

Mhe. Mwenyekiti, ni pale serikali au wizara yangu itakapopata pesa basi hiyo kazi tutaifanya Inshaallah.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante, swali la nyongeza.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Aah! Mhe. Mwenyekiti, niliuliza maswali mawili (a) na (b)

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri alisema anajibu kwa pamoja.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Kwa pamoja?

Mhe. Mwenyekiti: Ndio, ameshajibu.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Haya sawa.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Viwe Khamis swali la nyongeza.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa fursa hii asubuhi ya leo kuweza kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali moja la nyongeza.

Niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kujenga barabara nyingi kwa Unguja na Pemba, lakini kuna changamoto ambazo zimejitokeza katika barabara zetu za Pemba, kwenye maeneo ambayo yako karibu na skuli na kutokujenga *zebra cross* ambazo zinaleta usalama kwa watoto wetu wakati wa kutoka skuli.

Jee, Mhe. Naibu Waziri, wizara yako ina mikakati gani ya kuweka *zebra cross* kwenye maeneo ambayo yako karibu na skuli ili kuondosha ajali za mara kwa mara katika maeneo haya.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako ninapenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli tumeona kwamba upo umuhimu wa kuweka *zebra cross* katika maeneo ambayo kuna skuli au kuna sehemu ambazo watoto wanapita kwenda skuli. Ni suala ambalo tunalifanyia kazi na Inshaallah kwa uwezo wake Mwenyezi Mungu, bajeti ijayo tutatenga fungu kwa ajili ya kuifanya hiyo kazi. Ni kweli hilo suala tumeliona limejitokeza. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza muda mfupi baada ya tangazo hili nitampisha Mhe. Spika kuja kunipokea hapa. Lakini kwanza kuna tangazo.

Mhe. Ali Suleiman Ali Shihata anawatangazia Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii mkutano chumba namba 2 baada ya maswali na majibu, ahsanteni.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim. Kwanza subiri nikuombe, nyote nyinyi wenye taarifa, kwa sababu nimeshatoa taarifa kwamba Mhe. Spika anakuja subiri taarifa yako itajibiwa. Ahsante.

(Hapa Mhe. Spika alikalia kiti)

Mhe. Spika: Kuhusu utaratibu Mhe. Jaku Hashim.

UTARATIBU

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Spika, ama jambo la heri huenda kwa heri.

Mhe. Spika, Waswahili wanasema nguo ya Ijumaa hufuliwa Alhamis. Naomba ninukuu maneno yako au sijui nisome Kanuni kwanza iliyonisimamisha hapa.

Kanuni ya 63:-

"Mjumbe anaweza kusimama wakati wowote na kusema neno **"kuhusu utaratibu"** lakini Mjumbe anapofanya hivyo itabidi ataje Kanuni ya Baraza iliyokiukwa, Mjumbe yeyote ambaye wakati huo atakuwa anasema, papo hapo atakaa chini, vile vile Mjumbe anayesimama kwa kusema utaratibu atakaa chini akishakueleza jambo hilo la utaratibu...".

Mhe. Mwenyekiti, hoja yangu siku tuliyofungua Baraza 15/02/2017, niliomba baada ya maswali na majibu utaratibu, na ninukuu maneno yako Mhe. Spika:-

Mhe. Spika, alivyozungumza.

"Jaku nimesikiliza huo muongozo ambao unatoa na ni kweli na ni muhimu, lakini umuhimu wake zaidi ni kwamba wananchi waweze kupata elimu kutoka kwa serikali, waelimishwe. Kwa hivyo, mimi nitaishauri sana serikali ndani ya mkutano huu waweze kutayarisha Kauli yao kuhusiana na

masuala hayo ambayo umegusia kuhusu mchanga na viwanja, halafu baadae waje watutolee humu sote tufaidike pamoja na wananchi na hiyo elimu ambayo itakuja kutolewa wakati huo na serikali".

Kwa hivyo, mimi niitake Serikali ili mje mtoe Kauli hapa ndani ya Mkutano huu, nitatafuta muda nitamjulisha Spika, halafu nitairuhusu kwa kutoa nafasi Serikali itoe maelezo.

Mhe. Spika, naona Kikao kinakaribia kumalizika na kesho sijasikia harufu ya aina yoyote mpaka muda huu, isijekuwa kama ile Kauli aliyoitoa Waziri makini. Saa 8:30 mchana tarehe 27 Juni, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohammed Aboud Mohammed, alisema;

"Mhe. Jaku kabla ya kufunga Baraza hili tutaleta taarifa siku zilizobaki ni kidogo karibu tutamaliza. Nina uhakika tulete kitu cha msingi, kitu kizima, kitu kilichokuwa kina uhakika kitawafurahisha Wajumbe wote na wananchi wetu kwa jumla. Hatuna nia wala dhamira mbaya kugombana na Wajumbe na kugombana na wananchi. Dhamira ni kutatua tatizo lililojitokeza kwa misingi mizuri ambayo tunayazungumza hapa Mheshimiwa sote ni kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wetu, serikali ipo kwa wananchi, Waheshimiwa Wawakilishi wapo kwa wananchi nia yetu ni kuondoa kila tatizo ambalo wananchi wanalikabili. Kwa hivyo, tunawaomba Waheshimiwa Wajumbe, watuelewe kwamba jambo hili litamalizika na tutaleta Kauli hapa kabla ya kukiahirisha kikao".

Mhe. Spika, maneno haya aliyasema Waziri makini Mhe. Mohammed Aboud, lakini hatimaye ripoti hii ikaingia mitini, haikutoka Kauli ya Serikali.

Hofu yangu Mhe. Spika, yasijeyakanikuta yale ya mwanzo. Ukitafunwa na nyoka basi hata ukuti ukiuona basi utaona ni nyoka tu. Mhe. Spika, naomba muongozo wa kiti chako.

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Jaku Hashim nimekusikia na Muongozo wako nimeusikia, na bahati nzuri serikali pia ipo imesikia. Tuna leo na kesho, mimi naomba uturuhusu Ofisi ya Spika ikae na Serikali halafu tuone namna gani tutaweza kulitatua tatizo lako. *(Makofi).*

UTARATIBU

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Spika, kuhusu utaratibu naegemea Kifungu nambari 40, ambacho kina maelezo yafuatayo,

Kifungu cha 40

"Maswali ya nyongeza yanaweza kuulizwa na Mjumbe yeyote kwa madhumuni ya kutaka kuelezwa zaidi juu ya jambo lolote lililotajwa katika jibu lililotolewa".

Mhe. Spika, sisi ambao tunakaa upande wa kushoto kwako, tuna masikitiko makubwa kwa Mwenyekiti wetu wa Baraza, akiwa kwenye kiti chako hapo haangalii upande huu, hatuna uhakika kama anaumwa na shingo au mzima, yaani huku hatupati nafasi mpaka tuwe tumeuliza upande huu mtupu ule kule haukuuliza. Tunataka kujua Muongozo ni kwa nini inakuwa hivi, na hii tunaona sisi inasababisha kutokuwa na utulivu Barazani na hiki ni chombo kikubwa ambacho kinatakiwa kitolewe haki humu sawa, lakini tunaona kwamba mambo yanakwenda ovyo. Kwa hivyo, tunaomba Muongozo wako. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante Mhe. Machano Othman Saidi na hilo naomba nilichukue halafu nitakaa na wenzangu Mhe. Naibu Spika pamoja na Wenyeviti ili tuweze kulipatia ufumbuzi.

Lakini tutajitahidi sana maswali yanapoulizwa, labda kwa kuwa Mawaziri mara nyingi wanajibu kwa upande huu wa kulia, anasahau kurejesha uso upande kushoto kwake Mhe. Mwenyekiti. Lakini tutaliweka sawa Waheshimiwa Wajumbe, tupeni muda tu. Katibu kwa shughuli inayofuata.

HOJA ZA WAJUMBE

HOJA YA MJUMBE KUHUSU ONGEZEKO LA UINGIZAJI NA UTUMIAJI WA MADAWA YA KULEVYA ZANZIBAR

(Imefanywa chini ya Kanuni ya 27(1)(n), 27(3), 49(1) na Kanuni ya 50 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2016).

MAELEZO YA HOJA

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu sana. Lakini pili nikushukuru na wewe kwa kuniruhusu kusimama mbele ya Baraza lako na kusoma hoja yangu hii. Lakini tatu, nimshukuru sana Makamu wa Pili wa Rais kiongozi wa serikali katika Baraza hili na yeye kwa kuruhusu hoja yangu kuweza kuisoma leo.

Nne, niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, kwa kuendelea kuniamini na kuendelea kunipa ushirikiano tosha wakati nikisoma hoja zangu. Lakini niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Mpendae kwa kuendelea nao

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, tunaomba tusikilizane, mumsikilize Mhe. Mjumbe akiwasilisha hii hoja. Mhe. Mohammed Said Mohammed endelea.

Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa): Niwashukuru sana wananchi wa Jimbo langu la Mpendae pamoja nao kwa kuweza kuniamini na kuendelea kufanya kazi zao. Vile vile nikishukuru Chama changu Chama cha Mapinduzi, kwa kuendelea kuniamini.

Kubwa zaidi na la mwisho lakini kwa umuhimu wake niwashukuru Wajumbe wako wote, pamoja na wananchi wa Jimbo la Mpendae, pamoja na wananchi wa Zanzibar yote kwa kunifariji wakati wa msiba wa mama yangu mzazi, nawashukuru sana. Ni vigumu sana kumshukuru mmoja mmoja, nilisema nitumie nafasi hii kuweza kuwashukuru wote, nawashukuru sana kwa kunifariji.(*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba sasa niendelee na hoja kama ulivyonitaka nisome.

Mhe. Spika, chini ya Kanuni ya 27(1)(n), 27(3), 49(1) na Kanuni ya 50, Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la Mwaka 2016, naomba niisome na maelezo ya hoja hii.

Mhe. Spika, dawa za kulevya ni kemikali ambazo huathiri kufanyakazi katika mfumo wa fahamu unaojumuisha uti wa mgongo, ubongo na kuleta mabadiliko ya hisia, fikra na tabia. Dawa hizi hutumiwa na watu kati ya milioni 155 na 250 duniani, na pia ni biashara kubwa inayokadiriwa kufikia Dola bilioni 320 kwa mwaka, kiasi ambacho ni karibu asilimia moja ya pato lote la dunia.

Mhe. Spika, biashara ya dawa za kulevya hujumuisha shughuli zote zinazowezesha upatikana kwa dawa hizi kwa ajili ya matumizi haram, ambapo shughuli hizo ni pamoja na uzalishaji, ikiwemo kilimo, utengenezaji, usafirishaji, mauzo, manunuzi na uhifadhi na usambazaji wa dawa hizi.

Mhe. Spika, biashara haramu ya dawa za kulevya inakatazwa kisheria takribani katika nchi zote duniani ikiwemo Zanzibar. Kwa sababu hiyo, watu wanaojihusisha na biashara hii huiendesha kwa siri na hujiunga katika

mitandao kutoka nchi mbali mbali na hivyo kujulikana kama mitandao ya kimataifa.

Mhe. Spika, madhara ya biashara haramu ya dawa za kulevya sio tu huathiri shughuli za kiuchumi, lakini pia athari kubwa sana huonekana katika jamii pale inapozidi idadi ya watumiaji wa dawa za kulevya katika jamii na kuongezeka kwa athari zinazosababishwa na utumiaji wa dawa hizi hasa kwa vijana siku hadi siku, ambapo athari hizo ni pamoja na kukithiri kwa vitendo vya rushwa, ujambazi, maambukizo ya maradhi ya ukimwi, kupoteza nguvu kazi ya taifa ambayo wengi wao ni vijana, kushuka kwa kiwango cha elimu nchini na kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Spika, pamoja na athari hizo zinazotokana katika jamii yetu, ambapo wengi wao wanaoathirika ni vijana wetu, lakini la kusikitisha zaidi wapo baadhi ya wanawake ndani ya Zanzibar ambao tayari wanajihusisha na usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya, aidha kwa kushawishiwa au kwa namna nyengine yoyote ile, jambo ambalo hupelekea kuzidi kwa vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake.

Takwimu iliyofanywa Tanzania kwa mwaka 2015 inaonesha kuwa wanaume wanaendelea kuwa wahusika wakuu wa biashara ya madawa ya kulevya, ingawa wanawake nao wanajimuhushwa na biashara hiyo kwani kati ya watu 15,815 waliokamatwa nchini kwa tuhuma hizo, wanawake walikuwa 1,436.

Mhe. Spika, pamoja na athari zilizoonekana ndani ya nchi, lakini wapo baadhi ya wananchi ambao ni raia wa Tanzania wakiwemo Wazanzibari, hukamatwa katika nchi mbali mbali ulimwenguni kwa kujihusisha na biashara haramu za madawa ya kulevya, jambo ambalo inaitia nchi yetu kwenye sifa mbaya ulimwenguni. Maelfu ya Watanzania wanatumikia vifungo mbali mbali nje ya nchi ikiwemo vifungo vya maisha na wengine wanasubiri kunyongwa. Takriban wafungwa 578 wamekamatwa na madawa ya kulevya nje ya nchi.

Nitatoa mifano michache Mhe. Spika, ili wananchi wajue nchi gani ambazo watu wengi wamekamatwa Watanzaznia wakiwemo Wazanzibari. Nchi ya kwanza nchi ya China peke yake inasemekana kuna wafungwa 200 ambao wamekamatwa nchini China lakini nchini Brazil 12, Iran 63, Ethiopia 7 na Afrika ya Kusini 269 ambayo ndio wengi waliokamatwa**.**

Lakini takwimu hizi zimepatikana na *(Chanzo: Hotuba ya Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa ya Kuahirisha Bunge tarehe 10/02/2017 – Dodoma).* Katika kuthibitisha hili, mnamo mwaka 2013 meli iliyosajiliwa Tanzania (upande wa

Zanzibar- *MV Gold Star)* nayo ilitupa aibu kubwa sana iliripotiwa kukamatwa nchini Italia ikiwa na tani 30 za dawa za kulevya zenye thamani ya paundi milioni 50 (sawa na bilioni 123 za Kitanzania).

Mhe. Spika, kwa pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na nchi mbali mbali duniani kupiga vita biashara haramu ya dawa za kulevya, lakini bado nchi nyingi katika Bara la Afrika ikiwemo Zanzibar zinaeendelea kupata changamoto kubwa inayotokana na uzalishaji, utengenezaji na usafirishaji pamoja na matumizi haramu ya aina mbali mbali za dawa za kulevya zikiwemo bangi, *heroin, cocaine* na mirungi.

Mhe. Spika, mnamo mwaka 2009, Baraza la Wawakilishi la Zanzibar lilipitisha Sheria Namba 9 ya 2009 ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya ambapo Sheria hiyo ilianzisha Tume ya Taifa ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya ya Zanzibar pamoja na kuanzisha Mfuko Maalumu kwa ajili ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya kwa lengo la kuratibu na kuishauri Serikali namna bora ya kudhibiti usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na kuanzishwa Tume hiyo na kuwepo kwa Sheria iliyoweka adhabu kwa watakaokwenda kinyume na masharti ya Sheria hii, lakini bado tatizo la usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya unaendelea siku hadi siku katika visiwa vya Zanzibar ambapo vijana wengi wakiwemo wanafunzi wa skuli mbali mbali wanaendelea kuathirika kutokana na kujiingiza katika makundi ya watumiaji wa dawa za kulevya.

Mhe. Spika, yapo maeneo maarufu ndani ya Zanzibar ambayo yanajulikana kwa kwa kuwa na watumiaji wengi wa dawa za kulevya ambapo kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya ya Zanzibar. Maeneo hayo kwa ruhusa yako niweze kuyataja ili tuone athari kubwa ambazo zimepatikana katika maeneo yale. Mhe. Spika, maeneo hayo ni Kundemba, Mlandege, Miembeni, Mikunguni, Mboriborini, Muembeladu, Muembe Shauri, Jang'ombe, Kinuni, Maumbe Makumbi, Kwahani, Kwaalinato, Mpigaduri, Kiwengwa, Nungwi na Fujoni.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa sababu ya umuhimu wa suala hili na athari zake katika jamii, Sheria hiyo Namba 9 ya 2009 katika kifungu cha 8 inaitaka Tume ya Kuratibu na Kudhibibiti Madawa ya Kulevya Zanzibar, kutoa ripoti kwa umma hali ya kitaifa kuhusu usambazaji na utumiaji wa dawa za kulevya Zanzibar pamoja na kutoa mapendekezo ya namna ya kupiga vita dawa za kulevya na baadae ripoti hiyo iletwe mbele ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwa wananchi juu ya kukithiri kwa rushwa katika shughuli zote zinazohusiana na dawa za kulevya hasa kwa wasafirishaji wa dawa hizo, na hivyo wananchi wengi kukosa imani na vyombo vinavyohusika na utoaji haki vikiwemo Jeshi la Polisi, Afisi ya Mwendesha Mashtaka (*DPP*) na Mahkama, jambo ambalo limepelekea kurudisha nyuma sana juhudi za Serikali katika kukabiliana na tatizo hili na hivyo watuhumiwa wa makosa haya kushindwa kutiwa hatiani na kuadhibiwa kwa mujibu wa Sheria.

Mhe. Spika, pamoja na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kuhakikisha inadhibiti utumiaji na uingizaji wa dawa za kulevya, ikiwemo pamoja na kuanzisha nyumba za kurekebisha tabia (*Sobber Houses)* ambapo kwa sasa zipo nyumba kumi (10) kwa Zanzibar kati ya hizo (08 _ Unguja na 02 – Pemba) kwa ajili ya kuwatoa watu ambao walishaathirika na matumizi ya dawa za kulevya na kuwarudisha katika hali ya kawaida, lakini idadi ya watumiaji inaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Spika, suluhisho sio kuwadhibiti watumiaji peke yake lakini juhudi za ziada zinahitajika kufanywa katika kuwashughulikia wanaoingiza dawa hizi nchini, ambapo tunaamini kuwa kutokana na udogo wa kisiwa chetu watu wanaohusika na kuingiza dawa za kulevya nchini wanafahamika katika jamii, kwani watu hawa ndio ambao wanarudisha nyuma malengo ya Serikali na hivyo Serikali kushindwa kufikia malengo yake.

Mhe. Spika, pamoja na kuwa biashara haramu ya madawa ya kulevya ni suala mtambuka, lakini tunaamini kuwa endapo Serikali itaamua kikweli kweli kukomesha biashara hii nasema itawezekana, kwani ipo mifano ya nchi mbali mbali ambazo zimefanikiwa kukomesha biashara hii katika nchi zao, kwa mfano China.

Mhe. Spika**, k**atika kuthibitisha hoja yangu, nimeweka kiambatanisho ambacho kinaonesha takwimu mbali mbali za kesi za madawa ya kulevya katika Mikoa yote ya Zanzibar kuanzia mwaka 2013 hadi mwaka 2016 ambapo bado takwimu zinaonesha kuwa katika mwaka wa 2016 bado kuna ongezeko la kesi za madawa ya kulevya Zanzibar kulinganisha na miaka ya nyuma. Naomba uniruhusu kwa manufaa ya wananchi wanaotusikiliza nizisome takwimu hizi kwa ufupi kwa kuangalia miaka kama hivi ifuatavyo:

S/NO	MWAKA	IDADI YA KESI ZILIZOFUNGULIWA
1.	2013	166
2.	2014	125
3.	2015	108
4.	2016	170

Unaona ni jinsi gani idadi inavyopanda na inavyozidi kukua**.**

Mhe. Spika, hivyo Basi Mimi, Mohammed Said Mohammed, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Jimbo la Mpendae, chini ya Kanuni ya 27(1)(n), 27(3), 49(1) na Kanuni ya 50 ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012, naliomba Baraza hili tukufu , kwa kutumia uwezo liliyo nayo liridhie kupitisha maazimio kama nitakayosoma hivi sasa:

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba nitoe maazimio haya ili Wajumbe wa Baraza lako tukufu waweze kuichangia hoja hii, lakini wakiona bora tuweze kupitisha maaizimio haya kwa umakini zaidi ili kudhibiti janga hili ambalo kubwa lililotukabili.

Kwa idhini yako naomba kwenda hatua moja baada ya moja na vile vile ningekuomba uniruhusu baada ya michango kama kuna maazimio ya nyongeza niweze kuyasoma ili tuweze kuyapitisha kwa pamoja.

MAAZIMO

1. Serikali ihakikishe kuwa inasimamia bila ya muhali wowote utekelezaji wa Sheria Namba 9 ya 2009 ya Kuzuia Biashara Haramu ya Dawa za Kulevya ili kulinusuru Taifa pamoja na vijana wetu katika kujiingiza kwenye biashara haramu na matumizi ya dawa za kulevya.

2. Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Zanzibar *(ZAECA)* ihakikishe inafuatilia kwa ukaribu kesi zote zinazohusiana na dawa za kulevya ili kubaini wanaojihusisha na vitendo vya rushwa katika kesi hizi, pamoja na kuwachukulia hatua za kisheria kwa yeyote atakayebainika kuchukuwa rushwa.

3. Jeshi la Polisi, Waendesha mashtaka pamoja na Mahkama ziandae utaratibu maalumu ambao utasaidia ushahidi wa kesi za dawa za kulevya kukamilika kwa haraka ili kesi zimalizike kwa wakati na kwa mujibu Sheria ili kurudisha imani kwa wananchi kwa vyombo vyao vya kutoa haki katika kesi zinazohusiana na dawa za kulevya. Kwani takwimu zinaonesha kuwa kiasi ya kesi zisizopungua 294 za madawa ya kulevya bado zianendelea na uchunguzi.

4. Wakuu wa Wilaya, Masheha pamoja na wananchi watoe ushirikiano mkubwa kwa vyombo vya dola kwa kutoa taarifa haraka iwezekanavyo pale wanapobaini vitendo vya uingizwaji au utumiaji wa dawa za kulevya katika maeneo yao.

5. Serikali iimarishe ulinzi ikiwemo pamoja na kununua vifaa vya ukaguzi vya kisasa vikiwemo (*x-ray* mashine na *test kit*) katika maeneo ya usafiri ikiwemo uwanja wa ndege na bandarini ili kuhakikisha kuwa njia hizo hazitumiki kuingiza madawa ya kulevya nchini. Kwani imebainika kuwa maeneo hayo ndio njia kuu zinazotumika kuingiza dawa za kulevya. Mhe. Spika, hii *test kit* nadhani Zanzibar bado haijawahi kuja lakini unaweza ku-*detect* madawa ya kulevya pale pale katika *destination*. Hii itatusaidia sana kuliko kutegemea zile *X-ray machine* ambazo zile za kupekua mizigo haziwezi ku-*detect* mambo ya unga.

6. Serikali itafute suluhisho la kudumu juu ya kukomesha matumizi ya bandari bubu nchini, jambo ambalo pia ni sehemu ambazo hutumika mara kwa mara kuingiza dawa za kulevya ikiwemo bangi na mirungu.

7. Serikali ihakikishe inaleta Barazani Ripoti ya Tume ya Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya Zanzibar ya mwaka 2016, ili kukidhi masharti ya Kifungu cha 8 cha Sheria Namba 9 ya mwaka 2009 na Wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi waelewe kuhusu taarifa zinazohusiana na dawa za kulevya nchini. Mhe. Spika, utakumbuka nilileta baadhi ya vyombo mbali mbali kuleta ripoti zao Bararani na huu ndo umuhimu wake.

8. Pamoja na juhudi za Serikali za kuwatoa vijana katika matumizi ya dawa za kulevya, tunaomba sana Serikali ianzishe operesheni maalumu ya kuwasaka wanawake wote au wale wote wanaotumia dawa za kulevya ili kuwanusuru na janga hili, kwani endapo tutaendelea kulifumbia macho tatizo hili tunaweza tukalikuta kundi kubwa la watumiaji wa dawa za kulevya ni wanawake na wale wengine na hivyo kuipelekea jamii kubwa katika sehemu mbaya zaidi, nimesema wanawake kwa sababu wanawake unapomuelimisha mwanamke mmoja umeelimisha jamii kubwa sana, sitaki kueleweka vyengine lakini nataka kueleweka juu ya mapana mazima ya kuweza kueelewesha jamii hii.

9. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, iandae utaratibu maalumu kwa skuli zote za Serikali na binafsi zilizopo Zanzibar ili kuhakikisha

wanawatambua wanafunzi wote ambao wanatumia dawa za kulevya na hatua zinazo stahiki zichukuliwe kwa mwanafunzi yeyote atakayebainika kutumia dawa za kulevya ili kukomesha matumizi ya dawa za kulevya kwa wanafunzi wote wa Zanzibar.

Mhe. Spika, pamoja na hotuba yangu ya hoja yangu ndefu sana au ndefu kiasi sasa niliombe Baraza lako tukufu kuangalia kwa makini na kisha kuichangia na tukesha tuondoke na maazimio, na kama lipo azimio ambalo wataliotoa Waheshimiwa Wawakilishi niweze kulitoa.

Mhe. Spika, niwashukuru sana Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kunisikiliza sasa naomba kutoa hoja.(*Makofi*).

Mhe. Waziri wa Afya: Naunga mkono hoja.

Mhe. Spika: Waheshimiwa napenda kuwatangazia kwamba wale walioleta maombi wengi wao wako nje, yaani wameleta barua ya kuchangia lakini hapa ukumbini hawapo, baada ya hivyo kuna tangazo dogo ambalo limetoka kwa Mhe. Bihindi Hamad Khamis anawatangazia Wajumbe wote wanaotokea Pemba kwamba mara baada ya kuahirisha mchana wa leo basi mkutane.

Baada ya taarifa hiyo sasa naomba sasa nimuite mchangiaji wetu wa mwanzo Mhe. Zulfa Mmaka Omar, kwa sababu wengi wako nje baadae atafuatia Mhe. Nadir na Mhe. Hidaya Ali Makame ajiandae.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi hii na kuwa mtu wa mwanzo kutia baraka kutokana na hoja hii.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa masikitiko makubwa. Nasikitika kuwa kuna msemo unaosema, "Zanzibar inaeleweka kimataifa kuwa ni njia kuu ya kuingiza madawa ya kulevya". Mhe. Spika, kipindi cha nyuma tulikuwa tunajua kwamba kuna msemo unaosema, "Zanzibar ni njema atakaye aje". Mhe. Spika, sifa yetu hii kwa kweli tunaiharibu, kwa sababu nchi ambazo zitasikia kwamba Zanzibar inaongoza kwa kuingiza madawa haya kwa kweli wale wageni wetu nao wataogopa kuingia kwa sababu mbali mbali.

Mhe. Spika, madawa haya yanaingizwa kwa njia tofauti. Kuna njia ya *Airport*, la kusikitisha Mheshimiwa pale *Airport* kuna *CCTV* ambazo zinaona masuala yote ambayo yanaingizwa, lakini la kushangaza wakati wa kuingiza madawa haya sijui zile *CCTV* zinakuwa zimezimwa au inakuwa hazifanyi kazi, kwa kweli ni mtihani mkubwa, pia madawa haya yanaingizwa katika fukwe zetu.

Mhe. Spika, tukiacha bandari za vichochoroni tunakuta kwamba kuna meli ambazo zinashukiwa za mafuta zinafika Zanzibar na kufunga nanga pembeni baadae kuna *fiber* ambazo zinakwenda katika meli zile na kuchukua mzigo ule wa madawa ya kulevya, hivi Mhe. Spika, ulinzi wetu uko wapi?

Mhe. Spika, tukienda katika zile bandari ndogo ndogo nyingi sana ambazo zinapigiwa kelele kuingiza madawa ya kulevya. Kwa mfano kama ile bandari ya Wesha ukiangalia moja kwa moja unaona kwamba hapa uingizaji wa madawa haya ya kulevya inakuwa ni rahisi, bandari ile kwa mfano asubuhi utakuta kuna watu kuna ulinzi kidogo, lakini inapofika tu muda wa jioni watu wale wanaondoka. Kwa hivyo pale ni njia rahisi wale wanaokuja mfano na majahazi kutoa ile mizigo ambayo wamekuja nayo na kuisambaza nje. Kwa kweli ipo haja kubwa sana ya kuzilinda bandari zetu hizi kubwa na bandari ndogo za vichochoroni ambazo zinaingiza madawa haya ya kulevya.

Mhe. Spika, takwimu zinaonesha kwamba takriban kilo 200 mpaka kilo 400 zimekamatwa ndani ya kipindi cha miaka ya karibuni, hivyo inaonesha kwamba wimbi la uingizaji wa madawa ya kulevya linaendelea na wala halipungui. Mhe. Spika, athari za madawa haya ni kubwa sana na athari za madawa haya hazimfikii mtu mmoja, kama sio mimi muadhirika basi ni wewe muathirika. Mhe. Spika, kwa sababu kama sio mtoto wangu basi itakuwa ni mdogo wako, sio kaka yangu basi itakuwa ni dada yake. Kwa kweli suala hili linaumiza sana. Mhe. Spika, vijana wetu wengi sana sasa hivi wamejikita katika madawa haya ya kulevya si wanaume tu mpaka wanawake, tujiulize hapo mbele nani atakuwa msimamizi wa familia, hapo mbele nani atakuja kuzaa na kupata viongozi bora bila ya kulisimamia suala hili tutabakia na kilio, bila ya kusimamia suala hili, vijana wetu wengi sana watatoka katika masomo na kuingia katika madawa haya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa hivyo tuiombe Serikali, tunajua kwamba wana kazi kuwa wanayoifanya kupigania juu ya madawa ya kulevya, lakini tuseme kwamba tuzidishe juhudi za hali ya juu. Mhe. Spika, mwanadamu tumeumbwa katika umbile ambalo liko zuri lakini la kusikitisha sasa hivi mwanadamu yule yule ambaye kaumbwa katika umbile lile la uzuri, uzuri wetu tunauharibu kutokana na madawa haya. Mhe. Spika, ukienda Miembeni kwa mfano au ukienda pale Pemba Afrikana unakuta vijana wazuri, watanashati, lakini uzuri wao ule wote umeharibika kutokana na madawa ya kulevya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, vijana wale walikuwa wanategemewa katika familia zao lakini sasa hivi tunakuta kwamba kuna wimbi kubwa la walemavu. Kwa mfano pale Chake Chake, mimi tu vijana ambao nawajua wamepata ulemavu wa miguu

wanne kutokana na madawa ya kulevya. Kwa kweli suala hili linauma sana na kila siku suala hili linaendelea. Mhe. Spika, kwa kweli mtihani huu si wa mtu mmoja, mtihani huu ni wetu sote. Suala hili la uingizaji wa madawa ya kulevya kuna makundi matano. Kuna watumiaji wale ambao tunawakuta barabarani wanasinzia na kubaka baka ovyo, hao Mhe. Spika, ni tabaka dogo. Kuna wasambazaji wadodo wadogo.

Mhe. Spika, tukitoka kundi la tatu, kuna makontena. Haya makontena ni wale ambao wanazimeza dawa kwa njia ya pipi au wanaingiza madawa yale katika miili yao kupitia sehemu za haja kubwa, hawa tunaamini kwamba wapo na wanakamatwa lakini mwisho wake hatujuwi wapi wanafikia.

Mhe. Spika, tukitoka hapo kuna kundi moja ambalo hili ni hatari zaidi ni kundi la matajiri. Hawa matajiri ndoyo ambao wanaingiza mzigo mkubwa wakifika hapa wanawapa wasambazaji wadogo wadogo, lakini tunakuta kwamba wale watumiaji wanakamatwa na kupelekwa Polisi au Mahakamani, lakini hatujawahi kusikia hata siku moja tajiri mkubwa kakamatwa na kupelekwa Mahakamani. Mhe. Spika, hawa wadogo wadogo kwa kweli tunawaonea, wakamatwaji ni hawa wakubwa ambao tunawatambua wanaingiza. Kuna matajiri wanaosifika hasa kwa uingizaji wa madawa ya kulevya lakini matajiri hawa tujiulize kitu gani wanafanywa? Hamna kitu chochote, tukiwaacha hawa matajiri Mheshimiwa mimi naamini kwamba hatutoweza kulimaliza suala hili.

Mhe. Spika, naomba nitoe mfano kwa kule Pemba. Katika Mahakama zote Pemba ambazo zinashughulikia kuendesha kesi za madawa katika miaka mitatu kutoka 2014-2016 takriban kesi 77 za madawa ya kulevya zimekamatwa, katika kesi hizo 77 kesi 56 zimeshamalizika, kesi 21 zinaendelea. Kitu cha kushangaza na cha kusikitisha na cha kuvunja moyo, katika kesi 56 zilizomalizika kesi 5 tu ndizo ambazo zimepatiwa hatia. Hii inaumiza sana. Hivi kesi 77 zinapelekwa na mwisho wake Mhe. Spika, tunakuta kwamba kesi 5 tu, hapa tujiulize kweli jamani watu wa Mahakama, watu wa Polisi, Serikali, suala hilo tukilinyamalizia litamaliza! Kutoka twakwimu ya kesi 77 kwa miaka mitatu, mimi naamini kwamba kesi 77 ni kidogo sana lakini kama ni kidogo hiyo 77 tukitizama kwamba kesi zilizotolewa hukumu ni kesi 5. Mimi niseme kwamba askari wanaohusika na kukamata madawa haya na hichi chombo maalum ambacho kimetungwa niseme bado kazi wanaifanya lakini naamini bado hawaja na utayari wa zaidi sana.

Mhe. Spika, tunashuhudia kwamba tunakuta watu wengi, mimi kwa macho yangu nishawakuta askari katika eneo langu la Madungu wanakuja wanamkamata mtu. Kwa mfano kuna siku alikuja Dada X mmoja anakamatwa

ana kete 85 za unga, dada yule alikamatwa akapelekwa mpaka Polisi. Siku ya pili dada yule akapelekwa Mahakamani, Mahakamani alikaa wiki mbili badala ya huku na huku baada ya wiki mbili kijana yule katolewa hadi leo kesi ile imenyamaziwa, hatma yake siye vishihata ambao tulikuwa tukenda kuifuata kesi ile tumeonekana kwamba wabaya na kutishia amani yetu. Mimi nipo tayari kuuliwa, kupigwa, kususiwa, kufanywa kila kitu kutokana na madawa ya kulevya. Niiombe Serikali mimi niko tayari muda wowote, kuwafichua ambao wanaingiza madawa na kuwafichua ambao wanauza madawa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, tukiwaonee watumiaji wa madawa, wakukamatwa ni waingizaji wa madawa. Haya ni manyangumi yapo na yanajulikana na yanashirikiana na baadhi ya askari wetu kwenda kuchukua pesa. Mhe. Spika, kwa mfano pale Mtoni kuna askari kila siku unawakuta wao wanapita wanakwenda katika nyumba inayoshukiwa inauzwa madawa, wanakwenda kufanya nini? Kama ni salamu wanakwenda kusalimia, kwa nini wasipigiane simu. Mhe. Spika, tujiulize sisi wenyewe kwa sababu mtu anashukiwa anauza madawa ya kulevya, halafu leo wale wale wanakwenda asubuhi katika nyumba ile unaona kwamba wanaingia pirika hizi na hizi bila ya kukamatwa. Suala hili linauma sana. (Makofi).

Mhe. Spika, niseme kwamba watu wote humu ni waathirika wa madawa ya kulevya, utakuta kwamba mikakakati mingi sana inaweka juu ya madawa ya kulevya, mikakati ile inakwenda kwa wiki moja tu ikimaliza wiki moja unakuta kwamba ziii! limenyamaza. Tunaiomba serikali ikisikilize kilio hichi. Mhe. Spika, suala hili mimi nalisema kwa uchungu sana kwa sababu mimi mwenyewe ni muathirika wa madawa ya kulevya. Mhe. Spika, tushapeleka kesi nyingi sana kuhusiana na madawa ya kulevya. Mimi mwenyewe mdogo wangu wa damu ambaye peke yake mwanamme katika tumbo letu alikuwa ni muathirika wa madawa ya kulevya, unakwenda Polisi unasema kwamba namshuku fulani kwamba ni muuzaji wa madawa ya kulevya, kwa sababu fulani na fulani. Mhe. Spika, mtu yule yule katika nyumba zile zile ambazo tunazishuku mara nyingi anakamatwa na vitu vya wizi. Hivi tujiulize serikali tunafanya nini Mhe. Spika, wanatuuwa wauzaji wa madawa hawa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi naiomba sana serikali iangalie tena, najua kwamba na wao pia wanaumia kwa sababu hili suala la madawa ya kulevya ndilo pia linalosababisha udhalilishaji. Mtu akishakuvuta madawa ya kulevya ndiyo unamkuta kichochoroni anatuibia, mara anatuanulia nguo, mara anafanya wizi. Mhe. Spika, tusiposimamia juu ya madawa ya kulevya, tusipopiga kelele juu ya madawa ya kulevya, naamini kwamba udhalilishaji utazidi kwa asilimia mia tatu sio mia moja. Mhe. Spka, niiombe tena serikali madawa yanatuuwa

Mheshimiwa. Leo hii unaniona mimi kwamba Zulfa niko vizuri, kesho tu nikitumia pesa yangu kwenda kuingia madawa ya kulevya Mhe. Spika, naamini ukiniona nje utanikimbia. Sasa tujiulize kuna faida gani? Hakuna faida hata moja juu ya suala hili.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa hivyo tunawaomba Waheshimiwa, tunawaomba wote ambao wameguswa na suala hili tushirikiane, tuseme madawa basi, tuwafichue, tuwapeleke katika vyombo ili na wao tuangalie serikali, kwa sababu serikali tusiiachie mzigo peke yake na sisi tunatakiwa kushirikiana na serikali kuwatoa wale ambao wanahusika na haya madawa, tuache kwamba tunailaumu tu serikali. Serikali inaamini kwamba na wao pia wanaumia na suala hili. Kwa hivyo niwaombe Waheshimiwa wenzangu tushirikiane kila mmoja katika jimbo lake, naamini kwamba anajua nyumba fulani na mtu fulani analeta unga, tukishakushuku vile inaenda pale serikali inaangalia, mtu yule tumempeleka kafanyiwa uchunguzi sawa uchunguzi ule ndio kagundulikana kwamba yupo katika kesi ile tuangalie ni hatua gani itachukuliwa. Mhe. Spika, ikiwa kama haikuchukuliwa hatua mimi naomba uturuhusu turudi tena hapa tuje tusema kwamba fulani tulimshuku na fulani tulimtaja lakini hakuchukuliwa hatua yoyote.(*Makofi*).

Mhe. Spika, hivyo niwaombe, Waheshimiwa tuungane hichi kilio ni chetu sote na hichi kilio sote kinatuumiza. Kwa hiyo niwaombe sana tushirikiane na serikali tuwatoe hawa madudu ambao wanataka kuimaliza Zanzibar yetu na kuipa sifa chafu Zanzibar yetu, kuhusiana na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika kwa kweli mimi nina uchungu. Mhe. Spika mimi nahisi niunge mkono hoja hii, naunga mkono hoja hii.

(Hapa Mheshimiwa alitokwa na machozi kwa uchungu)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka Omar. Mheshimiwa Zulfa umechangia muda wa dakika 15 juu ya alama, nashukuru sana kwa matumizi yako ya muda na nashukuru kwa mchango wako.

Waheshimiwa naomba kuwatangazia zaidi hawa *sergeant at arm* vinakuja vikaratasi vingi sana hapa mezani lakini vya watu ambao wako nje kabisa ya Baraza. Kwa hivyo nadhani hali hii kiongozi wa *sergeant at arm* ajaribu ku-*control*, vibarua vya watu ambao wapo nje ya Baraza, watu ambao si Waheshimiwa visije huku kwenye kiti, wakati tunaendesha Baraza wajitahid sana kwa hilo.

Baada ya hapo Waheshimiwa kuna taarifa ya msiba ninadhani unamuhusu Mhe. Abdalla Maulid Diwani na baadhi ya Waheshimiwa watakuwa wametoka kwa ajili kwenda kumsaidia. Kwa hivyo taarifa kamili zitakapokuja tutatoa tangazo lililokamilika.

Lakini kwa wale waliopo naomba sasa nimwite Mhe. Nadir simuoni kwa hivyo badala yake nitamwita Mhe. Hidaya Ali Makame, lakini niwatangazie kabisa watakaofuata ni Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis, Mhe. Asha Abdalla Mussa, Mhe. Mtumwa Suleiman Makame halafu tutaendelea.

Mhe. Mwantatu tafadhali.

Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi nikaweza kuchangia hoja hii.

Baada ya kukushukuru weye Mhe. Spika, nimshukuru mwakilishaji wa hoja hii Mhe. Mohamed Said Mohammed kwa kuona uzito wa suala hili na akaona ailete hoja hii ambayo ni muhimu kwa maslahi yetu na vizazi vyetu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, vijana ni taifa letu ambalo tunalitegemea na hivi sasa kila siku zikienda vijana wengi wanajiingiza katika dimbwi hili na utumiaji wa madawa ya kulevya. Kibaya zaidi madawa haya si kama yanauzwa katika maeneo maalum, sasa hivi madawa haya yanauzwa mpaka katika maskuli ambapo tunategemea vijana wetu wanakwenda pale kupata elimu ili waweze kuja kujitegemea baadae waongoze taifa hili, lakini sasa biashara hii imekuwa inapelekwa mpaka maskulini. Labda tujiulize, je, taifa letu tunalipeleka wapi na ukiangalia athari inazidi kubwa. Labda nielezee tu baadhi ya athari zinazosababishwa na utumiaji wa madawa ya kulevya.

Kwanza kuna ongezeko kubwa la watu wenye ulemavu. Mhe. Spika, tukitizama vijana hawa katika utumiaji wao wanakuwa wanapoteza nguvu kazi, yaani wanapoteza nguvu za kufanya kazi mwanzo atajikaza lakini mwisho kutokana na ubaya wa madawa haya wanakuwa hawana hata uwezo wa kufanya kazi, ndio pale wanapojikuta wanajitia katika masuala ya wizi. Wanapojiingiza katika masuala ya wizi wanakutana na mambo mbali mbali, wanapigwa na kupewa ulemavu wa maisha kama alivyozungumza mchagiaji aliyetangulia wengi utawakuta sasa hivi ni walemavu wa viongo.

Lakini vile vile suala hili linaathari kubwa la ongezeko la wagonjwa wa akili, wanatumia madawa vijana na baadaye tunawakuta au wanajikuta tayari

wameshaathirika akili zao. Kwa hiyo wengi wanakuwa wanapata matatizo ya akili.

Lakini Mhe. Spika, vile vile kuna athari inayowapata familia. Familia zinaathirika kisaikolojia kwa sababu unapokuwa na kijana ambaye atatumia madawa basi yule mzazi akili yake saa zote inakuwa iko kwa yule mtoto tu, hafikirii kitu chengine kwa sababu anajua kutokana na mambo anayoyafanya, kutokana na matumizi dawa anayoyatumia, kuna mambo mawili yatamtokezea, kupata ulemavu au kifo na kwa kweli wanapigwa vibaya na wanaumizwa vibaya.

Mhe. Spika, lakini chengine kifo ni haki ya kila mtu na, "*Kullu nafsi dhaikatul mauti*", lakini vijana wanaotumia madawa wanauliwa kwa vifo vya kikatili, wanachomwa moto vijana hawa, wanapigwa mapanga, lakini vile vile wakati mwengine wananyogwa tu wakatupwa. Kwa sababu jamii inakuwa ishachoshwa na vile vitendo vyao, lakini bila ya kujua kwamba tunawahukumu kwa kosa ambalo ninasababishwa na nani.(*Makofi*).

Mhe. Spika, utumiaji huu wa madawa, taifa letu linakosa nguvu kazi. Kwa sababu sasa hivi kuna vijana wengi kuanzia miaka tisa, kumi na kuendelea wanatumia madawa na ubaya wa hawa wenzetu wanaofanya hizi biashara zao hawaangali hata wa kumuuzia. Mtoto wa mwenzio wa miaka tisa unakwenda kumpa madawa ambayo unahakikisha kwamba haja madawa yatamuathiri, wao hawaliangalii hilo. Mhe. Spika, ni jambo la kusikitisha sana, tuliopo hapa wengi wetu tumeshaathirika, kama si mwanao ni ndugu yako, kama si ndugu yako ni mtoto wa jirani yako, wote ni wako. Mhe. Spika, na akitumia madawa mtoto wa jirani yako basi wewe jirani huna raha kwa sababu unajua wakati wowote na wewe atakuathiri. Kwa hivyo Mhe. Spika, hili jambo ni zito na linahitaji juhudi kama alivyotoa maazimio Mhe. Mohammed Said Mohammed, linahitaji juhudi lakini vile vile linahitaji mikakati ya hali ya juu ili tuweze kudhibiti na kunusuru vizazi vyetu lakini vile vile na kujinusuru sisi wenyewe.

Mhe. Spika, mimi sikubaliani na watu wanaosema kwamba utumiaji wa madawa unasababishwa na ukosefu wa ajira, si kweli. Kwa sababu kuna vijana ambao tayari wapo maskulini wanajiandaa ili kufikia huko kwenye ajira, hawamalizi hata masomo wanaanza kutumia haya madawa, mtoto wa miaka tisa ajira gani anayoitaka na nyumbani anahudumiwa kila kitu, mtoto wa miaka kumi mbili anahudumiwa kila kitu na familia, ajira gani aliyoikosa ikamsababishia kutumia madawa yale. Lakini Mhe. Spika, kuna wengine wanakuwa matajiri, wanamiliki majumba, wanamiliki magari, wanamiliki vitega uchumi chungu mzima lakini wanajikuta wanakuwa maskini wanarudi

kama walivyozaliwa "alif", wanaanza moja. Kwa hivyo mimi sikubaliani kabisa kusema kwamba ukosefu wa ajira ndiyo unaosababishwa utumiaji wa madawa ya kulevya, naona huu ni mtihani tu Mwenyezi Mungu ametuletea. (*Makofi*).

Mhe. Spika, tunahitaji kutumia juhudi zetu zote, tuwe na mashirikiano ya pamoja ili kuhakikisha suala hili tunalitokomeza. Mimi nitoe ushauri kutokana na kuwa vitendo hivi vinaongezeka na kwa kuwa kuna Kitengo ambacho ni cha askari Polisi hawa, pale pana Kitengo cha Udhibiti wa Madawa ya Kulevya. Kitengo hichi niiombe hii ZAEKA kufanya kazi ya kufuatilia kitengo hiki kwa karibu. Kwa sababu haiwezekani Kitengo hiki kipo lakini tunazozisikia kesi ni za wale watumiaji tu. Hawa watumiaji wanaupata wapi? Kama hawa wangelikuwa wanawatumia hawa watumiaji kwa kueleza wapi wameupata basi na hawa wasambazaji na wauzaji wangekamatwa. Lakini mimi nina wasi wasi kabisa na hichi Kitengo, haiwezekani kitengo hiki kipo na kinafanyakazi hiyo na hii hali ikaongezeka. ZAEKA wafanye kazi karibu na hichi Kitengo.

Mhe. Spika, katika azimio la nane katika hoja hii linasema kuwa, "Serikali ianzishe operesheni maalum ya kuwasaka wanawake wote wanaotumia dawa za kulevya ili kuwanusuru na janga hili".

Mimi Mhe. Spika, nilipongeke hili lakini si kwa wanawake tu, kwa wote wanaotumia lakini vile vile Serikali iandae utaratibu wa kuwadhibiti wale vijana ambao wanatumia, kwa sababu watakapodhibitiwa wale, hawa wanaouza soko lao litapungua watakuwa hawana wakuwauzia. Lakini vile vile wakidhibitiwa wale, wale wale watatusaidia kumjua nani na nani, nani anaingiza, nani anasambaza, nani yuko wapi, vipi tutamkamata.

Kwa hivyo niombe sana serikali kulizingatia hili, jamani tunaumia, jamani tunaathirika, kila unapopita na cha ajabu Mhe. Spika, ukipita tu mazingira yanakwambia, hapa pana jambo fulani, tatizo liko wapi. Katika hoja yametajwa maeneo mbali mbali lakini kuna eneo la Meli-nne/Uzi, huko mtoto mdogo anayenyonya anatumwa akanunue unga, kuna maduka chungu mzima, tunaumia wazazi watoto wanateketea taifa linateketea.(*Makofi*).

Mhe. Spika, naomba niunge mkono hoja.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis. Sasa naomba nimwite Mhe. Hidaya Ali Makame nimekuona atafuatiwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa na Mhe. Mtumwa Suleiman Makame ajiandae.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuweza kuchangia hoja hii ya Mjumbe kuhusiana na ongezeko la uingizaji na utumiaji wa madawa vya kulevya.

Mhe. Spika, kwanza napenda nikiri kwa hii hoja ya Mjumbe kwamba Mjumbe huyu ameona mbali, na Mjumbe huyu hajakurupuka juu ya suala hili la uingizaji na utumiaji wa madawa ya kulevya. Katika nchi yetu hii ya Zanzibar suala la uingizaji na utumiaji wa madawa ya kulevya lipo na kila mtu analijua na kila mtu anaona kwamba hili suala lipo na linafanyika. Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba suala la uingizaji wa madawa ya kulevya tunayoyaingiza madawa haya ya kulevya ni sisi wananchi, lakini pia tunayoyatumia ni sisi wananchi, sikuyatumia mimi basi kaka yangu, baba yangu, dada yangu moja ndani ya famili lazima hili suala limemgusa au kwa sote limetugusa.

Mhe. Spika, hili ni janga ambalo kwa kweli sasa hivi linatuathiri ndani ya akili zetu na linatusababishia matatizo makubwa sana yakiwemo ya udumafu wa akili lakini pia maharibiko ya saikolojia ya akili kupotea pia na kuwa haifanya kazi, kwa sababu mtumaji wa madawa na kulevya tunafahamu mwisho wake anakuwa kama ni chizi au mwendawazimu kutoka lile suala ambalo analitumia liko tofauti na maombile yake au liko kinyume na hisia za binadamu.

Mhe. Spika, tunafahamu kwamba madawa ya kulevya ni athari kubwa sana kwa jamii lakini tunafahamu kwamba madawa ya kulevya ni tatizo sugu juu akili na afya pia ya mwanadamu, tukienda mahospitalini lakini tukienda kwenye tiba za aina yoyote tunambiwa kwamba hili suala halitufai sisi wanadamu kulitumia, na tunafahamu kwamba madawa ya kulevya yako ya aina nyingi na kila mtu ana ulezi wa aina yake. Lakini tu suala la madawa ya kulevya sio kama ndio ulevi ambao ule ulozungumzwa kwamba kila mtu ana ulevi wa aina yake tunafahamu kwamba kuna ulevi wa aina nyingi. Kuna wengine wakila muhogo tu hapa wanalewa, kuna wengine wakila shelisheli wanalewa, lakini suala la madawa ya kulevya nafikiri hakuna hata binadamu mmoja ambaye anaweza akalitumia lisimuathiri tofauti na ule muhogo au viazi au haragwe ambazo kila mmoja wetu zikaweza kumletea athari ndani ya mwili wake, tunajua zile ni athari za kawaida na za kibinadamu lakini ni tofauti na haya madawa ya kulevya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, madawa ya kulevya yanaingizwa ndani ya nchi yetu kwa kupitia njia tofauti zinatumika kuingizia madawa haya. Mhe. Spika sisi tunaoishi huu mwambao wa pwani pwani huku kwenye kanda za bahari, tunakumbana na hizi changamoto nyingi na kuona haya masuala yakikithiri katika jamii zetu. Mhe. Spika, mimi ninaishi ndani ya kijiji cha Nungwi naona matukio mbali mbali

yanayotokea kutoka na hawa watumiaji wa madawa ya kulevya, lakini pia na kutokana na huu uingizaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kule kwetu Nungwi sasa hivi kuna gari hizo ambazo zinapita tu muda wa saa 6:00 usiku, gari hiyo ikipita basi watoto utawasikia hee! gari ya 6:00 hiyo na gari hiyo *speed* yake inakuwa haisemeki wala mwendo wake hausimamiki, hujui gari hiyo inakwenda wapi na inaendea kufanya nini, wanaojua ni wao wenyewe.

Mhe. Spika, haya mambo yapo yanafanyika lakini tu kwa kuzingatia ndani ya vijiji hivi au ndani ya Shehia hizi au ndani ya nchi hii kuna vyombo vya ulinzi na usalama ambavyo vimewekwa kwa ajili ya kazi hii kulinda na kutetea haki za wananchi. Lakini je, tuseme kweli haya masuala yanayofanyika hawayaoni hatuwezi kujua, wanajua wenyewe na Mwenyezi Mungu ndiye anayewaona. Kwa sababu kama umepewa dhamana ya kulinda na kutetea, basi uisimamie dhamana ile lakini ukumbuke kwamba iko siku utakwenda kuulizwa juu ya ile kazi uliyopewa uifanye na uisimamie, kwa hiyo utakwenda jibu mbele ya haki kwa kazi hiyo kwa hiyo. Mhe. Spika, tuwaombe tu wenzetu hawa waliopewa kazi hii na kuipuuza na kuiona kwamba haina maana hapa tunapita lakini huko tunakokwenda mbele ya haki ndiko kwenye mahesabu kamili na mtu ndiko atakako kwenda jibu. *(Makofi)*

Mhe. Spika, tunaoathirika zaidi ni sisi vijana hususani kuanzia miaka 15 kuendelea mpaka miaka 40, mzee anapo yafanya haya, anafanya kwa kujua lakini pia kwa kujitakia. Lakini kijana akiwa kama kijana kuna changamoto nyingi ambazo zinamsababisha kuyatumia madawa ya kulevya, zikiwemo za upungufu pia wa kutokuwa na muhimili wa kushika juu ya masuala yake ya kimaisha lakini pia na mchanganyiko wa mawazo, wenyewe wanasema kwamba unapokuwa na *stress* nyingi ukizipata zile mbili zinapunguza. Mhe. Spika, hili si kweli na kuna mambo mengi tu ambayo yanaweza kukuondoshea *stress* zako za kimaisha na ukaweza kuendelea na maisha yako kama kawaida lakini sio kuvuta madawa ya kulevya au kutumia madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kwenye hoja ya Mjumbe hapa kalizungumzia suala la *sober house.* Mhe. Spika tunafahamu kwamba nchi yetu hii kuna hili suala la *sober house* ambalo limeandaliwa kwa ajili ya hawa watumiaji wa madawa ya kulevya ili eti warekebishwe tabia, siyo kweli kwamba *sober house* zinarekebisha tabia. Hili suala mimi napinga kwa sababu ndani ya hizi *sober house* watumiaji wa madawa ya kulevya ambapo wanamoenda kuwekwa ili warekebishike zile tabia ndio huko huko yanakopelekwa haya madawa ya kulevya. Mhe. Spika, utamkuta mtu yumo ndani ya *sober house* lakini hajaacha wala hajasahau

kutumia madawa ya kulevya. Je, tunajiuliza hizi nyumba zimewekwa kwa ajili ya kurekebisha tabia au hizi nyumba zimewekwa kwa ajili gani, hatuwezi kujua lakini si kwa ajili ya kurebisha tabia.

Mhe. Spika, tunafahamu hizi nyumba zimewekwa ili watu waweze kuongeza mapato yao ya kiuchumi au ya kimaisha kwa sababu kama kweli ingekuwa zimewekwa kwa ajili ya kurekebisha tabia haina haja tena kule, yule mtu ambaye tayari kishapelekwa kwenda kurekebisha ile tabia, ukamkuta bado anaweza kulitumia hili suala, je, limefikaje kule wakati kule yuko mtu kapelekwa kwa ajili ya kupata tiba. Hivyo kweli mgonjwa umemtoa nyumbani anaugua tetekuwanga umempeleka hospitali bado unakwenda kumuweka na wale wale wanaoumwa tetekuwanga halafu humpi dawa, huyu mtu atapona au atakufa?

Mhe. Spika, kwa kweli hili suala hatujalikalia kitako na hili suala kiufupi tunataka liendelee ndani ya nchi yetu, kwa sababu kama hatutaki liendelee ndani ya nchi yetu basi hivi vyombo ambavyo vipo, vikiwemo ni vya ulinzi vifanye kazi yake ya ulinzi na usalama kwa ajili ya kuyalinda haya na kuyatetea kwa sababu sifahamu, sijui kwamba hawawezi kujua hizi njia ambazo zinatumika kuingiza madawa ya kulevya, njia ziko nyingi ambazo zinatumika. Kuna njia za bahari, bahari ambayo sasa hivi ina kila aina ya njia ambazo zinatumika kwa ajili ya kuingizia hivi vitu.

Kuna madiko kuna hata kwa jina jengine sijui niyaitaje, yaani ndio wao wanaweka hizi *special* kwa ajili bandari zao huru yaani wanaziita huru kwa ajili ya mambo yao hayo, wakati ukiangalia bandari hizi sio huru na si salama. Lakini kama ni huru na salama kwa nini hawayafanyi kila sehemu haya masuala yakaonekana, wanafanya muda wa usiku lakini na muda ambao wanajua sasa hivi hata nikienda kule hakuna atakayeniona na hata kama yupo hana uwezo wa kunifanya chochote.

Mhe. Spika, hili jambo linatuathiri na kwa kweli linatuvunjia amani ya nchi yetu kwa sababu hatuishi kwa amani wala hatufanyi yale masuala ambayo tunaweza tukafanya mtu akajisikia kama kweli mimi niko huru ndani ya nchi yangu, kwa kuhofia tu mimi hapa nikaweza nikafua nguo yangu ya maana nikaiyanika lakini hapo hapo akapita mla unga akaichukua. Lakini mimi hapa ninaweza nikakaa kwenye nyumba yangu hii nikalala mlango wazi kwa kuhofia kwamba hawa watu watakuja muda wowote waingie wavunje wafanye kila kitu.

Mhe. Spika, kwa kweli suala hili tunahitaji kama ni viongozi tukae chini tulitafakari na tutafute njia mbadala ya kufanya juu ya suala hili la uingizaji na utumiaji madawa ya kulevya, kwa sababu tunamini kwamba tukishalidhibiti hili la uingizaji, basi mtumiaji hana njia ya kutumia kwa sababu atalipata wapi. Wakati huku ushafanya njia zote umeshazuia kwamba haya masuala yasiingie ndani ya nchi hii. Jee, yule mtumiaji wakati na yale mengine ambayo yapo ndani ya nchi kushayadhibiti umeshayachoma moto umeshayaweka pahali ambao hapastahiki, yule mtumiaji anapata wapi na si kweli kwamba vijana wetu wanafanya hivi kama alizungumza Mhe. Mwantatu kwa ukosefu wa ajira au kwa kuwa labda mtu yule ni maskini. Mhe. Spika, tunafahamu kwamba hao watu ambao wana uwezo kwa sasa hivi au hao vijana ambao kuna uwezo basi wao ndio watumiaji wakubwa wa madawa ya kulevya kulikoni hata hao wanonekana ni maskini.

Mhe. Spika, maskini anaweza kutumia madawa ya kulevya lakini tofauti na wale ambao wana uwezo kwa sababu yule mwenye uwezo anajua yeye akienda kwao akidai chochote atapewa ili aende akatumie, lakini maskini na mimi kama hajaenda kuparamia mnazi wa watu na sasa hivi ana uhakika akienda kuiba nazi atafungwa jela miezi mitatu au miaka mitatu inakuwa ni tofauti. Kwa hivyo, hawa ambao wana pesa zao ndio ambao wanasabisha hili janga kuenea kutokana na ile pesa kwa sababu tunajua kwamba *cocaine* au *heroin* au chochote kidonge au sindano huwezi kuipata kama huna pesa, utaipata wapi na wakati huna pesa. Mhe. Spika, kwa kweli hili suala ni kubwa na ni zito ndani ya nchi yetu. Mimi ningeiomba tu Serikali yetu ya Zanzibar ambayo inasimamiwa na Rais wetu makini Mhe. Dk. Ali Mohamed Shein, alione suala hili na auone uzito wa suala hili juu ya uingizaji wa madawa ya kulevya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, waingizaji wapo na wanajulikana wadhibitiwe, wakishadhibitiwa hawa mimi sifikirii ndani ya nyumba ukishamkamata baba, mtoto hana fursa ya kuweza akaku-*force* wewe wakati yule baba tayari umeshamkamata umeshamdhibiti. Mhe. Spika, tunajua kwamba ndani ya nyumba baba ndiye mwenye nguvu zote na baba ndiye mamlaka na ndiye mwenye uwezo wa kusema kila kitu kikasikilikana na kikafanyiwa kazi. Kwa hivyo tungemuomba Mhe. Rais wetu alisimamie suala hili kama anavyofanya kulisimamia na kuweka hizi *sober houses*, basi alisimamie ili hawa wanaoingiza waweze kudhibitiwa na waweze kukamatwa wawekwe kwenye vifungo vya maisha. Kwa sababu tukiwaachilia mpaka huyo Mwenyezi Mungu ambaye katushusha ndani ya ulimwengu huu, basi hayuko radhi na siye, ndio maana mjanga mengi yanatokea kutokana na suala hili kwamba hatuko makini na kile ambacho tunakifanya lakini tunapinga na maamrisho yake.(Makofi).

Mhe. Spika, mimi nisingependa kuzungumza mengi juu ya suala hili kwa sababu kwa kweli hata uzungumze vipi, basi unaona kama hujafikia hata ile robo ya hili suala, linatuumiza na linatunyanyasa na linatukosesha raha kweli ndani ya nafsi zetu.

Mhe. Spika, mimi niunge mkono hii Hoja ya Mjumbe kwa asilimia zote ahsante.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Hidaya Ali Makame. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Asha Abdalla Mussa atafuatiwa na Mhe. Mtumwa Suleiman Makame na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf ajiandae.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Spika na mimi kunipa nafasi hii ili kuchangia machache katika hoja ya Mjumbe inayohusiana na ongezeko la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza kaka yangu Dimwa kwa kuleta hoja hii na pia kutoa maazimio ili nasi tuweze kumuunga mkono. Mhe. Spika, kila Mjumbe atakayesimama natumai atajirudia maneno yale yale, lakini mimi niende kwenye njia ambazo wanazotumia watumiaji wa madawa ya kulevya. Ninavyofahamu mimi ni njia mbili ambayo wana njia ya kunusa lakini pia kuna njia nyengine ambayo wanatumia ya kujidunga sindano.

Mhe. Spika, njia hii ya kujidunga sindano kwa kweli inaathiri mambo mengi na inasabishia kwamba watumiaji wa madawa haya kuwapelekea kuwa na maambukizi mapya ya virusi vya ukimwi. Mhe. Spika, kwa kweli suala hili linatisha tena linatisha. Mhe. Spika, niungane na wenzangu kwamba tutafute mikakati na kuona kwamba suala hili linamalizika hapa kwetu Zanzibar. Nimpongeze sana Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi Mhe. Ayoub kwa kuamua kwa makusudi kuanza operesheni ya kutafuta hawa wafanya biashara wa madawa ya kulevya, na tumeona tumeshuhudia kwamba wahusika na wao pia wamo humu Jeshi la Polisi nao wanahusika lakini na wengineo. Kwa hivyo, tuone kwamba suala hili bado halijafikia muafaka kwa kuweka mikakati maalum ya kuhakikisha kwamba linaondoka.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya nyengine nao pia wafuate nyayo zake Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi, na tukifanya hivi basi tutahakikisha kwamba hawa maadui zetu wanaoleta unga hapa katika visiwa vyetu hivi wanatatafuta pa kuelekea na kuona wanapeleka sehemu nyengine.(*Makofi*).

Mhe. Spika, wafanyabiashara hawa wanakimbia Dar es Salaam, wanakimbilia hapa Unguja na kwa sababu tu hakuna njia ya kuonesha moja kwa moja hawa wanaoleta unga huu hapa Zanzibar.

Mhe. Spika, lakini pia tumeshuhudia kwamba vyombo vya habari vikitangaza kwamba wamekamata bangi lakini wanapokamata wakipelekwa sehemu husika, na badala yake wanaambiwa hii si bangi ni majani tu ya kawaida. Kwa kweli suala hili linasikitisha sana Mhe. Spika, tunasema bado hatujawa tayari.

Mhe. Spika, lakini pia kuna maeneo mfano Kiwengwa, kuna vibanda vidogo vidogo ambavyo havina maana yaani hujui hasa kibanda hiki kinafanya shughuli gani, lakini tunavitizama tu. Ningeiomba Serikali kupitia Halmashauri zilizopo zihakikishe kwamba inafanya *operation* mkubwa katika maeneo yao ili kuhakikisha nyumba ambazo zipo tu hazijulikani kazi gani ambayo zinafanya basi zihakikishwe kwamba zinaondoshwa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, wanaotumiwa kuingiza madawa haya ya kulevya ni wanawake. Wanawake wengi ndio wanaotumiwa kuchukua unga na kuingiza katika eneo hili, kwa sababu kwamba utakuta mwanamme yeye kwanza anakuwa wakati mwengine anasuasua, anaogopa lakini mwanamke anajidhatiti kabisa kwamba mimi naweza kuchukua mzigo huu na kuupeleka sehemu nikaufikisha kwa sababu tu ya tamaa. Mhe. Spika, nitoe wito kwa wanawake wenzangu kwamba sasa basi wakati umefika sasa na sisi tubadilike kitabia.(*Makofi*).

Mhe. Spika lakini pia utakuta Shekhe kavaa kanzu vizuri tu lakini kumbe ndani ya kanzu ile kwenye mifuko kabeba unga. Mhe. Spika, masuala haya yapo na tunayaona lakini tunayanyamazia. Mhe. Spika, niendele na kusema kwamba waletaji unga hapa Zanzibar ni watu wenye pesa zao na sio kama hawajulikani wanajulikana lakini Serikali bado inawaachia.(*Makofi*).

Mhe. Spika, tuungane na kaka yetu Dimwa tuhakikishe kwamba maazimio ambayo tutakayo yatoa hapa basi yachukuliwe hatua na yatekelezwe.

Mhe. Spika nimalizie kwa kusema kwamba kuna dawa hizi ambazo wanatumia wagonjwa wa akili Hospitali ya Kidongochekundu, kuna baadhi yao kuna ma-*doctors* baadhi wanachukua dawa zile na kuwapekea vijana wanatumia kwa ajili ya haya madawa ya kuevya. Mhe. Spika, maeneo hayo yapo na vijana wapo, lakini tunasema kwamba tushirikiane kila Mkoa na Wilaya kuna Kamati ya Ulinzi na Usalama ishirikiane pamoja na Masheha wote pamoja na Tume ya Kudhuibiti Madawa ya Kulevya, naamini kwamba tukishirikiana kwa pamoja

tutaleta mabadiliko na tutahakikisha kwamba madawa haya yanaondoka katika kisiwa hiki chetu cha Zanzibar.

Mhe. Spika, nami niungane na wenzangu walionitangulia niunge mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Ahsante sana nakushukuru sana *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wajumbe nadhani ile faida ya semina ya UWAWAZA inaonekana kwa sababu wachangiaji wetu wa leo wa mwanzo wote ni wanawake na tunaendelea Mhe. Mtumwa Seleiman Makame atachangia sasa hivi, lakini sasa anafuatiwa na Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri ajiandae.

Mhe. Mtumwa Sueliman Makame: Ahsante sana Mhe. Spika kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia hoja hii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kufika hapa leo tukiwa katika hali ya uzima na afya njema, katika Baraza lako hili Mhe. Spika kuweza kuyatetea yale yote ambayo yatatuletea maendeleo katika nchi yetu na pia kuyazungumzia yale yanayotudhalilisha ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, vile vile namshukuru Mhe. Mohammed Said Mohammed na kumpongeza kwa dhati kwa kukaa na kutafakari wakati huu muafaka kuileta hoja hii katika Baraza letu hili tukufu. Kwa kweli suala hili ni tatizo kubwa sana au ni janga kubwa sana katika nchi yetu. Mhe. Spika, vijana wetu wengi wanateseka sana kutumia madawa haya yenye *chemical* ya kuathiri mwili wao. (*Makofi*).

Mhe. Spika, ukitembelea katika maeneo yetu kipindi hiki tulichokuwa nacho saivi tunashindwa hata kuanika nguo uwanjani, kwa sababu ya vijana hawa wengi sana na vijana hawa wakeshatumia madawa haya wanakuwa hawana akili, hususan haya madawa yanayoitwa viroba, sijui kama viroba au mapolo. Mhe. Spika, madawa haya kijana anaweza akaichukua nyumba nzima akaona nyumba ile anaibeba na kumbe haibebi, yeye mwenyewe kishaathirika kwa madaya yale kwa kweli madawa haya yanatuathiri sana katika jamii na katika serikali.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa sababu serikali yetu inawategemea vijana na vijana ndio watendaji wakuu wa nchi yetu wakutuletea maendeleo. Vile vile jamii tunawahitaji vijana kwa sababu mama unapo mlea mtoto unategemea kufika

miaka kumi na tano (15) atakuwa si mtoto, bali atakuwa ni mwenzako. Kwa kweli sisi wanawake ndio tunaoumia sana kwa madawa haya kwa sababu mwanamke akimkuta mtoto wake ameshadhalilika kakaa kitako, basi mtoto yule anasema anasafiri yeye mwenyewe anaona raha, kwani anasafiri kakaa kitako anasizia jicho hata kufumbua hawezi, na denda linamtoka kutokana na kuathirika kwa madawa haya.

Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe alizungumzia kuhusu hizi *Sober house*, kwa kweli majumba haya Mhe. Spika, ni majumba mazuri lakini bado hatujaweza kuyahifadhi madawa haya. Kwa sababu ikiwa mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kushughulikia Viongozi Wakuu tumetembea katika hizi *Sober house* Unguja na Pemba. Mimi niliyekuwa na kichwa kilichokuwa na matatizo siwezi kuingia kwenye nyumba ile, ukifika mlangoni harufu inaanza kutoka pale pale mlangoni ya bangi, ndio unaambiwa nyumba ile imewekwa kuhifadhi vijana ambao waliokuwa wanataka kuacha madawa. Mhe. Spika, kuweka nyumba zile sio *solution* isipokuwa *solution* ya tatizo hili serikali, jamii tushirikiane kuviondoa vijiwe. Mhe. Spika, naiomba serikali pale ambapo sehemu yoyote palipokuwa pana vijiwe basi vijiwe hivi viondoshwe mara moja. *(Makofi).*

Kwa sababu vijiwe hivi ndivyo vinavyoleta suala zito au ushawishi mkubwa wa suala hili la madawa. Kwa hivyo, narejea tena kuiomba serikali tusimamie vya kutosha kuliondoa suala hili, kwani sisi viongozi ndio tutakaokwenda kuulizwa kesho, kwa sababu Mwenyezi Mungu katupa uongozi, na uongozi ni mtihani. Uongozi si chombo cha kusema kwamba unajinata unakwenda na gari kusema mimi nimepata uongozi wa kula starehe. Mhe. Spika, uongozi ni mtihani isipokuwa kubwa tu tumuombe Mwenyezi Mungu atupe subra na atupe maelekezo ya kuwashughulia wananchi wetu waliokuwepo katika maeneo yetu. (*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa kule kwetu Nungwi kuna zile zinazoitwa boda boda. Mheshimiwa hizi boda boda kwa kweli asilimia mia wanaochukuliwa usiku ni watu hao, waliokuwa washaathirika kwa madawa hayo na wanaokwenda kwenye lana nyengine.

Mhe. Spika, naiomba serikali iweke ulinzi wa kutosha katika kuwafuatilia mapikipiki yale, ni mazuri yanawasaidia watu wanaotoka kwenye mahoteli usiku, lakini ni mazuri kuwachangia wale watu wanaofanya lana. Mhe. Spika mimi sina makubwa kwa sababu mada hii ikizungumzwa ya madawa namgeukia Mhe. Zulfa na mimi nataka kulia, nipo kwenye Baraza la Wawakilishi siku moja nikaletewa taarifa kwamba mwanangu kameza vidoge tatizo kakatazwa kuwa asitumie madawa haya. Kwa hivyo, suala hili Mhe.

Spika na mimi nalipinga vya kutosha na pia nawaomba wenzangu tulisimamie suala hili kuwafichua wale wote ambao wanaouza na wanaonunua madawa haya ili wachukuliwe hatua. (*Makofi*)

Mhe. Spika, baada ya maelezo yangu haya mafupi nimesimama mbele yako kwa heshima na taadhima kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kaskazini Unguja kuiunga mkono hoja hii ya Mhe. Mohammed Said Mohammed. Ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mtumwa Suleiman Makame. Sasa namuomba nimwite Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf akifuatiwa na Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri, Naibu Waziri wa Elimu na Mhe. Omar Seif Abeid ajiandae.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: Ahsante sana Mhe. Spika, *Bismillahi Rahmaan Rahim* namshukuru Mwenyezi Mungu sana kutujaalia sote uzima na kufika hapa leo salama.

Mhe. Spika, mimi nimesimama hapa kuchangia hoja ya Mhe. Mjumbe, Mohammed Said Mohamed (Dimwa), Mjumbe makini, jembe aliyefanya utafiti huu ndani ya Unguja, Pemba pamoja na Tanzania Bara na ndipo akaufikisha ndani ya Baraza la Wawakilishi. Nimpongeze sana kwa kazi nzito ya kujitolea iliyokuwa haina malipo na wala haina lolote bali tu katika kusaidia nchi pamoja na serikali kwa ujumla. Nikupongeze sana Mhe. Mohammed Said Mohammed.

Mhe. Spika, jengine vile vile mimi nitaipongeza sana kwanza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na baade nitatolea kwa nini nikasema hivyo kwamba tumepata viongozi wa juu ambao hawana masuala ya kutumia madawa ya kulevya wala hawana *link* yoyote ambayo wanashirikiana na wauza madawa ya kulevya.(*Makofi*).

Tukianza kwa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi hawa ni viongozi mahiri na wako safi na hawana masuala haya ya kutumia madawa haya wala hawana *link* na watu ambao wanauza madawa ya kulevya. Nimesema hivyo kwa sababu kuna baadhi ya nchi duniani kuna Marais, Makamu wa Marais na Mawaziri Wakuu wanashirikiana na waletaji unga na wenyewe wanakula unga. Lakini sisi ndani ya nchi yetu Zanzibar tunatakiwa tushukuru sana kuanza kupata viongozi wa juu hawa nilowataja pamoja na Waziri, Manaibu Waziri na Wawakilishi wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar kwamba hatutumii madawa ya kulevya.

Nina asilimia 95% kwa sababu sitaki kuweka mia ni mtu ambaye Mwenyezi Mungu peke yake ndio ambaye kafikia asilimia mia na zaidi, nina asilimia 95% ambayo haya niliyoyazungumza kwamba masuala ya madawa ya kulevya humu ndani hatutumii, kama tunavuta sigara na pombe ni suala ambalo limeruhusika, lakini tukizungumza masuala ya madawa vya kulevya kwa humu ndani tunashukuru kwamba tuko vizuri. *(Makofi).*

Mhe. Spika, mimi zaidi ningeomba sana kwa hili kuhakishe hili suala ndani ya nchi yetu, Kitengo hiki cha Kuzuia Madawa ya Kulevya na Kudhitbiti Madawa ya Kulevya ndani ya nchi yetu Zanzibar, basi waje waanze kutupima sisi humu ndani Waheshimiwa wachukuwe vipimo vyetu vya mkoja, watupime kuhusu masuala ya madawa ya kulevya. Na nayazungumza haya kwa maana ya kwamba viongozi ndio wanatakiwa waoneshe mfano mwanzo, halafu ndio twende huko chini. Nathibitisha hili hata tukija kupimwa ndani ya ukumbi huu hakuna hata mmoja atakayekakatwa kama mtumiaji wa madawa ya kulevya.

Sasa sijui kama itatokezea labda Mjumbe mmoja au wawili pengine sina uhakika akawa ana-*link* na waletaji unga inawezekana, lakini kwa kuvuta unga, naweza kuthibitisha kwamba asilimia 95% ndani ya ukumbi wetu nina uhakika kwamba hamna anayetumia madawa ya kulevya hayo.

Mhe. Spika, vle vile mimi nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohamed Aboud (Jembe), ambaye pia hana makeke wala tukimwambia kitu hanuni wala hakereki. Katika mmoja ya Mawaziri ambao tunawazungumza, Mawaziri makini ndani ya Baraza hili basi mmoja yeye na wengine itafika siku nitakuja kuwataja humu ambao wana furaha na hata wakiambiwa hawanuni na wale wananuna nitakuja kuwataja vile vile ikifika siku. *(Makofi)*

Mhe. Spika, nitaanza kwenda kwenye masuala ya hoteli. Mhe. Spika, Zanzibar tuna hoteli nyingi sana na hoteli hizi ni hoteli kati ya ambazo zina-*link* sana na masuala ya madawa ya kulevya, hasa hoteli ambazo wana-*deal* nazo Wazungu pamoja na baadhi ya wa-*local* ndani ya Zanzibar wanaokuja na maboti yao yale ma- *yacht* kule kutoka South Afrika na kutoka nchi tofauti na ndani ya mahoteli wanauziana wenyewe Wazungu kwa Wazungu. Na hilo suala ili ikitaka serikali ithibitishe au iweze kukamata vitu hivi, basi ningeomba sana imefanye *link* vizuri na wale wafanyakazi wa ndani ya mahoteli au watendaji kwa kuwapa fedha, au kwa kuzungumza nao kwa njia yoyote wanaoijua wao uzuri ili wawape *information.* Lakini ndani ya nchi hii yetu wanaosababisha madawa ya kulevya sio Wazanzibari peke yao au Watanzania ni pamoja na wageni ambao

si Wazanzibari wala si Watanzania wanashiriki kwenye masuala ya madawa ya kulevya kuleta ndani ya nchi yetu.

Mhe. Spika, vile vile nikienda kuchangia kwenye suala la sheria zetu za Zanzibar kwenye masuala ya madawa ya kulevya, ni sheria nyepesi sana hata kama mtu atafugwa miaka kumi, ishirini. Ni sheria nyepesi sana kwa nchi yetu kama hii ndogo na watu walioathirika tukifanya *population* yetu na *percentage* ya ambao waliothirika ni wingi sana. Mhe. Spika, tukichukulia kwenye masuala ya visiwa dunia nzima, mimi nafikiri Zanzibar inaweza ikatokezea pengine namba mbili (2) katika watumiaji wanaotumia madawa mingi dunia nzima katika suala la kisiwa kama hiki au nchi ndogo kama hii Zanzibar inaweza kuchukua namba mbili au namba tatu watumiaji wingi sana wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, lakini mimi ningependekeza zaidi, sisi tuna marafiki kama nchi China rafiki wetu wa karibu sana, kuna nchi Iran, Singapore, Malaysia, na hata nchi nyengine kama Thailand, hizi nchi zimeweka sheria ni *death penalty* toka *Airport* inakwambia mapema ukikamatwa na unga basi wewe hakikisha kwako wewe ni kifo. Sasa kwa nini sisi Wajumbe isifike hatua tukabadilisha Sheria hii kushirikiana na sisi pamoja na serikali kwenye kukomesha suala hili ili tusiilaumu serikali tu, kwa sababu pia ukiangalia na sheria yenyewe ni nyepesi. Mhe. Spika, tukitaka tuanze kwenye masuala haya basi kwanza tukubaliane sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na serikali kuweka sheria *death penalty* ni kifo mtu atakayekamatwa kuleta madawa ya kulevya, na yule mtu ambaye haleti madawa ya kulevya bali ni mvutaji kakamatwa nimtumiaji basi kesi yake angalau iwe ya miaka fulani ili aashishwe apate kuwa mtu wa kawaida. Kwa sababu wale mimi nitasema tunawaonea, mimi nataka kuwaandama ni waletaji wa madawa ya kulevya na wasambazaji ndani ya nchi hii. (*Makofi*)

Mhe. Spik, wale wapewe *death penalty* na wale watumiaji ambao wameathirika wakamatwe wapewe adhabu fulani lakini waachishwe ili waendelee kuwa binaadamu wa hali ya kawaida ndani ya nchi yetu. Lakini tukenda kwenye suala hilo hilo ningeiomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwenye watendaji hawa ambao aliowateua katika kuthibiti madawa ya kulevya, basi wangeshirikiana na Serikali ya China kwa sababu katika nchi ambayo kuingiza unga tabu basi ni China kwa sababu sheria zake kali, wanawatendaji ambao wamesomea mambo yale, mtu akikuangalia kwa macho tu dakika mbili tu au moja basi kishaku-*suspect* kama unao na inawe kuwa unao kweli kwa kusoma macho au mienendo yako uliyokuwa nayo *psychological education* wanaoitumia wenyewe hao China na nchi nyengine.

Lakini mimi ningeomba sana watendaji hawa aidha wapelekwe nchini China na nchi nyengine ambazo zina udhibiti mzuri wa madawa ya kulevya au Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, iombe watendaji kutoka China waje walete mafunzo huku ndani ya Zanzibar kwa wale ambao wanaoshughulikia masuala ya madawa ya kulevya, ili tuweze kusimamisha haya mambo kwa njia ya kukamata kwa macho tu bila ya *machine* mtu akimsoma mtu anam-*suspect* huyo mtu ana kitu hichi basi aweze kumsoma bila ya *machine*.

Mhe. Spika, lakini kuna jambo jengine ambalo linajitokeza sana, leo unakuta wananchi wanasafiri sana kupitia *Airport* na kupitia bandarini. Lakini serikali hadi hivi leo mashine walizoziweka mle ndani hazikidhi haja katika masuala ya kudhibiti madawa ya kulevya kwani hazina kiwango kizuri, inaweza kukamata kalamu, ikakamata kompyuta, ikakamata peni na mambo madogo madogo na *chemical* fulani, lakini masuala ya madawa ya kulevya na masuala mengine ambayo watu wanatumia *system* kama nchi za nje kukamata mashine zetu ndani ya Zanzibar hazina kiwango hicho.

Mimi ningeiomba sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ili tulikomeshe hili suala basi mashinen tufanye kadri iwezekanavyo hata kama itakatwa bajeti fulani, basi ziletwe mashine ambazo kama wanazotumia nchi za wenzetu za kuweza kudhibiti katika maeneo yote ambayo ya watu muhimu wanaosafiri kuingia na kutoka ndani ya nchi yetu Zanzibar na Pemba. Vile vile ningependekeza masuala ya mbwa wanaonusa madawa ya kulevya wawepo katika masuala ya *Airport*, bandari *24 hours*, isewe tu kuna ndege fulani ndo mbwa anatolewa kwenye ofisi napelekwa *Airport*. Ningeomba sana ndani ya *Airport* kuweka vyumba maalum kuwe na mbwa angalau watatu, wanne *special* wa kunusa mabomu, wakunusa madawa ya kulevya pamoja na vifaa vingi ambavyo havitakiwi ndani ya nchi yetu waweze kuwepo pale *full time*.

Mhe. Spika, kwa sababu ilitokezea taarifa kipindi cha nyuma mbwa *time* za usiku wanakuwa hawapelekwi kwa kunusa madawa ya kulevya na mabomu. Lakini mimi ningeomba ndani ya *Airport* iwepo sehemu ndani ya bandari na sehemu nyengine zote za muhimu waweko wale mbwa *full time*, *machine* ziwepo na wale watendaji niliowazungumza ambao watakuwa na elimu ya kuwakamata watu kwa *psychological* kwa kuwasoma sura yao basi pia wawepo angalau mmoja au wawili kwenye *shift*.

Mhe. Spika, vile vile ukiangalia *Airport* hii hii ambayo tunatumia sisi, leo wananchi wanasafiri sana kwenda kwenye nchi za maajabu, kwa sababu tukitaka tusitake kuna nchi tunazifahamu hizi nchi ni za biashara. Leo mtu anakwenda zake Costa Rica, anakwenda zake Bulgaria, anakwenda zake

Venuzuela anakwenda Mexico na nchi nyengine ambazo zinaongoza kwenye uzalishaji wa madawa ya kulevya, halafu anasafiri kila siku anakwenda nchi hizo hizo na pale *Immigration Officer* hawawezi hata kumuhoji, wewe bwana unasafiri kwenda nchi hizi unakwenda kwa madhumuni gani? Una kipato gani unasafiri sana kama hivi mbona nchi unazokwenda haziingii akilini, kwa sababu hizi nchi Italy, Mexico, Costa Rica, South Africa, Colombia, Afghanistan, Russia, Pakistan ni nchi ambazo zinazalisha unga kwa wingi na ndio zinasafirisha unga kwa matani, Lakini leo pale *Airport* wanapita watu wanasafiri hana hata duka mjini, lakini kwa mwezi anasafiri mara mbili na ukiangalia mihuri yake ni ya nchi kama hizo.

Mhe. Spka, ifike wakati wazuiliwe na wahojiwe hizi nchi unaokwenda kwa biashara gani na ikibidi waoneshe vielelezo, waoneshe basi kwa sababu mtu unapofanya *deal* na nchi zile, kama ushawahi kufanya nao biashara basi risiti zinakuwepo, barua itakuwepo ya kuweza kuthibitisha kwamba wewe unafanya kazi fulani. Lakini leo manchi kama haya watu wanakwenda, wanarudi wanakenda ku-*set* mambo ya mzigo na tuwe makini sana na hata wafanyabiashara wa Zanzibar ambao wanachukua mzigo wao Pakistan, Afghanistan na Brazil tuwe makini, sisemi wanaleta unga tuwe makini sana wanaokwenda nchi hizi kuchukua sijui michele, unga na masuala mengine na kuleta bidhaa zao kwa njia ya makontena au meli nzima. Mhe. Spika, tuwe makini sana hizi nchi ni wataalamu na wamebobea, nikisema hivyo kwamba hawa ndio ma-*supplier* duniani unaweza kuwakuta wana-*supply* 75% ya unga ndani ya dunia. Mhe. Spika, ni watu ambao wamekamika na wenye mtandao mkubwa.

Mhe. Spika, vile vile mimi ningetoa ushauri mengine kwa Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwamba suala hili ni zito, na suala hilo linataka hekma. Suala hili hili ninataka ifike wakati mutayarishe bunda fulani ambayo ya kuwapa watu watakaotoa *information* kama *tip* muwapatie fedha ili *information* zizidi kutoka kwa wale ambao wanaoleta madawa ya kulevya na kuuza ndani ya Zanzibar au kutoa na kuingiza ndani ya Zanzibar. Kuwepo na fedha maalum na mfuko maalum ya kuwa-*tip* watu ambao watatoa *information.* Lakini tukiacha hapo hapo katika hili suala la hawa ambao la watendaji wa Tume wote, ningeomba sana muwatayarishie mazingira mazuri yenye ulinzi, yenye fedha nzuri katika malipo yao pamoja hata maslahi yao mukae nao muangalie, kwa sababu hili suala tunalotaka kulikomesha ni zito na lina njia nyingi. Mhe. Spika, mtu anaweza akaambiwa atapewa bilioni moja atoe *information* na wewe unamlipa laki mbili atachukua bilioni moja kutokana na hali ya maisha ilivyo.

Ningeomba sana hawa watendaji wa Tume hii, tutafika hatua tunaweza kuwasa-*suspect* kwamba labda hawafanyi kazi au hawataki wanashirikiana na watu wa madawa ya kulevya lakini pengine sivyo. Mimi naamini Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewateuwa hawa kwa kuwatambua kwamba wako makini na sio watu ambao wanashirikiana na masuala ya madawa ya kulevya. Masuala ya mshahara na ikibidi hata kama kuna bastola pia wapewe wakae nazo wenyewe mfukoni. Vile vile hata ulinzi wapewe mzuri watu wa kitengo hiki wanaohusiana na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, ningekwenda kwenye suala la kwamba kuna boti hizi za kitalii zinakuja sana sasa hivi Zanzibar wana-*park*, zina-*float* tu pale Nungwi, Kendwa, Forodhani. Nyingi zinatoka South Africa, zinatoka nchi za karibu na nyengine za mbali. Hizi katika watu ambao wanashiriki katika madawa ya kulevya ni moja ya maboti haya kwa sababu hata duniani ukiangalia kuna *yacht* zaidi ya 50 mpaka mia zimekamatwa Uingereza, Australia na nchi nyengine ambao wanasafirisha mwingi sana tani kwa tani ya madawa ya kulevya. Huu utafiti mimi nimeufanya na nchi nyingi ambazo wamekamata basi wamekamata kwa njia ya meli kuliko njia ya ndege.

Mhe. Spika, hili linasababishwa kwamba mtu anakuja na meli yake au anakuja na boti, wale watu wa doria ikiwa Polisi au nani wanatakiwa waende kwenye ile boti kabla mtu hajafika ni mgeni, basi waweze ku-*search* waingie na mbwa wao, waingie na *search warrant* wawaangalie mtu wamemkuta yuko safi basi wamuachie, lakini leo yanakuja maboti yana-*sell* tu katika bahari yetu hatuyaulizi mwanzo wala mwisho.

Mhe. Spika, suala jengine vile vile mimi ningeishauri tena serikali kwa mara ya pili. Nafahamu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iko makini na kama nilivyozungumza kwamba watendaji wako makini hasa viongozi wetu wa juu. Suala hili linataka hekma na tumeshamjua huyu mtu anauza madawa ya kulevya anauza au tumepata *information* kwamba...

Mhe. Spika: Dakika 15 umeshatumia Mheshimiwa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Dakika 15 niendelee?

Mhe. Spika: Nina *stop watch* ndio tatizo.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mimi Mheshimiwa samahani sana niliuliza nikaambiwa leo hakuna dakika, naomba dakika tano. *(Makofi/Kicheko)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa mchango wako mzuri.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Spika, naomba dakika tano mana nilikuwa sipo sijui masuala hayo.

Mhe. Spika: Hapana Mheshimiwa samahani, andika kwa maandishi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Spika, naomba kuunga mkono hoja. Hii ni hoja maalum ya Mhe. Mohammed Said Mohammed nai-*support* sana na naiunga mkono. Pia nategemea kwamba serikali itachukua hatua za hali ya juu ili kukomesha hili suala la kushirikiana kwa pamoja. Ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana. Waheshimiwa Wajumbe mpaka sasa hivi watu ni wengi sana ambao wameomba na sidhani kama watapata wote, kwa sababu tulikusudia kuikamilisha asubuhi ya leo hii hoja.

Moja ni kwamba nitakuhojini kukuombeni kwamba tupunguze huu muda kwa sababu michango mingi inakuwa inajirudia sana, tupunguze muda badala ya dakika 15 twende kwenye dakika 10. Lakini pia kuna tatizo ambalo limejitokeza la msiba wa baba wa mwenzetu ambaye amefariki na atazikwa Alaasiri.

Sasa na hili nalo nadhani tuliangalie, vyenginevyo itabidi sasa hii tuikamilishe sasa hivi ili jioni sasa ile hoja ya pili iweze kuja. Kwa hivyo, kubwa hapa naomba sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atoe hoja ya kupunguza muda ili tuchangie dakika 10 tu ili watu wengi zaidi waweze kupata kuchangia hii hoja muhimu.

KUWEKA KANDO KANUNI YA MUDA WA KUCHANGIA

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kama ulivyotoa maelekezo yako na hasa ukitilia maanani kufiliwa kwa Mjumbe mwenzetu, ndugu yetu Mhe. Abdalla Maulid Diwani, Mwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe kapata faradhi ya kuondokewa na baba yake. Kwanza nichukue fursa hii kumpa pole yeye na familia yake, ndugu, jamaa na marafiki wote.

Mhe. Spika, kutokana na hali hiyo basi tuwaombe Wajumbe wako ili tuweke kando muda wa kuchangia wa dakika 15 na badala yake tuchangie kwa dakika 10, ili tupate fursa zaidi za kuchangia na kama ikiwezekana tukizimaliza hoja zote mbili hivi asubuhi tukapata nafasi ya kushiriki maziko sote kwa pamoja

itakuwa jambo zuri zaidi. Lakini mimi ninachokiomba kuweka kando muda wa dakika 15 ili tuchangie kwa dakika 10 tuweze kumaliza shughuli zilizo mbele yetu.

Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Ahsante, Waheshimiwa Wajumbe hoja iliyopo mbele yetu ni ya kuweka kando Kanuni ya 56(8) ya muda ili tuchangie kwa dakika 10 badala ya dakika 15 ili kuweza kuwapata Waheshimiwa wengi zaidi kuichangia hoja hii. Lakini pia iwe mpaka kwa ile hoja ya pili vile vile itakayokuja nayo yenyewe ichangiwe kwa muda huo huo, isipokuwa tu kwamba baadhi yetu tutakwenda kushiriki maziko, lakini baadhi tutarudi hapa saa kumi na moja. Kwa sababu maziko ni *Faradhi Kifaya*, ni faradhi ya kuwakilishana. Kwa hivyo baadhi tutakwenda kwenye hiyo faradhi lakini baadhi watarudi hapa saa kumi na moja ili kuweza kumalizia na ile hoja ya pili.

Sasa naomba niwahoji wale wote wanaokubaliana na hoja hiyo ya Mhe. Waziri wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kunipa fursa hii. Mimi nitazungumza kwa muda ambao hautozidi dakika mbili wala sio kumi.

Hoja iliyo mbele yetu iko wazi na ukubwa wa tatizo katika jamii yetu unaeleweka kama ni tatizo kubwa la kijamii. Mimi ningependa kuzungumzia upande wa pili labda namna ya kuweza kulishughulikia suala hilo sio kueleza ukubwa au asili ya tatizo lenyewe. Hoja imeweka vizuri kabisa kuhusu suala hili.

Mhe. Spika, ili suala hili tuweze kulifanyia kazi ipasavyo na tuweze kufanikiwa taasisi zifuatazo lazima zifanye kazi yake ipasavyo:-

1. Sisi wanasiasa tufanye kazi yetu ya siasa ya kuwashajihisha na kuhamasisha wananchi wetu kuepukana na matumizi ya madawa ya kulevya.

2. Sisi serikali tufanye kazi yetu ya kiserikali ya kutekeleza sheria kikamilifu zinazohusiana na suala hili la kudhibiti, kuzuia na mambo mengine yote yanayohusiana na hayo.

3. Sisi wanaharakati kupitia jumuiya zetu za serikali tuna wajibu pia wa kufanya kazi zetu za kiuana harakati za kuelimisha jamii kuepukana, kuzuia na athari ya madawa ya kulevya.

4. Sisi wananchi tufanye kazi yetu ya uananchi ya kutii sheria bila shuruti, lakini wakati huo huo kuwa raia wema ambao tutatoa taarifa sahihi na kwa wakati katika taasisi zinazohusika.

Baada ya kusema hayo, ili haya niliyoyasema yaweze kufanikiwa kwa ukamilifu wake ni vizuri na ni vyema kuanzisha mjadala au mdahalo wa kitaifa juu ya suala hili kwa kuanzia katika Shehia, Majimbo, Wilaya na Mikoa. (*Makofi*).

Mhe. Spika, pia tuelewe kwamba jambo hili lina hatua tatu kwa upande wangu mimi. Hatua ya kwanza ni hatua ya kudhibiti, hatua ya pili ni hatua ya marekebisho na hatua ya tatu ni sehemu ya elimu. Mambo haya lazima yende sambamba.

Baada ya kuipitia ripoti hii na hasa katika maazimio nimeona kwamba maazimio yote tisa yameelekezwa kwa serikali. Serikali ifanye hivi, taasisi ya serikali ifanye hivi. Mimi nakubaliana nayo lakini pia kuna sehemu nyegine lazima zihusishwe.

Kwanza wanasiasa kwa maana ya Wabunge, Wawakilishi na Madiwani na wao pia waingizwe katika maazimio kwamba wana kazi fulani ya kufanya katika suala hili, isiwe serikali yake.

Pili, wazazi, walezi, Taasisi za Kidini na taasisi nyengine zote nazo zipewe wajibu katika azimio hili zifanye nini katika suala hili la kuzuia janga hili.

Baada ya kusema hayo nashauri kwamba tuingize azimio hilo kwamba Wabunge, Wawakilishi na Madiwani na wao pia watalazimika kufanya kazi yao ya kuelimisha na kuhamasisha wananchi juu ya suala hili.(*Makofi*).

Jengine niweke sawa zaidi kwamba Wabunge, Wawakilishi na Madiwani watasimamia kuendesha midahalo hii niliyoitaja katika Shehia, Wadi,

Majimbo, Wilaya na Mikoa suala hili, na tukifanya hivyo nadhani tutashinda, *yes* tutashinda.

Naunga mkono hoja. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri. Sasa naomba nimwite Mhe. Omar Seif Abeid atafuatiwa na Mhe. Viwe Khamis Abdalla na Mhe. Bihindi Hamad Khamis ajiandae.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii na namshukuru saa mleta hoja Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kwa kuiwasilisha hoja hii.

Lakini mimi kabla ya yote natanguliza shukurani zangu kwa Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha tukakutana hapa asubuhi hii tukamaliza shughuli zetu za maswali na majibu tukaingia katika hoja hii, tunakuomba Mwenyezi Mungu utuongoze. Kwa sababu jambo tunalolizungumza ni jambo kubwa jambo ambalo linaigusa jamii yetu sote na ni imani yangu kwamba tutakaposhirikiana kama alivyotangulia nimemsikia kidogo Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali yanawezekana hakuna lisilowezekana. Kwa sababu kuna aya moja katika Biblia inasema: "Kama ilivyokuwa mwili pasipo roho umekufa na imani pia bila ya matendo nayo imekufa". Kwa hivyo, ili tufungue imani yetu itekelezeke ni lazima mashirikiano ya pamoja yanahitajika.

Mimi kwa upande wangu nachukua fursa hii kwanza kuipongeza serikali kwa juhudi zake kubwa inazozichukua juu ya mapambano haya ya vita dhidi ya madawa ya kulevya. Lakini napenda tukumbuke kwamba kadhia hii inayotukabili tunayoizungumza leo ni kadhia ambayo ipo ulimwengu mzima na wenye kuendesha biashara hii ni watu wenye uwezo wa hali ya juu. Hapa kwetu sisi tumshukuru Mwenyezi Mungu kwamba haijafikia hali kama waliyonayo wenzetu huko Colombia na nchi nyengine, tunakuomba Mwenyezi Mungu hali kama hiyo isitufikie sisi na ni imani yangu kwamba kutokana na uwezo na ari na imani aliyonayo Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein juu ya wananchi wake hili linawezekana tutakapotoa mashirikiano ya dhati sote kwa pamoja.(*Makofi*).

Mhe. Spika, suala la madawa ya kulevya wenzangu wamelizungumza kwa kina, wamelizungumza sana, limezungumzwa na wengi, limeanza Tanzania Bara hivi karibuni tumekuta jinsi ya mwelekeo wake lilivyopokelewa na pia nampongeza sana Rais wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Makamu wa Rais nimemsikiliza, akisema vita hivi si moto wa ndifu ni vita

endelevu. Ni kwamba mashirikiano yanahitajika kwa rika zote, sekta zote kwa nyanja zote kwa sababu waathirika ni sisi sote. Kwa hivyo, mashirikiano yanahitajika kwa taasisi pia za serikali, taasisi za serikali zenye majukumu haya zinapaswa kuonesha uaminifu wao wa hali ya juu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nasema hivi nikinukuu maneno ya Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma kwa sababu mimi takwimu sina, kwamba kuna kesi za kuanzia mwaka 2000 zilizotangulia na zikafikia kesi 70, lakini zilizopatikana majibu yake au hukumu ni kesi tano. Hivi kweli tujiulize ndio uhalisia ulivyo? Hivi haya yote yaliyokamatwa hayakuwa kweli madawa ya kulevya, yalikuwa ni majani makavu pengine au unga wa ngano, au sembe. Hii inaonesha kwamba bado miongoni mwetu hatujakubaliana na ile dhana ya Rais wetu au viongozi wetu wakuu kwa kupambana na janga hili la madawa ya kulevya. Nitoe wito kwa taasisi zetu ziwe na uaminifu wa hali ya juu na pia suala hili lilihitaji mashirikiano ya dhati.

Tume ya Madawa ya Kulevya ni taasisi iliyoanzishwa kwa mujibu wa sheria, wenzetu hawa wanafanya kazi ambayo inapaswa kuungwa mkono na sisi viongozi kuanzia ngazi ya Shehia, Wadi, Jimbo, Wilaya mpaka Taifa, ili kuonesha kwamba sisi sote ni waathirika na juhudi za pamoja zinahitajika.(*Makofi*).

Mhe. Spika, hakuna wizara ambayo haiguswi, ukienda Wizara ya Afya inaguswa, ukienda Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali inaguswa, ukienda Polisi wanaguswa, ukienda Mahakama wanaguswa, kila taasisi na wizara za serikali zinaguswa juu ya janga hili. Naendelea tena kutoa wito uaminifu unahitajika ili kupambana na tatizo hili. Mhe. Spika, wale wenzetu wachache ambao tamaa zimewashika au zimewatawala ni wajibu wakaona kwamba kuna baadhi ya maeneo hayahitajiki kuwa na tamaa kwa sababu tamaa yao ndogo inaweza ikaliponza taifa zima.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa nina ombi na naiomba sana serikali kwamba kuiongezea nguvu Tume hii ya Kupambana na Madawa ya Kulevya. Mhe. Spika, wapewe nyezo, wapewe vitendea kazi vya kutosha, wawezeshwe kwa kila hali ili waweze kufanya utaratibu wa kukamilisha kazi yao, kwa sababu bila ya hivyo itakuwa tutakuja kulaumu kwamba hii Tume haifanyi kazi, haifanyi hivi, lakini uwezo wa kisheria ni moja kati ya nyezo wanazotakiwa wawezeshwe. Nilisema mara ya kwanza kwamba iko haja ya kuiangalia Sheria ya Madawa ya Kulevya ikiwezekana ikapangiwa Mahakimu maalum kwa ajili ya kazi hii ya kusikiliza kesi za madawa ya kulevya, ili ziweze kwenda kwa haraka na iwekewe muda maalum. Pale inapotokea kwamba watuhumiwa wa

madawa ya kulevya au watu wanaojishughulisha na biashara za madawa ya kulevya wamekamatwa iwepo na sheria ya kuwazuia kutokuwapa dhamana, iingizwe hasa katika moja ya makosa ya kuwanyima dhamana katika orodha nalo liingizwe, kwa sababu hili ni tatizo kubwa, sugu, linalohitaji maamuzi mazito.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa sababu mfanyabiashara wa madawa ya kulevya unapomkamata ukampa dhamana ni wazi kwamba unamtengenezea njia ya kushinda katika kesi inayomkabili, lakini atakapokuweko ndani na kesi inaendelea, ni dhahiri kwamba uwezo wa kuharibu mwenendo mzima wa kesi unakuwa ni mdogo kwake ukilinganisha na kwamba mtu huyo yupo nje. Kwa hivyo, naomba sana serikali iliangalie hili kwenye utaratibu wa kisheria ya madawa ya kulevya, kwani kama nilivyotangulia kusema Mhe. Spika, watu wanaofanya biashara hii wengi ni watu wenye nguvu zao, wenye uwezo mkubwa wa kifedha. Sasa kupambana na mtu mwenye fedha kunahitaji mikakati mikubwa sana na madhubuti, vyenginevyo tutakuja kulaumiana tutasema hawa hawafanyi hivi, hawa hivi lakini naomba sana tumeanzisha Tume ya Madawa ya Kulevya...

Mhe. Spika: Una dakika moja Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Shukurani, tumeanzisha Tume ya Madawa ya Kulevya wanaendelea kufanya majukumu yao na zile *sober house* ikiwa kweli wako watu wanaendela basi hii Tume ya Kudhibiti wa Madawa ya Kulevya ichukulie suala hili kwa uangalifu wa hali ya juu na iwapo itabainika kwamba miongoni mwao wapo wanaofanya hivyo wakatamwe nao washitakiwe na waonekane kama wao ni wahalifu wakubwa na ni chanzo cha matatizo haya.

Mhe. Spika, kwa sababu serikali imefanya jambo hili kwa lengo zuri, inagharamia inatoa pesa kwa ajili ya kueleta mabadiliko, lakini wao wanarudi kufanya ubadhirifu. Kwa hivyo, naomba sheria kali zichukuliwe kwa wale wamiliki wa *sober* ambao watagundulika kwamba katika *sober* zao zinaendesha biashara hizi kinyume na utaratibu ambao Serikali na maelekezo ya serikali, hawa wawe na adhabu ....

Mhe. Spika: Naomba umalizie Mheshimiwa.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante Mhe. Spika, na mimi naunga mkono hoja hii. Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Omar Seif Abeid. Sasa naomba nimwite Mhe. Viwe Khamis Abdalla akifuatiwa na Mhe. Bihindi Hamad Khamis na Mhe. Hassan Khamis Hafidh ajiandae.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii nikaweza kuchangia hoja ya Mhe. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Mwakilishi wangu wa Jimbo la Mpendae Mhe. Mohamed Said Mohamed.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa utafiti wake ambao kuwa aliufanya na akaweza kutuletea hoja binafsi katika Baraza hili la Wawakilishi kuhusu Madawa ya Kulevya. Mhe. Spika, ni kweli tatizo la Madawa ya Kulevya hapa Zanzibar limeshamiri siku hadi siku. Mhe. Spika, janga hili la madawa ya kulevya linatupotezea vijana wetu wengi.

Mhe. Spika, itakuwa mpungufu wa fadhila kama nitakuwa sijaichangia hoja hii ya Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa sababu walionileta humu ndani ya Baraza la Wawakilishi ni vijana na vijana wengi ndio wanaoathirika na janga hili la Madawa ya Kulevya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, muda umefika sasa Zanzibar, serikli wakaweza kulishughulikia janga hili la madawa ya kulevya. Nimpongeze Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuhakikisha katika Mkoa wa Dar es Salaam janga hili la madawa ya kulevya limepotea kabisa. Kijana yule ni shupavu, kijana yule haogopi wakati wowote yuko tayari kuitumikia serikali yake.

Mhe. Spika, na sisi Wazanzibari ni lazima tuhakikishe janga hili la madawa ya kulevya limepotea. Mhe. Spika, mtumiaji wa madawa ya kulevya wakati wowote yuko tayari kuuwa, ikifika muda wake anatamani kupata ule unga au kidonge basi kama hajakipata anaweza akamuuwa mtu kwa shilingi elfu tano au anaweza akamchoma mtu kisu kwa simu ya shilingi elfu thalathini, mambo haya yanatokea katika mitaa yetu, kama ya Jangombe, Kwaalinato, Kwahani, Mboriborini yote yapo.(Makofi).

Mhe. Spika, niende kwenye hizi *sober house*. Mimi kwa upande wangu naona hizi *sober house* hazitusaidii katika nchi yetu, kwa sababu mwaka 2011 nilikuwa Mjumbe katika Kamati ya Habari na Uwezeshaji, Wananchi Kiuchumi. Kamati yetu ilibahatika kutembelea katika hizi *sober house* walitupa malalamiko makubwa, walitwambia sisi tuko hapa na baada ya kuondoka hapa tunarudi mitaani tunakuwa hatuna kazi za kuzifanya. Kwa hivyo baadae

hatuchukuwi muda tunarejea kule kule kwenye janga hili la madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, niiombe serikali kama wanataka kuziweka hizi *sober house* kwa kuwaelimisha vijana wetu ili waache janga hili la madawa ya kulevya, basi ziwepo *sober house* mbili tu za serikali kwa Unguja moja na Pemba moja, tutakapo ziendeleza *sober house* basi uingizwaji wa madawa ya kulevya yatazidi kuendelea Zanzibar na hawa waingizaji wa madawa ya kulevya Zanzibar wapo na ndio matajiri wakubwa hapa nchini.

Serikali kwa makusudi waache wote waliokuwa nayo suala la madawa ya kulevya walishughulikie itafika, muda Zanzibar itakuwa hatuna vijana wanaume wala wanawake. Sasa hivi akikupita kijana mdogo tu ana miaka kumi au kumi tano akianza kutumia haya madawa ya kulevya basi hata sura inabadilika. Vijana hawa wanaotumia madawa ya kulevya wameshawatia wazee wao ufukura, wanaanza kuiba kama mama yake ana dhahabu anauza dhahabu anakuja vyombo anamaliza nguo anamaliza na *TV* na deki yake.

Mhe. Spika, mimi kama Mwakilishi wa Vijana sina pingamizi na hoja hii aliyoileta Mhe. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa sababu muda wake umefika na wakati wake umefika wa kushughulikiwa janga hili la madawa ya kulevya.

Kwa hayo, machache naunga mkono hoja hii ya Mhe. Mohamed Said Mohamed asilimai mia moja.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsane sana Mhe. Viwe Khamis Abdalla, ahsante kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Bihindi Hamad Khamis atafuatiwa na Mhe. Hassan Khamis Hafidh na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu ajiandae.

Mhe. Bihindi Hamad Khamis: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ambayo ameifikisha hapa Mhe. Mohamed Said Mohamed kwa ufanisi zaidi pamoja na kufanya utafiti wake wa kina ili kujua kama janga hili linatuathiri wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, kwa sababu hoja hii imeletwa hapa tuweze kuichangia kwa ajili ya wananchi wetu ambao vijana wetu ni waathirika ni wakubwa wa madawa ya kulevya. Mhe. Spika, mimi niipongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuweza kuweka *sober house* kwenye Mikoa yetu ya Unguja na Pemba.

Mhe. Spika, kwa kusema hayo kwa sababu Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna Wilaya mbili; Wilaya ya Wete na Wilaya ya Micheweni. Tunamshukuru Mwenyezi Mungu Wilaya ya Micheweni hakuna *sober house* hata moja iliwekwa. Mhe. Spika, kwa sababu ya kusema hivyo, sasa hivi Mkoa wa Kaskazini Pemba Wilaya ya Micheweni vijana wengi sasa hivi wanatumia madawa ya kulevya. Mhe. Spika, naiomba serikali kwa kushirikina na Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Wilaya zake zote mbili ili kutoa elimu ya kutosha ili vijana wetu hawa wasiweze kuathirika na madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kama tunavyojua sasa hivi madawa ya kulevya yameingia kwenye nchi yetu kwenye sehemu mbali mbali hususan kwenye vijiji vyetu na maeneo ya bandari bubu. Bandari bubu hizi ndizo zinazoleta madawa siku hadi siku. Naiomba serikali kwa kushirikiana na viongozi ambao wanatoka kwenye Mikoa ili kuweza kutoa taalamu zaidi kuwaelekeza vijana wetu ili waondokane na kutumia madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kwa kuendelea mbele nije kwa mtoa hoja ameeleza hoja zake nyingi ambazo zina msingi, tunatakiwa tuweze kumuunga mkono ili serikali ishirikiane na viongozi ambao wamo kwenye maadili na wamo kwenye kuendeleza kuepuka na kuweza kutumia na kuweza kuuza na kuweza kununua ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mhe. Spika, kwa sababu hoja hii imeshachangiwa na Wajumbe wengi na mimi nisingemtendea haki mtoa hoja hii kama sikusimama hapa na nikaweza kuinga mkono hoja hii. Kwa sababu hoja hii imetugusa kwa sababu ni wazazi na tunaweza kukaa na vijana wetu ili kuweza kuwaelimisha zaidi ili wasitumie madawa haya. Naiomba serikali ishirikiane pamoja na mtoa hoja hii na sisi Wawakilishi tushirikiane na mtoa hoja ili kuweza kuendeleza na kutoa taaluma kwa vijana wetu ili wasiweze kutumia madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, naiunga mkono hoja hii mia kwa mia ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Bihindi Hamad Khamis kwa mchango wako. Sasa naomba nimwite Mhe. Hassan Khamis Hafidh atafuatiwa na Mhe. Hussein Ibrahim Makungu na Mhe. Salma Mussa Bilal ajiandae.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Spika, asubuhi hii na mimi Hassan *DIASPORA* wa Welezo kunipa nafasi ya kuchangia dhidi ya janga hili la taifa ya wanaoleta unga kutuumiza ndugu zetu na watoto wetu.

Mhe. Spika, kwa kweli leo nina orodha ya wale wanaoleta na wanauza nitawataja baadae ninayo hapa kwenye bahasha.(Makofi).

Mhe. Spika, kwanza naomba kwa fursa hii kumpongeza Mhe. Mohamed Said Mohamed kamanda kwa kuleta hoja hii kwa kuona jinsi gani vijana wetu wanaathirika na tunakosa nguvu kazi ya taifa. Lakini pili, nichukue fursa hii kumpongeza *RPC* Mkoa wa Mjini/Magharibi baada ya kuamka ameanza kufanya kazi ipasavyo kuwatafuta na kuwakamata waleta unga.(*Makofi*).

Lakini tatu leo nimefurahi sana Mhe. Spika, mwenyewe hayupo Mhe. Waziri wa Afya lakini nimeona jenereta kubwa imeletwa jana saa kumi na kumi na moja na dakika kumi katika Hospitali yetu ya Taifa ya Mnazi Mmoja. Kwa hivyo, nampongeza sana.

Mhe. Spika, sasa naanza kuchangia, Mhe. Spika, unga madawa ya kulevya ni kitu ambacho dunia nzima ikiwemo Zanzibar kinaathiri nguvu kazi za taifa vijana na si siri miongoni mwa athari za unga ni vifo. Mhe. Spika, tumeshuhudia sote jinsi gani vijana wanakufa na jinsi gani vijana wanauwa kutumia mapanga na mambo mengine wanapouvuta unga wao kwa kutaka kumnyanganya mtu simu au chochote kile wanampiga panga ili wapate pesa wakavutie unga.

Mhe. Spika, maradhi mbali mbali kama Ukimwi na mambo mengine yanasababishwa na mambo ya unga, uhalifu Zanzibar na dunia nzima umeongezeka kwa sababu ya unga. Mhe. Spika, wizi uliokithiri umeongezeka kwa sababu ya unga. Mhe. Spika, dunia nzima ikiwemo Zanzibar tunakosa nguvu kazi za vijana kwa sababu ya unga. Mhe. Spika, si siri dada angu Mhe. Zulfa Mmaka Omar alilia kwamba hili ni janga la taifa, umefika wakati Wazungu wanasema, '*realization as a human pontetial'*, muda na wakati umefika sasa wa kutokumsitiri mtu na kutokumuenea mtu haya kwa kutokumficha mtu, tuwatoe na tuwafichue wauza unga wanaoleta unga wote ili kupambana na janga hili la taifa.

Mhe. Spika, mimi nitazungumzia nani wanaoleta unga Zanzibar. Mhe. Spika, si siri Wazanzibari tuko milioni moja na laki tatu na kuna mzee wangu mmoja anasema Zanzibar ni kisiwa cha habari, wauza humu ndani tunawajua, tunajuana wanaozua unga lakini tuna tabia ya kufichana. Mhe. Spika, wauza unga ni matajiri. Sasa Polisi, Mkuu wa Madawa ya Kulevya, Kiongozi wote hawawezi kuwataja waleta unga kwa sababu ya utajiri wao. Mhe. Spika, kama tunavyojua tajiri ni mtu anaogopewa kwa sababu anatumia nguvu ya pesa. Mhe. Spika, kama ninavyosema lazima tuache muhali.

Juzi wakati tuko hapo nje Mhe. Spika, miongoni mwa mtu kubwa tu basi alisema kwani nani asiyemjua fulani na fulani na fulani kama ni muuza unga nchi hii, unashangaa huyo mtu anayesema maneno hayo na cheo alichanacho, unashangaa hivyo muuza unga kumbe mpaka watu wakubwa wanawajua lakini bado hatujawachukulia hatua, kwa sababu ya pesa zao, kwa sababu ya muhali wao. Mhe. Spika, hili ni tatizo tena ni tatizo kubwa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, jambo jengine kinachosababisha unga uwepo ni muhali, rushwa na kujuana kuoneana haya na kufanya mambo mengine. Mhe. Spika, la kusikitisha zaidi ukienda kule jela unawakuta watuaji unga wako wanne kama sikosei lakini hakuna mleta unga jela wala hakuna muuza unga jela. Mhe. Spika, hii inasikitisha ikiwa mwizi wa kuku naye mwizi nae lakini yuko jela, mwizi wa ndizi nae mwizi lakini yuko jela. Mleta unga anaoathiri na kuuwa watu chungu nzima katika tiafa hili, jela hayupo. Mhe. Spika, hii inasikitisha. (Makofi).

Mhe. Spika, juzi nilipokuwa nazungumzia mzee wangu mmoja alisema, hivyo nyinyi Baraza mnafanya nini, hao Majaji, bora Hayati Haji wa Haji, Mheshimiwa Jaji aliyekuwa anawaambia watu chungulia chini alikuwa anawafunga watu, hivyo Majaji waliosoma Mhe. Spika, hakuna anayefungwa.

Mhe. Spika, si siri sababu kubwa inayofanya bado unga Zanzibar unakuja ni matatu makuu. Kwanza muhali, la pili rushwa na tatu kutokufanya kazi kwa kutokushirikiana kwa taasisi tatu kuu, Polisi, *DPP* na Mahakama. Mhe. Spika, taasisi hizi kuu hazifanyi kazi kwa kushirikiana, kila taasisi katika hizi inamlaumu mwenziwe Mhe. Spika, *instead* ya kufanya kazi kwa kushirikiana ili kukomesha janga hili. Mhe. Spika, si siri kama tutaendelea na hali hii *DPP* hafahamiani na Polisi, Polisi hafahamiani na Mahakama, Mahakama hafahamiani na *DPP* hakuna hukumu itakayotolewa.

Mhe. Spika, sababu moja nyengine inayofanya unga uzidi kuletwa hakuna hukumu inayotolewa kwa mleta unga wakati waleta unga wamejaa nchini hii. Mhe. Spika, Zanzibar ni nchi ndogo tumejaaliwa nchi ya kisiwa. Milango ya kuleta vitu hivi ni vingi, ulimwengu umeendelea wanatumia *digital equipment*, wanatumia vifaa vya kileo katika kuleta unga. Ni kweli nakubali kwamba hata serikali baadhi ya vitu haina ya kutafuta lakini Mhe. Spika, kama tutakuwa tupo makini na kama tutakuwa tupo kwelini kama tukimkamata mmoja tu mleta unga, tukafanya mfano kama China ukiupeleka unga hukumu yake kifo Mhe. Spika, unga utapungua.(*Makofi*).

Mhe. Spika, hakuna asiyemjua mleta unga lakini bado tunafichiana mabaya. Mhe. Spika, wakati umefika tangu Tume hii ianzishwe sifikirii kama kuna mtu amemkata, na la kushangaza na la kusikitisha anayeongoza Tume hii ni dada yangu, askari mzoefu mzuri lakini hakuna mtu kakamatwa *serious.* Nawajua watu Mhe. Spika, wanaoleta unga wamekamatwa lakini baada ya miezi sita wako nje na siku hiyo bila ya kujua kama anazungumza na Mwakilishi namuuliza umefanya nini, anasema aah! eeh! bwana muuza unga anakamatwa, si nina pesa, nilipomaliza milioni ishirini nimetolewa. Mhe. Spika, kama nilivyosema unga hauwezi kwisha kwa sababu ya rushwa, waleta unga ni matajiri, waleta unga wana pesa na watu hapa roho zao hawajasema nazo. Mhe. Spika, janga hili litaendelea milele daima.

Mhe. Spika, ninaiomba sana serikali ilione hili tusifichiane, ninayo *list* mimi hapa ya waleta unga kwenye nchi hii. Kama utaniruhusi niitaje basi niko tayari kuitaja potelea mbali *list* ipo. Sisi Wawakilishi tumekaa tumefanya *research* tukasema bwana eeh!liwalo na liwe tumewa- *out line*, wacha tukawataje sasa ili tuone kitakuwa nini hii nchi ya Kimapinduzi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kwa heshima kubwa nitaomba nikukabidhi baadae *list* ya waleta unga kila jimbo wapo Mwera wapo, Welezo wapo, Kwahani wapo kila jimbo wapo. Lakini bado tunafichiana kama hatujapitisha maamuzi kama waliopitisha wazee wetu wakatufanyia Mapinduzi na sisi leo tunaishi salama Mhe. Spika, Zanzibar haitaishi salama kwa masuala ya unga na masuala ya udhalilishaji, kama bado tutaoneana muhali, kama bado tutaoneana haya, kama bado tutataka kula rushwa kwa mambo yanayouwa watu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa muda umefika tuamue kimapinduzi kuukomesha unga lazima tuondoshe muhali. Mhe. Spika, hii ni nchi ya kimapinduzi, hii ni nchi ya wakwezi na wakulima, leo watoto wote mitaani hakupitiki kwa wala unga, unaogopa hata kupita kwa sababu unaogopa kupigwa panga sababu ni unga. Vifo visio mpango kila jambo lisilo mpango linasababishwa na unga na cha kusikitisha Mhe. Spika, wauza unga tunawajua, waleta unga tunawajua sote tunawajua Mhe. Spika, lakini bado tunawaficha kwa sababu wana pesa, bado tunawakumbatia kwa sababu wana pesa.

Mhe. Spika, leo sitaki kusema mengi lakini kama tuko tayari kuwataja kwa sababu tumefanya *research* ya kutosha dhidi ya wauza unga wote wa Zanzibar, sio wote lakini tumefanya *research* ya kutosha na tunao kunako vitabu hivi hapa, huyu muunza unga, huyu nani, huyu mleta unga tunao Mhe. Spika, tuko tayari kwa sababu tumekubali Waheshimiwa wa Baraza la Tisa Wawakilishi ndio Baraza litakalokuja kumkomboa Mzanzibari na sote tunajua Baraza hili

hamna humu wote ni wana Mapinduzi, jukumu letu ni lile lile kuwaokoa wakwezi na wakulima wa nchi hii, wana Mapinduzi wote ni kazi tuliyopewa na wazee wetu.(*Makofi*).

Baada ya hayo machache Mhe. Spika, kwa heshima kubwa na taadhima kubwa naomba kuunga mkono hoja hii iliyoletwa na kamanda Dimwa, na baadae tutakukabidhi majina hayo Mhe. Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe kwa mchango wako. Meza ilikuwa inaomba hiyo *list* iletwe hapa kwa Spika, hiyo orodha uliyonayo Mhe. Mjumbe iwasilishe kwa Spika. Naomba sasa nimwite Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa) atafuatiwa na Mhe. Salma Mussa Bilal na Mnadhim Mhe. Ali Salum Haji ajiandae.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa): Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa mchana huu na kuijadili hoja hii muhimu sana. Lakini pia nikushukuru na wewe Mhe. Spika, kwa kunipa nafasi ya kuichangia hoja hii ya Mhe. Mohammed Said Mohammed Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae wa kudumu, kwa hoja yake nzuri kuhusu ongezeko la uingizaji wa utumiaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, hii hoja ni nzuri sana na mimi nampongeza Mhe. Dimwa kwa kuliona hili, na hii ni vita vya taifa lakini sio vya taifa tu ni vita vya dunia, nimpongeze sana mleta hoja kwa kuliona hili.

Mhe. Spika, mimi niseme tu kwamba kwanza tumechelewa kwa sababu ya janga hili la madawa ya kulevya. Lakimi mimi naomba sana tuwe *serious* kwa jambo hili na bila ya kuwa *serious* basi hatuwezi kufanikiwa kwenye vita hivi. Kwanza niombe sana Mhe. Spika, kwa nia njema Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, hebu na huku itusaidie kwa hali na mali kwa kupitia Usalama wa Taifa wa kule Dar es Salaam. Kwa sababu ukitizama kunatakiwa nguvu kazi, sio kutumia askari, kutumia Usalama wa Taifa kuchunguza haya madawa, hawa waingizaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, mimi niseme kwenye ripoti ya Kamati yetu iliyokuja Baraza la Wawakilishi ya Utawala Idara Maalum ya Sheria ilitoa changamoto nyingi, na ukitizama moja tunahusika wenyewe, Mkemia Mkuu ana malalamiko makubwa kwenye masuala haya. Ukitizama kesi nyingi karibu 15,815 ziliripotiwa lakini Polisi wenyewe wanachangia kuharibu kesi hizi. Ripoti hii ipo ya Kamati ya Baraza la Wawakilishi sio kama maneno yangu. Kwa hivyo, sisi wenyewe hatujawa *serious* kwa suala hili, hatuwezi kulimaliza kama

hatujawa *serious*. Mimi nilisema juzi hapa Mhe. Spika, kwamba hizi *sober house* hazina maana, kwa sababu tunakuta tunawazalisha wenyewe watumiaji wa unga, wanatumia tunawapeleka *sober house*, wakishakutumia wakirudi mitaani Mhe. Spika, imesemwa hapa kisha wanakuja kurudia tena madawa yale.

Mhe. Spika, mimi ninaye mwananchi wangu mmoja wa familia moja, baba mtu anavuta unga tu, ana watoto wanne, amini Mwenyezi Mungu hakuna kinachofanyika kule, mambo yote napigiwa mimi simu kuanzia skuli, matatizo, maisha, kwa kweli hatari kubwa na huwezi kuwa usisaidie familia kama ile, baba mtu hana nyuma wala hana mbele, yeye anashughulikia madawa. Kwa hivyo, janga hili ni kubwa sana Mhe. Spika, na hatari hata Mwenyezi Mungu atusaidie sana kutuokoa au vijana wengi wataharibika baada ya muda sio mkubwa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, pale Forodhani ukienda utawakuta wale watumiaji wa madawa hawana pesa, wanakuja pale wanawakamata wageni na mpaka sisi tukienda pale wanaomba pesa ili wapate kwenda kuvuta madawa, na unamuonea huruma, anakuambia naumwa mguu unaniuma mkono, ili umpe pesa akavute. Ukimwambia wewe unavuta madawa ya kulevya, anakuambia aah! mimi sivuti mimi naumwa, unampa shilingi 1,000/- au 2,000/- lakini matokeo yake anapeleka kwa nani, kwa muuzaji. Mimi nasikitika sana kwa hawa watu ambao wanaleta madawa.

Mhe. Spika, mimi kwanza nimpongeze sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. John Pombe Magufuli kwa juhudi zake, na pia Mhe. Mkuu wa Mkoa, kajitolea kufa na kupona kwa kufanya vita hivi. Mimi niseme kwa nini nampongeza Mhe. Rais. Nampongeza kwa sababu vita hivi sio vidogo, na mimi nampongeza kwa kuwatangaza wale wauzaji wa unga. Kwanza kafanya juhudi kubwa na nzuri na sisi tuige mfano ule ule, mfano mzuri unaigwa, kwa nini sisi hatuigi Mhe. Spika, tatizo liko wapi. Vita hivi ni vikubwa, hata mtu akitangazwa akiwe siye atajieleza atatoa ushahidi basi tutajua. Kama anashutumiwa basi atangazwe na aitwe, kwa sababu vita vile anavyofanya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, sasa hivi imekuwa unga Dar es Salaam haupatikani, hata wale waingizaji wameogopa.

Mhe. Spika, mimi nitoe mfano mmoja, kwa sababu kazi aliyoifanya Mkuu wa Mkoa wa pale Dar es Salaam kuwakamata kwanza watumiaji, watumiaji wale kuwakamata na kuwaleta kituoni wataeleza wanaupata wapi, walisaidia Jeshi la Polisi. Lakini hapa naona mpaka leo naona kimpya halijafanyika suala hili, wakamatwe wale waelezwe wanaupata wapi. Kuna wasambazaji watatu, kuna

mtumiaji ambaye ni mdogo, huyu mimi wala simtii kwenye shutma sana, kwa sababu yeye anaingizwa kwenye majangwa haya kwa kushawishiwa tu. Kuna wanawake wanaingizwa, kuna marafiki wanaingizwa, wanatoka watu Arabuni wana pesa zao, wanakuja hapa wanawachukua vijana wetu, ili wapate kampani tu ya kuvuta unga nao na kupiga *story*, anamwambia vuta kidogo, akiondoka yule mgeni yule anapata kutumia yale madawa.

Kwa hivyo, mimi naomba sana hawa watumiaji wakamatwe lakini kwa nia njema, watoe *information* wapi unga wananunua, hawa watatusaidia sana na wakitoa maelezo yao basi watafuatiliwa. Mhe. Spika, haya makundi yako matatu. Lakini kundi la kwanza watumiaji, wa pili ni wasambazaji hawa wa ndani ya mji wetu ambapo kwenye majimbo yetu pia wapo wanasambaza unga huu wanauza kama maduka yao yapo. Kundi la tatu, ni hawa wafanyabiashara wakubwa wanaoleta, ambao hawa hawaukamati hata unga wenyewe, hawa wanauleta halafu wanawapa hawa wasambazaji.

Mhe. Spika, mimi nitoe mfano mmoja mzuri. Pale bandarini kwetu hapa Zanzibar. Mfano mfanyabiashara analeta, simtaji nani ni mfanyabiashara X, sisemi nani lakini nasema ule unga au mchele au sukari umetoka nje kama Pakistani, India au kwengineko, kule inapopakiwa ile bidhaa basi hakuna *checking* yoyote ya ule mzigo. Kama kutatiwa vipolo kumi vya *cocaine* mfano ndani, ukija hapa nani atajua kama kuna *cocaine* mule ndani. Pale bandarini una uwezo kontena lako kulichukua kwenda kuikata nyumbani kwako, ukalipia ukaambiwa chukua kakatie nyumbani kwako, haya mambo yanafanyika pale. Kama kontena ina vipolo kumi vya unga itakuwaje, unga mwingi unaingizwa pale kwa wafanyabiashara, ikiwezekana yale makontena yaangaliwe kwanza na kuwe na mbwa ambao wanaweza kujua kuna nini ndani, bila hivyo unga mwingi unaingizwa pale. Kuna wafanyabiashara wanaingiza mchele, unga na sukari, sio kama nia yao kuuza sukari na unga, nia yao mle ndani kuna *cocaine* na ndio maana faida yote inapatikana, anaweza mtu akauza hasara kwa hasara lakini ile faida yake imo mule ndani na usambazaji mwingi unakuwa wakileta wale ndio wanasambaza huku sehemu nyengine kuwapa watu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mimi nitowe mfano, nimeshabahatika kwenda USA Marekani Manhatan nimeshakwenda kwenye mwaka 1993, nilikwenda kwa biashara zangu. Lakini nilipofika Manhatan siku ya kwanza New York, nimekwenda pale nikakamatwa nikaambiwa bwana njoo hapa na nikapigwa *X-Ray*. Kwa sababu kuona *style* yangu niliyokwenda nayo pale nimekwenda kwa madhumuni gani, na nikahojiwa karibu masaa mawili. Nikapigwa *X-Ray* nikaangaliwa, mimi nikawa ninacheka, nipigeni *X-Ray* mpaka mumalize, wakanipiga *X-Ray* kabisa, wakaniangalia. Lakini mwisho wa siku wakaniambia

kweli wewe huna tatizo nenda. Nikenda Kanigar Canada, kuna mji mmoja, kuna mbwa ndani ya uwanja wa ndege kwenye *migration*, anakuja mbwa kabisa mkubwa, tena mbwa yule usimfanye kitu, anakuangalia na anakunusa na mikoba yako, kama una unga unaambiwa kaa pembeni, wala hawana matatizo na wewe. Haya mambo ni muhimu sana yafanyike *checking*. Unga tatizo kubwa katika nchi za wenzetu ni kuingia nao mzigo, lakini mzigo kutoka sio tatizo. Kama Marekani mzigo kutoka hauna tatizo wewe toa, hata kama una unga wewe utoe, lakini kuingia kwenye nchi yao ndio tatizo. Jee, sisi kwenye nchi yetu tuna *checking* gani.

Mhe. Spika, hapa Uwanja wa Ndege wa Zanzibar kwenye miaka miwili ya nyuma Baraza lililopita tumeshuhudia sote sisi tuliokuwemo humu tunajua, umeletwa unga umekamatwa ndani ya uwanja wa ndege begi la unga, limekamatwa halijulikani limetoka wapi. *CCTV camera* mwisho unauliza zipo hazija-*record.* Sasa tunafanya vipi haya mambo. Kwa hivyo, uingizwaji unakuwa ndio muhimu na hatujui umeingia vipi ule unga. Kwa hivyo kwenye kuingia tuwe makini sana pale *camera* zifanye kazi tupate kuona na kujua tatizo liko wapi.

Kwa hivyo, *CCTV camera* hizi ni muhimu kwa upande wa uwanja wa ndege. Pia wageni wakifika pale mbwa wetu ahakikishe mizigo yote anainusa. Sasa hivi Dar es Salaam nawapongeza sana Mhe. Spika, wageni wakitoka nje wanasumbuliwa sana uwanja wa ndege wa Dar es Salaam. Ukiwa kijana, mzee, mtoto ni lazima waku-*check* vizuri. Mimi nitoe mfano mmoja Ugiriki nilipata historia moja zamani. Mama, mtoto na baba mtu, yaani familia ya watoto wawili na mama na mumewe wamechukua unga wote wametia kwenye viatu familia nzima, wewe utamuona mtu na familia yake anatembea lakini kumbe ana unga tayari. Kwa hivyo, biashara hii usim- *judge* mtu ukamuona huyu kijana na huyu mzee, unaweza kumuona mzee kumbe ana unga, ukamuona kijana kumbe ana unga au mtoto. Kwa hivyo, tuwe na *checking* ya watu wote na tuwe makini, hasa masuala ya mbwa haya, mbwa ndio anaweza kujua unga uko wapi, sio mashine zile zilizokuwepo uwanja wa ndege, zile mashine hazijui kama kuna unga kwenye viatu hazijui hazina uwezo huo. Kwa hivyo, mimi naomba sana tuangalie suala hili la ku-*check* haya mambo ya madawa ya kulevya.

Jambo jengine Mhe. Spika, tuangalie sana bandarini kama nilivyosema, makontena yanapotoka tuyaangalie mpaka yanapokwenda kuna usalama wafuatilie, kwa sababu na mzigo unakwenda halali lakini ule unga unakuwa hata mtu hauweki nyumbani kwake anauweka kwenye sehemu tofauti. Kwa hivyo, ni suala gumu sana kugundua na kujua unga huu uko wapi. Mimi

naomba sana mizigo kutoka bandarini pia kuna watu wawe wanafuatilia unapokwenda, unaposambazwa madukani na hata mtu *life style* yake iangaliwe, huyu mtu ana biashara gani, kuna kodi ya mapato na *TRA* mtuaangaliwe wewe una maisha haya, lakini kwa nini unamiliki kitu fulani na fulani umepataje, kuulizwa sio tatizo huko ndio kufanya uchunguzi ili mtu aeleze mimi nafanya biashara moja, mbili na faida yangu napata moja, mbili na tatu, tatizo liko wapi.

Suala jengine ninaloomba Mhe. Spika, Mhe. Mjumbe kasema hapa kwamba wauzaji unga anawajua, mimi naomba watangazwe hadharani, tusiwe tunachelewa sana kwa sababu mtu anapata kujipanga sasa hivi anakimbia na ile biashara anaiwacha analala Msikitini kabisa mtu anakuwa, ili mjuwe yeye ni mtu wa Dini hana mambo hayo, lakini tukitangaza tukimwita tutamuhoji moja, mbili, tatu tutapata kujua. Mimi naomba sana watangaziwe wafanyabiashara waletaji unga, hasa hao wakubwa, watangaziwe ili serikali ipate kuwahoji vizuri na kama wanaingia hatiaji basi wafungwe kwa sababu hili suala ni kubwa hasa kwa visiwa vyetu vya Unguja na Pemba matatizo haya yapo, na imekua sasa hivi kama hapa ni *transit* ya unga, unga unakuja hapa na ndege za usiku pale uwanja wa ndege.

Mhe. Spika, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano naelewa kwamba ndege za usiku sana zinawachukua mara nyingi wafanyabiashara wanaosafirisha unga kupeleka nje, hata ukitizama kila siku Mamlaka wanabadilisha askari, utakuta leo wamewekwa *JKU*, kesho polisi.

Mhe. Spika: Naomba umalizie Mhe. Mjumbe.

Mhe. Hussein Ibarahim Makungu: Kwa hivyo, mimi naunga mkono hoja na namshukuru sana Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kuliona hili na Mwenyezi Mungu amzidishie na serikali yetu iweze kufanya kazi vizuri ya kuwafichua hawa wafanyabiashara wote wa madawa ya kulevya, hasa kwenye dawa hizi za *cocaine.*

Nashukuru sana Mhe. Spika. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa naomba nimwite Mhe. Salma Mussa Bilal atafuatiwa na Mhe. Ali Salum Haji.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuchangia hoja ya Mhe. Mjumbe ya kuhusu ongezeko la uingizaji na utumiaji wa madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, naomba na mimi nimpongeze kwa dhati kabisa Mhe. Mohammed Said Mohammed kwa kuamua kuleta hoja hii mbele ya Baraza lako tukufu, hoja ambayo naweza kusema kwamba imechelewa kwa sababu tayari athari imeshakuwa kubwa, lakini pia niseme ni wakati muafaka imekuja.

Mhe. Spika, Wajumbe wengi wameshachangia na mengi ambayo nilipanga kuyachangia yameshazungumzwa. Lakini pia na mimi niseme kwamba madawa ya kulevya yamekuwa ni athari na yanatuathiri nadhani katika jamii yetu au katika sisi Wajumbe wa Baraza ni asilimia kubwa na sisi tumo waathirika wa tatizo hili. Kwa sababu tuna watoto, ndugu, wajukuu wote nao wameathirika. Kwa hivyo, kila mmoja wetu linamgusa. kwa hivyo ninamshukuru sana Mhe. Dimwa kwa kuleta hoja hii.

Mhe. Spika, mimi labda nianze na hivi dawa za *methadone* ambazo wanapewa hawa waathirika za kuwasaidia katika uachaji wa haya madawa ya kulevya. Dawa hizi zimekuwa zikitolewa katika Hospitali ya *Mental* tu, na ukizingatia kwamba hili janga hivi sasa limeenea nchi nzima mijini hadi vijijini, Unguja na Pemba. Halafu dawa hizi hawa waathirika wanatakiwa watumie kila siku, wanatakiwa waripoti pale *Mental* wanatumia halafu wanakwenda na siku ya pili wanakuja tena.

Mhe. Spika, na hawa vijana wetu wa vijijini, maana vijijini nako sasa hivi kumeathirika sana, vijana wetu wa vijijini wanataka sana kutumia dawa hizi, lakini wanashindwa wanakuwa hawana uwezo wa kuja mjini kila siku kupata huduma hii. Kwa hivyo, Mhe. Spika, mimi naomba sana Kitengo hiki kijitanue ili dawa hizi zisambazwe katika hospitali za Wilaya, hospitali za vijiji ili na hawa vijana wetu wa vijijini waweze kufaidika na dawa hizi, ili ziweze kuwasaidia katika uachaji wa kutumia madawa hayo.

Mhe. Spika, halafu jengine ni kwmba Mheshimiwa mtoa hoja alisema hapa kwamba Wakuu wa Wilaya, Masheha na wananchi tushirikiane katika kulipiga vita hili suala. Lakini mimi ningeomba kwamba sio tu tuanzie na Wakuu wa Mkoa. Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi ameshaanza, lakini hata na Mikoa mengine, kwa sababu kama nilivyosema kwamba utumiaji huu sasa hivi umesambaa nchi nzima. Kwa hivyo, naomba sana waanzie Wakuu wa Mikoa, Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi ameshaanza lakini na wakuu wa Mikoa mengine na wao walichukulie kwa uzito wake suala hili ili liweze kuchukuliwa hatua zinazofaa.

Mhe. Spika, mimi nathubutu kusema kwamba hizi *sober house* zinasaidia. Mimi niende kwenye *sober house*. *Sober house* kwa kiasi fulani zinasaidia kwa

sababu kuna wengine wakitoka *sober house* wanakuwa wanaacha kabisa kabisa, kuna wengine wakitoka *sober house* wanakuwa wanarudia. Sasa Mhe. Spika, mimi ninachoomba hizi *sober house* zitumike, tuwatumie hawa vijana wa *sober house* katika kutoa taarifa. Waheshimiwa waliotangulia walisema kwamba watumiaji ndio ambao wanashikiliwa, wakati watumiaji mimi nathubutu kusema kwamba ni wahusika, lakini sio wahusika zaidi kuliko hao wanaosambaza na wanaoingiza haya madawa.

Kwa hivyo, mimi nataka niseme kwamba labda niseme natoa na mimi mawazo yangu ya azimio kwamba hizi *sober house* tuzitumie kwa hawa vijana ambao wako *sober house*, hawa tuwatumie kwa kutoa taarifa kuhusu huu unga wao wanaupata wapi na wakishasema wanakoupata na wale ambao wanausambaza na wao waseme kwamba wameupata wapi hata mpaka wakaweza kuusambaza. Kwa hivyo, naomba *sober house* zitumike kwa ajili ya kutafuta au kuchunguza au kutafiti, hapo tunaweza kufanikiwa katika suala hili.

Jambo jengine Mhe. Spika, ningeomba kwamba, wenzangu wameshazungumza lakini na mimi natilia msisitizo kwamba mikakati izidishwe zaidi katika maingizo yote, uwanja wa ndege, bandarini, bandari bubu ifanywe mikakati ya makusudi ili tuweze kuzuwia janga hili lisiweze kuongezeka katika nchi yetu.

Mhe. Spika, kama nilivyotangulia kusema kwamba mambo mengi yalikwishazungumzwa na Kanuni haitutaki kurejea, lakini inabidi na sisi tutoe msisitizo kwa sababu hili janga ni kubwa na hili janga limeshatuathiri sana na linaendelea kutuathiri, na wakati umefika sasa tuweze kulizuwia hili jambo lisiendelee kutuathiri.

Kwa hivyo, namshukuru sana mtoa hoja na kwa haya machache ambayo nimezungumza, naomba kuunga mkono hoja hii kwa niaba ya wananchi au wanawake wa Mkoa wa Kusini ambao nawawakilisha kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mjumbe. Waheshimiwa Wajumbe, wachangiaji bado ni wengi na sitowapa wote. Kwa hivyo ningewashauri wengine wakachangia kwa maandishi. Nitawapa Wajumbe watatu tu kabla sijamwita mtoa hoja aje ahitimishe hii hoja, na bora niwataje kabisa, kwanza nilimwita Mhe. Ali Salum Haji nitampa yeye, halafu nitampa Mhe. Mwanaasha, halafu nitampa Mhe. Naibu Spika. Hawa wana muda mfupi sana wa kuchangia, halafu nitamwita Mhe. Mohammed Aboud, baadae nitamwita mtoa hoja. Mhe. Ali Salum Haji karibu.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Spika, na mimi nitajaribu kuchukua muda wako mfupi sana.

Kabla sijasema lolote Mhe. Spika, mimi naungana na mtoa hoja na naunga mkono hoja yake. Lakini Mhe. Spika, kuna maeneo tu ambayo na mimi napenda kutoa masikitiko kwa mtoa hoja katika maelezo aliyoyaeleza, ama hakuwa makini katika kufanya utafiti au amedanganywa na vitengo vinavyohusika Mhe. Spika. Hoja nzuri sote tunakubaliana nayo, lakini nasema kuna maeneo ama hakuwa makini au hakufanya utafiti, inawezekana ikawa anapotosha kwa kupitia watafiti waliompa.

Katika ukurasa wake wa 3 Mhe. Spika, chini kabisa inasema;

"kwa kuwa yapo maeneo maarufu ndani ya Zanzibar ambayo yanajulikana kwa kuwa na watumiaji wengi wa madawa ya kulevya ambapo kwa mujibu wa utafiti ulifanywa na Tume ya Kitaifa".

Ndio hapo niliposema inawezekana Tume au maeneo ya kisekta yamemdanganya. Mhe. Spika, ameyataja hayo maeneo kwamba ni Kundemba, Mlandege, Miembeni, Mikunguni, Mboriborini, Mwembeladu, Mwembeshauri, Jang'ombe, Kinuni, Mwembemakumbi, Kwahani, Kwaalinatu na Mpigaduri.

Mheshimiwa kama utaangalia humu Jimbo la Kwahani lina Shehia sita lakini Shehia tatu zimeingizwa humu Mhe. Spika, na si fikirii, mimi ndio Mwakilishi maeneo nayajua, inawezekana utafiti huo ulikuwa miaka ishirini sio miaka ya karibuni. Kuna maeneo hayavuti unga kabisa sasa hivi lakini cha kushangaza kwamba Shehia sugu na kama tutatoka mimi na yeye kwenda kuwachukua watu wa Shehia tatu na Shehia yake moja tu ya Mpendae, basi nina imani Mpendae inaongoza zaidi kuliko Shehia tatu kutoka jimboni mwetu. Kuna Shehia ya Mpendae Uwanja wa Taifa inaongoza kwa kutumia madawa ya kulevya. Mhe. Spika, naomba sasa hivi nichangie awe makini katika kufanya utafiti na asikubali kupewa ma-*document* ambayo hayana ukweli hata kidogo.(*Makofi*).

Mhe. Spika, michango yangu inakwenda katika maeneo haya moja nilita kutaja hayo maeneo ambayo yeye kayaacha. Eneo kubwa ambalo lilikuwa linatumika ambalo lilikuwa likitajwa ni eneo la Mji Mkongwe, ambalo lilifikia pahala Mhe. Mwakilishi akaanzisha Taasisi ya kuwachukua wavuta ungua na kwenda kuwapeleka katika ma-*sober* na kuwalipia, lakini humu halimo na ndio pale nilipomwambia kwamba utafiti wake unaonekana haukuwa yakinifu ama amedanganywa na vitengo vinavyohusika.(*Makofi*).

Mhe. Spika, napenda nimpongeze sana Mkuu wa Usalama Barabarani pamoja na kushirikiana na vikosi vya SMZ. Kwa nini nataka kusema hivyo Mhe. Spika, hawa wenzetu sasa hivi baada ya kutokana na kadhia ya ndugu zetu wa *T-one* walikuwa wanafanya operesheni ya mara kwa mara katika maeneo tofauti, hatimae jambo hili tumeweza kulidhibiti kwa asilimia kubwa. Sasa niwaombe Mhe. Spika, hichi Kitengo cha Kupambana na Madawa ya Kulevya, hebu wawafuate hawa wenzao ambao wanaonyesha bidii ya ulinzi katika nchi yetu, kuna nini.

Mhe. Spika, mimi nakifahamu hichi kitengo, nakifahamu sana wakati Mhe. Hamza Hassan Juma alipokuwa Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi, niliwahi kuwa mfanyakazi ambaye sio muajiriwa katika kile Kitengo. Mheshimiwa kile Kitengo kwanza hakina zana za kuweza kukabiliana na haya makazi, magari yao machache, zana zao ndogo. Lakini kuna baadhi ya mambo ambayo nilikuwa nayabaini katika utendaji wa kazi. Niliombe Jeshi la Polisi Mhe. Spika, kama ilivyokuwa tuna utaratibu wa wenyewe wanaujua wa kikazi wa kuhamisha watu kutoka eneo moja kwenda eneo jengine, hichi kitengo wafanyakazi wake wanachukua muda mrafu na wanakuwa wanajulikana, hata wanapotaka kufanya kazi zao inakuwa ni tabu sana. Maana yake akishuka tu katika eneo, mhusika akiwepo tu anaanza kujua huyo askari wameingia kwa sababu wanajulikana, yaani kazi zao zinakuwa tabu na ndio maana nikasema kipindi hicho Mhe. Hamza alisaidia sana Kitengo hichi alivyoamua kutumia magari ya binafsi, aliamua kutumia raia katika kupambana na masuala haya, na kwa kipindi kifupi suala la utumiaji wa madawa ya kulevya au uuzaji lilirudi nyuma kutokana na utaratibu ambao alikuwa akiutumia kipindi hicho Mhe. Hamza alipokuwa Waziri wa Nchi Afisi ya Waziri Kiongozi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa niwaombe wanajaribu kutumia utamaduni na kipindi kile kulikuwa kuna ofisa pale sijui kama ameshastaafu au vipi, Kamanda Kheri kwa kweli walifanya kazi moja kubwa sana. Sasa naomba tubadilike katika kutumia mbinu mbadala katika masuala ya kupambana na haya matatizo ya madawa ya kulevya. Mhe. Spika, hii kadhia ni kubwa sana na hakuna ambaye anaipenda lakini ndio janga limetukuta tunahitaji sote kutoa ushirikiano wa pamoja katika kuhakikisha kwamba tunapambana na janga hili.

Mhe. Spika, katika maeneo ambayo na mimi nataka nilizungumzie, hili suala la Mahakama lazima tukiri ukweli utabakia ni ukweli tu, baadhi ya Majaji wanasababisha suala la madawa ya kulevya Zanzibar kuendelea na wanasababisha kwa sababu tuna ushahidi, tukizungumza sisi humu sio kama tunapiga kelele tu. Mheshimiwa nina ushahidi wa mwananchi wa Jimbo la Kwamtipura alikamatwa na madawa ya kulevya akapelekwa Mahakamani

yakapita mazungumzo baina yake yeye na familia, Mhe. Jaji anafika kumwambia familia ya wanaohusika tafuteni mbinu huyu mwananchi aje achukuliwe dhamana lakini mjitayarishe nikimpa dhamana aondoke, huyo mtu mpaka sasa hivi yuko Uingereza. Sasa ndio maana tunafika pahala kusema kama tuna nia thabiti tutafika lakini inachoonekana baadhi ya maeneo hatuna nia thabiti na hususan katika haya maeneo yetu, kupitia Jeshi la Polisi, kupitia Mahakama na maeneo mengine watu wemetaja maeneo mengi hapa mapolo yaliyokamatwa *Airport* kesi hazijulikani, yaani unashangaa kinapita vipi hiki kitu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, sasa mimi niombe tu tuna kawaida sana Wazanzibari kutunga sheria nyingi lakini tuna tatizo la kutokusimamia sheria zetu ipasavyo ama kwa tamaa ama kwa ujamaa ama kwa njia nyengine yoyote, nina imani sheria tulizozitunga kama zitasimamia ipasavyo kihaki lillahi, basi tunaweza kutokemeza suala zima la madawa ya kulevya katika nchi yetu.

Mhe. Spika, nimesema sichukui muda wako mwingi, nakushukuru pamoja na kasoro nilizozitoa nataka niunge mkono ya hii ya Mhe. Mohammed Said Mohammed, hoja nzuri sana lakini narejea tena kwamba waliompa ushahidi au takwimu wamempotosha.

Mhe. Spika, nakushukuru. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa naomba nikutwite Mhe. Mwanaasha Khamis Juma utakuwa na muda mfupi halafu nitamruhusu na Mhe. Mgeni Hassan Juma achangie.

Mhe. Mwanaasha Khamis Juma: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii lakini nimeona nichangie hotuba hii au hoja hii ya Mjumbe iliyoletwa hapa kwa sababu na mimi naona inanigusa nikiwa kama mzazi au mlezi na hata kwa vile ni kiongozi.

Lakini pia Mhe. Spika, naomba nimpongeze sana Mhe. Mjumbe Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kwa hoja yake hii kwa sababu ameileta wakati muafaka na hili tatizo bado lipo Zanzibar na linaendelea kuwepo kwa hivyo nampongeza sana kuleta hoja hii, na kwa vile ametumia haki yake ya msingi kama ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kutumia Kanuni ambazo amezieleza hapa, kwa hivyo nampongeza sana.

Lakini Mhe. Spika, nije kwenye hoja. Hoja aliyoileta Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) kuhusiana na suala zima la madawa ya kulevya Mhe.

Spika, kwanza mimi nilikuwa nataka nigusie au nipongeze kwanza hii Tume ambayo imeanzishwa ya Kitaifa ya kuratibu na udhibiti wa dawa za kulevya. Lakini katika Tume hii imetaja maeneo hapa ambayo kama walivyotaja Wajumbe wenzangu Kundemba, Mlandege na maeneo mengine yaliyokuwemo katika hii hoja. Lakini bado naiomba hii Tume ya Kitaifa iratibu tena upya, inaonekana imeanza kuratibu labda kipindi cha nyuma lakini sasa hivi baada ya maeneo haya aliyoyataja inaonekana maeneo haya ni kidogo kwa janga hili la madawa ya kulevya.

Kwa hivyo naiomba sana Serikali kupitia tume hii ya kitaifa iratibu tena. Lakini Mhe. Spika, itakuwa sisi kazi yetu au hii Tume kazi yake ni kuratibu tu lakini jee, wametaja maeneo ambayo yameathirika na madawa ya kulevya ambayo wameyataja humu katika uratibu wao, ni hatua gani ambazo wamezichukua kukomesha au kutokomeza kabisa maeneo haya ambayo yametajwa hapa yasiwe kabisa na kuwepo haya madawa ya kulevya, badala yake siku hadi siku yanaongezeka ndio maana nikasema wafanye tena utafiti kwa sababu maeneo ni mengi na miji mingi na mitaa mingi bado haya masuala yapo.

Lakini Mhe. Spika, nije katika hizi *sober*. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuanzisha hizi *sober*, lakini sober hizi Mhe. Spika, hazitofanya kazi ikiwa wale wanaotoka katika zile *sober* wanarudi mitaani na wakirudi mitaani wanazikuta zile dawa za kulevya, sifikirii kama Serikali itakuwa imefanya kitu kizuri sana kuhusiana na kuwa wametengeneza *sober* ili kuwadhibiti wale vijana ambao wanahusika na madawa ya kulevya, baadae wakitoka kule tunaamini vijana wale wako vizuri na wanatoka kule wameshaacha yale madawa. Lakini wakija mitaani zile dawa wanazikuta na wakizikuta bado wanatumia. Kwa hivyo bado hapa Serikali kama wamejenga *sober* basi wadhibiti zile nyanja zote zinazopitisha madawa ya kulevya, la si hivyo tutajenga *sober* hata elfu kumi ndani ya Zanzibar lakini hazitazaa matunda kwa sababu wakirudi mitaani tayari zile dawa wanazipata.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nataka nije kwenye hizi sekta ambazo zimetajwa mfano Ofisi ya *DPP* na Polisi pamoja na Afisi ya Mkemia Mkuu. Mhe. Spika, nilikuwa naiomba Serikali vitengo hivi waviangalie sana au licha ya kuangalia, lakini wawe na mkabala mzuri wa mashirikiano katika utendaji wao wa kazi ili kuondosha kadhia hii, kwa sababu inavyosemekana au inavyoonekana Ofisi ya *DPP* na Askari Polisi hawana mkabala mzuri katika masuala mazima ya hizi kesi. Na hawa watu wote wanajenga nyumba moja na kama wanajenga nyumba moja kwa nini wasiwe na mkabala mzuri katika kufanikisha hizi kazi zao.

Mhe. Spika, lakini pia nilikuwa naiomba Serikali humu katika hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed katika maazimio yake, alikuwa anaiomba sana Serikali iimarishe ulinzi ikiwemo pamoja na kununua vifaa vya ukaguzi vya kisasa. Hivi Mhe. Spika, serikali haioni kwamba tayari mtoa hoja au watu wanalalamikia sana, mfano kwenye vyanzo vyetu vya usafiri kama Uwanja wa Ndege pamoja na bandarini, hizi ndio njia kuu au hizi bandari bubu. Hizi ndio njia kuu ambazo zinasababisha huu upitaji wa dawa za kulevya. Kwa hivyo Mhe. Spika, nilikuwa naomba Serikali iangalie sana lakini halikadhalika pale Uwanja wa Ndege kuna siku kunakuwa na ndege nyingi ambazo zinatua pale usiku hasa Jumanne na wageni wanaingia pale. Kwa hivyo hata ule uangalizi wake unakuwa sio mzuri, unapita tu unavyotaka. Kwa hivyo bado Serikali naomba sana suala hili ilitizame na ishughulikie kwa sababu waathirika wakubwa ni vijana na sisi wanawake ni walezi mara nyingi matatizo haya yanapotokea akina mama ndio tunaathirika sana na watoto wetu.(*Makofi*).

Kwa hivyo naiomba sana Serikali ichukue hatua za dharura au hata ichukue hata kemeo watamke hapa watwambie kwa suala hili litafikia hatua gani kuhusiana na masuala mazima ya dawa ya kulevya. Naona Mhe. Spika, unaiwashia *Mic* yako hapo kwa sababu muda umekwisha, lakini nampongeza sana Mhe. Mohammed Said Mohammed na naunga mkono hoja yake hii lakini naomba na Serikali ione hoja hii na maazimio haya wayabebe wayachukue na wayafanyie kazi kwa maslahi ya Zanzibar na maslahi ya vijana wetu wa Zanzibar.

Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa naomba nimwite Mhe. Mgeni Hassan Juma atafuatiwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Mhe. Mohamed Aboud kabla ya sijamwita mtoa hoja aje ahitimishe.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, ahsante sana na mimi kwa kunipa fursa hii nami niweze kuchangia katika hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed inayohusiana na masuala mazima ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa uwezo wa kuwepo hapa hii leo lakini pia nimpongeze sana Mhe. Dimwa kwa kuleta hoja muhimu sana kwa ajili ya maslahi ya taifa letu. Mimi sitozungumza sana lakini nimesimama hapa kwa sababu hoja hii mimi mwenyewe binafsi inanigusa sana, nimekuwa kwa kipindi kirefu nimeifanyia kazi nilipokua nje ya Baraza la Wawakilishi nikiwa kama mwanaharakati, lakini nimeweza

kutembea katika maeneo mbali mbali na nchi mbali mbali na niliona tatizo hili kwamba ni tatizo kubwa sana.

Mhe. Spika, tatizo hili halitaki masihara tatizo hili linataka kujipanga ikiwa kama tumeazimia kweli kuondosha tatizo la madawa ya kulevya lazima tujipange, kwa maana kwamba Serikali ijipange iweze vile vile ku-*invest* katika masuala mazima ya kuondoa madawa ya kulevya lakini na wananchi wake vile vile wawe tayari kusaidia Serikali katika suala zima la kuondoa madawa ya kulevya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, kuna masuala mazima ya rushwa, rushwa inafanyika sana katika suala zima la madawa ya kulevya, lakini kwa sababu katika maeneo mengi masuala ya madawa ya kulevya yanaripotiwa, ukianzia katika maeneo ambayo madawa ya kulevya yanakamatwa, lakini hata katika Mahakama zetu. Mhe. Spika, lakini tumeona kutokana na utafiti ambao unapatikana ni kesi chache sana ambazo kwa kweli zinapata hukumu, *almost* kama hamna kutokana na wale ambao wanakamatwa. Kwa hivyo hilo ni tatizo kubwa ni tatizo la rushwa na kama hatutoweza kulifanyia kazi tatizo la rushwa Mhe. Spika, ninasema suala zima la madawa ya kulevya litabikia kuwa hivi hivi, itabakia kama ni nyio sote kila siku tutakuwa tunakuja ndani ya Baraza kulipitia kelele lakini hakuna kitekachoweza kupatikana.

Mhe. Spika, tuna sheria moja ya *Money Laundry*. Hiyo Sheria Mhe. Spika, ni muhimu sana kutumika katika kuondosha tatizo hili, lakini tumeona sheria ile haina meno. Sheria ile kwa sababu itawakamata sana wale *finesses* ambao wanatumia vijana wetu kwenda kusafirisha madawa ya kulevya na kuyaleta hapa na mengine kuyapeleka katika nchi nyengine, tumekuwa tunapata majina mabaya nchi yetu kwa sababu kuna *finesses* ambao inawezekana wapo hapa Zanzibar au Tanzania, lakini inawezakana pia wako nje ya nchi wanaotoa fedha kwa ajili ya shughuli hii ya madawa ya kulevya.

Mhe. Spika, kuna watu ambao wapo hapa hapa Zanzibar hawajulikani wanafanya kazi gani, hawajulikani kama ni wafanya biashara, hawajulikani kama ni matajiri lakini wana uwezo mkubwa na watu hao wamekuwa wanatutambia sana katika mitaa yetu, wakichukua watoto wanawake wakiwadhalilisha kama wake, na wanawake kwa sababu ya uwezo wao wa fedha, Mhe. Spika, tatizo hili ni kubwa sana. Kuna watu ambao fedha, majumba, magari wanayomiliki unaweza ukajiuliza anapata wapi pesa, lakini hawa wanajulikana Zanzibar tunasema ni ndogo na tunajuana hana mbinu yoyote ya kuingia fedha, tujiulize Mhe. Spika, na hawa watu wanaoshughulikia masuala haya lazima waweze kufuatilia nyendo za hawa watu wanapata fedha

wapi. Nimesema Sheria ya *Money Laundry* wao ndio wengine wanazichukua pesa wanazipeleka huku na huku, lakini alimradi wanaweza kufanya mambo yao na kuchukua watoto wetu na kuwasafirisha na wakenda kudhalilika nje ya nchi ya Zanzibar. Mhe. Spika, hilo lazima Serikali ielewe kwamba kuna kazi kubwa ya kufanya.(*Makofi*).

Mhe. Spika, jengine ambalo nalisema tumegundua kwamba suala la madawa ya kulevya Serikali imekuwa inachukua jitihada kubwa sana. Kipindi kirefu sana kumekuwa kuna kampeni mbali mbali kuhakikisha lakini watendaji hususan polisi. Mhe. Spika, mimi kwetu ni Miembeni na Miembeni kuna tatizo kubwa sana la madawa ya kulevya, lakini watu wa Miembeni wanashirikiana na Polisi kutoa taarifa Mhe. Spika, ukienda Miembeni utafikiri pale ndio soko la madawa liko maalum kwamba hapa pametengwa kwa ajili ya kuuza madawa.

Mhe. Spika, Polisi wanapofika katika maeneo yale mnawaona wanatoka katika nyumba ambazo zinauzwa madawa ya kulevya wakifurahi na wakicheka, hilo ni tatizo. Pale kwenye makontena Michenzani Mhe. Spika, kuna watu wanajulikana anapotembea lazima atakuwa ana madawa ya kulevya anauza, hawakamatwi kwa nini na wakati wanajulikana na watu wanasema. Mhe. Spika, tatizo lipo kwenye Polisi wetu.(*Makofi*).

Mhe. Spika, naishauri Serikali kwa sababu hawa ambao wamepewa majukumu hayo ya kukamata watu kama wale hawafanyi kazi vizuri, tutafute sasa hii kazi iweze kufanya kazi vizuri tutafute *private investigators*, watu ambao watakuwa wanafanya kazi ambao hawana *interest* na hata tukitoa nje ya nchi lazima tu-*invest* kwenye jambo hili ili kuhakikisha kwamba wauza unga wanaondoka, hawana *interest* kabisa, watu ambao hawatokuwa tayari kupokea rushwa, wao ndio wataweza kufanya uchunguzi na kukamata watu hao. Lakini kila siku tukiwa na hawa hawa ambao kila siku tunawapigia makelele kwamba wao ndio wanaosababisha unga uuzwe Zanzibar vijana wetu waharibike wao hawatoweza kuifanya kazi hiyo. Nina wasi wasi mkubwa na Jeshi la Polisi Mheshimiwa kwa sababu bado tatizo la unga Zanzibar litaendelea kuwepo kama tukiendelea na mfumo huu huu na utaratibu huu huu wa kuhakikisha kwamba suala zima la unga linaondoka Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Spika, nichukue fursa hii vile vile kumpongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa kuona hili suala na kuweza kulifanyia kazi vizuri, na nampongeza Mkuu wa Mkoa wetu vile vile wa Mkoa wa Mjini/Magharibi kwa kuanza kufanya kazi vizuri. Mhe. Spika, ningewaomba wananchi wote wa Tanzania wasaidiane na vitengo ambavyo vinashughulika na masuala ya madawa ya kulevya, kwa

sababu madawa ya kulevya yameshatuulia. Mhe. Spika, mimi mdogo wangu mwenyewe amefariki kwa sababu ya madawa ya kulevya, akina mama wanaumia wanaumia, wazee wanaumia, kwa sababu ni suala ambalo linamgusa kila mtu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwakunipa muda wako wa kuweza kuchangia, nachangia hoja hii kwa asilimia mia moja, napongeza hoja hii kwa asilimia mia moja. Mhe. Spika, nakushuru. (*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante Mheshimiwa, Waheshimiwa Wajumbe nilitamani sana nimpe Waziri wa Habari, Utalii na Michezo kama dakika mbili tu kabla sijampa Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Dakika mbili tu Mheshimiwa.

Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo: Ahsante sana Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa dakika hizo chache ulizonipa na mimi sitaki kupoteza muda naunga mkono sana hoja ya Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), hoja hii ambayo kwa kweli ni thakili, inaumiza, inatesa kwa jamii, mataifa, mikoa na wilaya yetu ambayo tunaishi.

Mhe. Spika, suala la madawa ya kulevya kwa kweli ni vita, nataka tuungane kabisa ni vita vinavyopaswa kupigana kwani biashara hii ina mizizi mirefu na kuing'oa kwake, kunahitaji sana tena kwa zana nzito katika kuing'oa na sio tu kukaa tukaja tukaweza kusema kelele naweza kumtaja, naweza kumleta, naweza kusema hivi, kunahitaji mapambano makubwa sana.

Mhe. Spika, ukweli wa athari na majanga ya dawa za kulevya hazifananishiki na kitu chengine, zinazidi majanga ya moto zinazidi majanga ya mafuriko yana uzito wake. Mhe. Spika, nilichokuomba hata na mimi nikataka kutamani kupata dakika mbili ni kueleza wazi dhana ya utalii. Inaonekana wazi kuwepo kwa utalii wetu ni njia ndefu sana ni chanzo kikubwa kabisa cha kutumia madawa ya kulevya. Serikali ilivyoanzisha utalii ilikuwa na nia safi baada ya kuona uchumi wake umeporomoka. Hivyo nataka tuwajulishe wenzetu, Wajumbe wenzetu, wananchi kwa ujumla serikali haikuwa na lengo la kuanzisha utalii, kuanzisha mahoteli mengi, kuanzisha michezo ya bahari na vitu vyengine kwa nia ya kuweza kutumia njia hizi kuleta madawa ya kulevya. Lengo lake serikali ni kutoa huduma kwa wanaotaka kuja kutembea ki-kweli kweli, wanaotaka kupata huduma za Zanziabar, wanaotaka kujua vivutio vya Zanzibar, ili hatimaye serikali ipate uchumi wake.

Mhe. Spika, namalizia kwa kusema kwamba kwa kuongeza wigo wa utalii si kuongeza madawa ya kulevya. Tushirikiane pamoja tuhakikishe sote tunayapiga vita madawa ya kulevya na nchini petu yasiweze kuingia kwa kupitia hizi njia za utalii.

Nakushukuru sana Mhe. Spika.(Makofi).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mheshimiwa na ahsante kwa kutumia dakika mbili juu ya alama. Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili tafadhali, kama dakika tano hivi au zaidi kidogo unaweza ukatumia.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili: Mhe. Spika, nakushukuru kwa kuwa walionitangulia wote akiwemo na mtoa hoja hii wameeleza kwa undani tatizo lilivyo, ukubwa wake na shida yake katika kupambana nalo. Mimi kwa ufupi na mimi nichukue fursa hii nimpongeze mtoa hoja kwa namna alivyowasilisha hoja yake na maazimio yake. Lakini pia niwashukuru Wajumbe waliochangia hoja hii kwa ushauri walioutoa.

Mhe. Spika sisi kwa upande wetu kwa niaba ya serikali maazimio haya takriban yote yanafanyiwa kazi kila siku. Kwa hivyo kwetu sisi hatuna tatizo hata kidogo kuyapokea maazimio haya na kuyafanyia kazi kwa pamoja. Kutokana na uzito wa suala lenyewe naamini kwa michango ambayo Wajumbe wameitoa watatoa ushirikiano mkubwa katika kufanya kazi hii. Ni kweli kazi hii inahitaji ushirikiano wa pamoja katika kuitekeleza na ni kazi inayohitaji uadilifu na ukweli katika kutekeleza kwake.

Mhe. Spika, niseme Mhe. Rais wetu alishatoa muongozo, ameshatoa maelekezo ya namna ya kulisimamia jambo hili. Na nirudie kusema niliyosema katika Baraza hili, viongozi hawa kila mmoja ana-*style* yake katika uongozi, ana hekma zake, busara zake na utaratibu wake. Yeye Mhe. Rais ameshatoa maelekezo ya kutosha na anatuita mara kwa mara kuzidi kuelekeza ili kuzidi nguvu ya mapambano katika suala hili. Sasa nataka kwa umoja wetu tumpongeze Rais wetu kwa kazi hiyo anayoifanya ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mhe. Spika, ni kweli katika shughuli hii lipo tatizo la rushwa. Ni kweli wapo baadhi ya askari si waaminifu ambao wanatakiwa kutekeleza jambo hili. Kwa hivyo ushauri wenu tunaupokea na ni vizuri kuwe na Kikosi |Maalum cha askari walio waadilifu, walio tayari kupambana na jambo hili, wapewe kazi hii wafanye. Kwa sababu watekelezaji wa kazi hii ni askari Polisi kwa kushirikiana na vyombo nyengine vya dola, naamini wahusika wamesikia na sisi tutakao nao wenzetu tuwape mashauri ambayo mmetupa ili utekelezaji uwe sahihi.(*Makofi*).

Lakini napenda tuelewe kwamba maelezo ambayo yametolewa hapa mengi yanabidi mashirikiano yetu na wananchi pia katika kutoa taarifa. Lazima tushirikiane katika kupeleka taarifa vizuri na zilizo sahihi. Si vizuri sana orodha ile kuitaja hadharani haitusaidii sana. Maana unapotaja wahusika wataanza kutafuta mbinu nyengine za kuupoteza ushahidi. Mhe. Spika, lakini tutakapokuwa na orodha, tunaye Kamishna wetu wa Polisi, tunayo Tume hii inayoratibu na kudhibiti, ukiwapelekea orodha hiyo wataiwasilisha kunakohusika ili ifanyiwe kazi vizuri. Mhe. Spika, tukiiwasilisha hapa kwenye Baraza itakuwa ni *public document*, matokeo yake ni yale yale tumewataja, ukiwataja watajitayarisha kwa njia nyengine. Kwa hivyo utaratibu hautokuwa mzuri.(*Makofi*).

Mhe. Spika, na nirudie kusema kwamba Tume hii kazi yake ni ya kisera zaidi ya kutoa miongozo, lakini utekelezaji kwa mujibu wa sheria ni wa Jeshi la Polisi. Ndio wanapaswa kabisa kabisa kusimamia kazi hii vizuri. Mwenzetu mmoja alitushauri hapa kwamba sote tukiwa waadilifu, tukitekeleza sheria bila ya shuruti itatusaidia sana. Mimi nakubaliana kwamba nguvu za ziada zitumike katika mapambano haya ili kupiga vita jambo hili.

Mhe. Spika, limezungumzwa pia *sober house* hizi kwamba baadhi yake haziendani na malengo na matakwa zilizoanzishwa. Kwa hivyo tuwaambia wenzetu wa Tume wazidi kufanya utafiti zaidi, wapeleleze zaidi, *sober* sote zenye sifa mbaya zifungwe na zile ambazo zinafanya wajibu wake ndizo hizo ziendelee kusaidia jamii yetu. Dhamira ya serikali kuwa na *sober* ni kuhakikisha kwamba wale walio tayari kujirekebisha baada ya gonjwa hili hatari kuwasibu tusaidiane nao ili tupate raia wema warudi kufanya kazi na wananchi wenzao. Mhe. Spika, kwa sababu mulisema hapa kama nguvu kazi inapotea, hatuwezi kama serikali kuwaachia vijana hao wakaendelea kusumbuka wakati wapo tayari kushirikiana na wenzao na kujenga taifa lao. Ni jambo muhimu kuwa na *sober* hizi ambazo zinatekeleza wajibu wake. Mhe. Spika, tutakayemgundua yeyote ndani ya *sober* au mtu ameanzisha *sober* kwa minajili ya kuharibu badala ya kutengeneza tutamshtaki kwa mujibu wa sheria ili tuhakikishe kwamba *sober* zinakuwa safi.

Mhe. Spika, ni tatizo kubwa kupambana na waletaji lakini tunapoyakamata haya maduka yanayouza unga na watu wameyataja na orodha ipo, sasa ni kazi ya Polisi kwenda kuwakamata wahusika, ukiwakamata hao, ukiwafanyia upelelezi vizuri watataja wameupata wapi, wakitaja walipo upata na hao tunaowaita mapapa nao watatambulikana. Kwa hivyo sote tushurikiane, maana kuna wengine ni waletaji na washiriki wakuu katika biashara hii haramu, lakini hujifanya watu wema sana, hujifanya watu wa Dini sana, watu wanaosaidia

watu sana. Kwa hivyo jamii ni lazima sote tuwaelewe hao ili tupambane nao kwa pamoja na tuikatae misaada yao na tuwaambie kwamba nyinyi hamna imani na tuwatolee taarifa. Kwa sababu wanajipendekeza kwa viongozi, wanajipendekeza kwa askari, wanajipendekeza kwa Wajumbe humu ndani, wanajipendekeza kwa kila mmoja, tuwatambue hao, tukiachana nao itatusaidia kwa njia moja ama nyengine kuendeleza vita hivi.(*Makofi*).

Mhe. Spika, mambo yalikuwa mengi ya kuyasema hapa lakini kutokana na muda wako nauona huu, siwezi kuendelea kusema zaidi, zaidi ya kusema maazimio haya sisi kwa upande wa serikali tunayapokea na tutayafanyia kazi, isipokuwa tufanye marekebisho madogo kwenye namba 8, pale inaposema "Pamoja na juhudi za serikali za kuwatoa vijana katika matumizi ya dawa za kulevya tunaomba sana serikali ianzishe operesheni maalum kuwasaka wanawake", baada ya kusema neno "kuwasaka wanawake", tuseme neno "kuwasaka wahusika wote" iwe ni kuwasaka wahusika wote kama ambavyo mtoa hoja alirekebisha.(*Makofi*).

Naomba tukifanya marekebisho hayo basi sisi hii tunaipokea na tuko tayari kushirikiana ili tukafanya na kupambana na suala hili la madawa ya kulevya katika nchi yetu. Naamini kwa pamoja tunaweza.

Ahsante sana Mhe. Spika.(*Makofi*).

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Mheshimiwa Mtoa hoja naomba uje uhitimishe hoja yako tafadhali.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru sana na niwashukuru Wajumbe wote kwa kuonesha imani na moyo thabit kwa kuweza kuiunga hoja yangu mkono. Mhe. Spika, idadi ya Wajumbe wote waliochangia ni 43, walionchangia moja kwa moja ni 17 lakini 25 wamechangia kwa maandishi.

Mhe. Spika, naomba niwataje ili tu basi tuone tunavyokwenda.

1) Mhe. Zulfa Mmaka Omar
2) Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis
3) Mhe. Hidaya Ali Makame
4) Mhe. Asha Abdalla Mussa
5) Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
6) Mhe. Nadir Abdu-latif Yussuf
7) Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali

8) Mhe. Omar Seif Abeid
9) Mhe. Viwe Khamis Abdalla
10) Mhe. Bihindi Hamad Khamis
11) Mhe. Hassan Khamis Hafidh
12) Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
13) Mhe. Salma Mussa Bilal
14) Mhe. Ali Salum Haji
15) Mhe. Mwanaasha Khamis Juma
16) Mhe. Mgeni Hassan Juma
17) Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
18) Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais

Mhe. Spika, waliochangia kwa maandishi ni:-

1) Mhe. Rashid Makame Shamsi
2) Mhe. Waziri wa Afya
3) Mhe. Bahati Khamis Kombo
4) Mhe. Simai Mohammed Said
5) Mhe. Zulfa Mmaka Omar - yeye alichangia mara ya pili
6) Mhe. Tatu Mohamed Ussi
7) Mhe. Miraji Khamis Mussa
8) Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
9) Mhe. Juma Ali Khatib (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
10) Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa
11) Mhe. Yussuf Hassan Iddi
12) Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
13) Mhe. Naibu Waziri wa Afya
14) Mhe. Hamida Abdalla Issa
15) Mhe. Maryam Thani Juma
16) Mhe. Suleiman Makame Ali
17) Mhe. Ussi Yahya Haji
18) Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo - ambaye alichangia alipata nafasi tena
19) Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiyekuwakuwa na Wizara Maalum)
20) Mhe. Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora
21) Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
22) Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
23) Mhe. Hamza Hassan Juma
24) Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo

25) Mhe. Zaina Abdalla
26) Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi

Mhe. Spika, wote kwa umoja wao wamekwenda katika sehemu nyingi tofauti, lakini kwa yote kwanza kabla ya muda haujanipita nilisema kutokana na michango yote mizuri ya Waheshimiwa Wajumbe tuseme basi tuongeze yale mapendekezo yangu ya maazimio. Lakini lile azimio alilolitaja Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais tayari nilikuwa nimekwisha kulisawazisha lakini sasa na yeye amelisawazisha nadhani tutakwenda pamoja.

Sasa niombe tu kutokana na michango mizuri ya Wajumbe tuongeze maazimio mawili kama ifuatavyo:-

1) Serikali iunde Mahakama Maalum ya kushughulikia kesi za dawa za kulevya kama ilivyo Mahakama ya Ardhi, Biashara au Mahakama ya Wahujumu Uchumi.

2) Ifanye marekebisho katika Sheria ya Dawa za Kulevya kwa kuongeza makosa ya usafirishaji, kuuza, kukutwa na kemikali badhirifu.

Kwa sababu wengine wanaleta kemikali zenye ashiria lakini bado haziwezi kukamatwa. Sasa tungeomba serikali ifanye sheria hizo. Lakini ya tatu hii nimeichukua kutokana na hoja kubwa nzito aliyoitoa Mhe. Naibu Waziri wa Elimu kuhusiana na viongozi, tumesema na hii tunaomba tuiongeze.

3) Viongozi wa Kisiasa hasa Wawakilishi, Madiwani na Wabunge washiriki kikamilifu katika vita vya kupambana na dawa za kulevya ikiwa ni pamoja na kufanya midahalo ya kitaifa kuhusu namna ya kuimarisha tatizo hili katika maeneo yetu. Wote kwa umoja wetu wana siasa tuweze kushiriki katika midahalo mbali mbali ili tuone jamii yetu imekuja vizuri.

Mhe. Spika, wengi tunaweza kupaswa wameelezwa hasa *DPP*, udhaifu wa *DPP*. Mimi natambua jitihada kubwa zinazofanywa na watendaji wa Ofisi ya *DPP* na nimetoa takwimu. Lakini licha ya juhudi hizo inasemekana kuwa kuna baadhi ya watendaji wasio waaminifu dhidi ya mapambano ya dawa za kulevya hutoa mambo ya siri au hutoa vitu vya siri. Sasa hili tukae na *DPP* tuweze kuzungumza naye, tuweze kuwaona wale watendaji ambao sio waaminifu kitu gani kinafanywa.(*Makofi*).

Mhe. Spika, jengine dhana ya uhuru wa Mahakama, wengine wamesema Mahakama, *DPP* na Polisi hazifanyi kazi vizuri, mimi naamini lakini sio wote. Lakini nasema natambua kuwa Mahakama kuwa ni muhimili ambao unajitegemea Kikatiba na kutenda shughuli zake ipo huru kabisa. Lakini pia Baraza la Wawakilishi haliwezi kuingilia shughuli za Serikali au Mahakama kwa sababu ni mihimili miwili tofauti. Lakini pamoja na uhuru huo Baraza hili limekuwa linakosoa serikali yake pale ambapo inaona pana kasoro.

Lakini vile vile Mhe. Spika, na Mahakama nayo iunde Tume ya kuweza kuona inaweza kuchunguza Mahakimu wake wanaoshughulikia kesi hizi, ili kubaini basi yupi anafanya. Ikiwezekana basi ni kuvuliwa vyeo au madaraka ili tukiona kwamba wanakwenda sivyo. Katika hoja yangu na maazimio yangu ya mwanzo nimewataka ZAEKA wafanye kazi hii. Lakini wafanye kazi kwa uadilifu ili tuone mwendo wa Mahakama katika katika kusikiliza kesi za madawa ya kulevya inakuwa sahihi sana.

Lakini vile vile mapendekezo mengine, haya sio maoni, haya ni mapendekezo kwamba serikali iunde Tume ya kuchunguza mwenendo wa kesi za Mahakama watakaobainika wadhifa au madaraka wanaotumia vibaya, basi wateremshwe na waondoshwe kabisa. Niungane na Mhe. Mgeni Hassan Juma alivyosema kwamba tutafute *private investigator*.(Makofi).

Mhe. Spika, natambua sana jambo hili kwa sababu tumekuwa tupo familia na watu hawa kwa muda mrefu. Lakini tukitafuta *private investigator* itakuwa ni vyema kutubainishia ukubwa wa jambo hili linapotokea. Niseme tu Mhe. Ali Salum Haji (Kirova) amesema Mpendae, wapi najua lengo lilikuwa ni nini. Lakini niseme tumechukua mawazo yako kama Mhe. Mwakilishi na watu wangu wa Tume walivyonipa hii hata mimi niliwauliza maeneo fulani lakini wakanambia Mpendae imeungana na Jang'ombe yote katika takwimu zao. Kwa hivyo hilo lako lililoonekana tutalichukua na tutalifanyia kazi kwa haraka zaidi.

Mhe. Spika, kwa hayo machache sana naungana na wote na natambua muda wako sasa naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mohamed Said Mohamed, Waheshimiwa hoja imetolewa na awali iliungwa mkono, lakini nachukua nafasi hii sasa kuwahoji wale wote wanaokubaliana na mapendekezo ya hoja ambazo zimetolewa na Mhe. Mohamed Said Mohamed (Dimwa) wanyanyue mikono yao, wanaokataa. Waliokubali wameshinda.(*Makofi).*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mheshimiwa kwanza kabisa nichukue nafasi hii kukushukuru sana kwa hoja yako. Hii hoja ni muhimu sana na inagusa maeneo yote ya nchi na haya mapendekezo ambayo yametoka si ya serikali tu lakini hata sisi tunapaswa kuyafanyia kazi.

Shukurani yangu ya pili Waheshimiwa inakwenda kwa Waheshimiwa wanawake ile Semina ya UWAWAZA imefanya kazi vizuri, kwa sababu wachangiaji wa mwanzo karibu wote walikuwa wanawake kama watu watano halafu baadaye tena, maombi pia yalikuwa mengi na wengi walikuwa ni wanawake ambao walipenda sana kuchangia hoja hii.

Tutaendelea jioni saa 11 kuna hoja nyengine ambayo inakuja. Kwa hivyo, tutaomba nayo ichangiwe kwa sababu tumetengua Kanunu ya Muda ili watu wachangie dakika kumi kumi mpaka hiyo jioni.

Kwa hayo mchache Waheshimiwa naomba kusitisha shughuli za Baraza mpaka saa 11:00 Alaasiri ya leo.(*Makofi*).

(Saa 5.57 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

HOJA BINAFSI

Maazimio Kuhusiana na Uimarishaji wa Mfumo Mzima wa Kisheria Unaohusiana na Uendeshaji wa Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto, Zanzibar

(Mhe. Mwenyekiti Mwanaasha Khamis Juma Alikalia kiti)

Mhe: Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako. Mhe. Mwenyekiti naliomba Baraza lako tukufu kutoa maazimio kuhusiana na Uimarishaji wa Mfumo Mzima wa Kisheria Unaohusiana na Uendeshaji wa Kesi za Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto, Zanzibar chini ya kanuni ya 27(1), (n), 27(3), 48(2), na 49(1) ya Kanuni ya Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, maelezo ya hoja kwa kuwa, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeundwa kwa nia ya dhati ya kupambana na matatizo yanayowakabili wanawake na watoto nchini kwa kuchukuwa hatua mbali mbali ambazo zinaonekana kuwa na lengo la kuwaweka wanawake na watoto katika mazingira salama.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka 2011 Sheria maalum yaani (Sheria ya Mtoto Nam. 6 ya mwaka 2011), inayohusu maslahi ya jumla ya mtoto iliwasilishwa Barazani na kupitishwa na hatimaye kutiwa saini na Mhe. Rais ambapo kifungu cha 150 cha Sheria hiyo kinakataza vitendo vya udhalilishaji wa watoto. Aidha, katika mwaka 2016, Serikali ilileta ndani ya Baraza la Wawakilishi, Mswada wa Sheria ya kufuta Sheria ya Ushahidi na kutunga Sheria mpya ya Ushahidi, ambayo ina nafasi kubwa katika kukabiliana na kesi za udhalilishaji, na hatimaye kupitishwa na Baraza la Wawakilishi, na kutiwa saini na Mhe. Rais na kuwa Sheria yaani (Sheria ya Ushahidi Nam. 9 ya 2016).

Mhe. Mwenyekiti, hata hivyo**,** licha ya kuwepo kwa jitihada hizo, bado vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto, kama ubakaji, ulawiti, kupigwa, kupewa ujauzito, kuambukizwa magonjwa ya zinaa kama UKIMWI, na kadhalika, vimekuwa vikiongezeka kwa kasi sana kadri siku zinavyokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuhakikisha haki inapatikana wakati vitendo hivi vinapofanyika na kuhakikisha wahusika wanachukuliwa hatua za kisheria, Serikali imekuwa ikichukua hatua za makusudi za kuimarisha mfumo mzima wa sheria ambao unahusika katika kuyakabili matatizo haya, lakini bado kuna changamoto kubwa ya kukabiliana na ongezeko la vitendo hivyo.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa, mbali na hatua zilizochukuliwa na Serikali katika kuimarisha mfumo wa Sheria unaohusiana na kesi hizi za udhalilishaji, bado ipo haja ya kuchukua hatua za haraka za kubadilisha mfumo wa kisheria unaohusika na kesi za udhalilishaji kwa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa, pamoja na kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji wa watoto na wanawake nchini, bado kuna idadi ndogo ya kesi zinazofikishwa katika Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kwa ajili ya kupelekwa Mahakamani, ukilinganisha na kesi zinazoripotiwa katika vituo mbali mbali. Katika mwaka 2016, kwa taarifa ya Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa Kamati ya Mifugo, Utalii, uwezeshaji na Habari ya Baraza la Wawakilishi, inaonyesha kuwa jumla ya matukio 2,346 ya udhalilishaji wa kijinsia yaliyoripotiwa katika vituo vya Polisi Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ambapo kati ya matukio hayo, ni kesi 105 tu ndizo zilizoripotiwa kwenye Mahakama za Unguja na Pemba. Ufafanuzi zaidi unaoneshwa katika jadweli lifuatalo:-

Mhe. Mwenyekiti, makosa yaliyoripotiwa katika vituo vya Polisi vya Mikoa ya Zanzibar katika mwaka 2016 ni kama ifuatavyo:-

MAKOSA YALIYORIPOTIWA VITUO VYA POLISI MIKOA YA ZANZIBAR KATIKA MWAKA 2016.

Idadi Ya Kesi	Kesi Zilizochini Ya Upelelezi	Zinazoendelea Mahakamani	Zilizopatia Hatia	Kuachiwa Huru Mahakamani	Zimefungwa Polisi	Mkurugenzi Wa Mashtaka
2346	1944	142	13	5	242	155

Mhe. Mwenyekiti, taarifa ya matukio ya udhalilishaji yaliyoripotiwa vituo vya mkono kwa mkono kwa mwaka 2016.

Mhe. Mwenyekiti, jumla ya kesi hizo ni:-

TAARIFA ZA MATUKIO YA UDHALILISHAJI YALIYORIPOTIWA VITUO VYA MKONO KWA MKONO, 2016.

KUKASHIFIWA	KUBAKWA	KULAWITIWA	UJAUZITO	JUMLA
344	513	35	121	1013

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa, vitendo hivi vimewekwa katika orodha ya makosa ambayo mtuhumiwa anayo haki ya kupatiwa dhamana, na kurudi katika jamii kuendelea na shughuli zake kama kawaida, Kifungu cha 150(1) cha Sheria ya Makosa ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, 2004, hakikujumuisha makosa haya ya udhalilishaji kuwa ni miongoni mwa makosa hayo hayatakiwi kupewa dhamana, hivyo kupelekea Mahakama kuwapatia dhamana watuhumiwa wa kesi za udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, utoaji wa dhamana kwa watuhumiwa hao, umewafanya baadhi ya watuhumiwa kurudia makosa hayo hayo mara baada ya kuachiwa kwa dhamana na hivyo kuathiri kwa kiasi kikubwa watoto, wanawake na jamii kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti na kwa kuwa**,** adhabu wanayopewa wahusika wanaotiwa hatiani kwa makosa ya udhalilishaji ni ndogo ambapo kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Namba. 7, ya mwaka 2004, inaipa Mamlaka Mahakama ya Mahakimu wa Mkoa ambapo kesi hizi zinaanzia, kutoa adhabu isiyozidi miaka **7** tu.

Mhe. Mwenyekiti, ambapo kiuhalisia haiendani na athari anayoipata muhusika aliyetendewa udhalilishaji, kama athari ya kimwili, kiakili, kupata mimba za umri mdogo ambazo hupelekea kuwa na ongezeko la watoto wa mitaani.

Mhe. Mwenyekiti, kuwaharibia wasichana wadogo malengo yao ya kimaisha, kushindwa kuendelea na elimu na madhara mengineyo.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa, makosa yanayohusu udhalilishaji, hufanyika kwa usiri mkubwa, kunakuwa na changamoto kubwa ya kuthibitisha nani ametenda kosa hilo na hivyo katika nchi nyingi na hata wenzetu wa Tanzania Bara, njia inayotumika ya kutumia mashine ya kisasa ili kuweza kujuwa vinasaba vya muhusika *(DNA)* ili kuthibitisha kosa, ambapo kazi hiyo huwa ni rahizi zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa, kutokana na kukosekana kwa uwelewa au kwa makusudi, kumekuwa na tabia ya wahusika wa kesi hizi kuchukuwa hatua za kusuluhishana na hatimae kuzifuta kesi hizi katika hatua ya vituo vya Polisi, hali inayopelekea watuhumiwa kuendelea kurudia vitendo hivyo kwa kuamini kwamba hakuna hatua za kisheria zinazoweza kuchukuliwa dhidi yao.

Mhe. Mwenyekiti na kwa kuwa**,** vyombo vinavyoendesha kesi hizi vimekuwa vinapata changamoto kubwa ya wananchi kutokutoa ushirikiano hasa katika kutoa ushahidi, kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo, usumbufu, muhali, tatizo la usafiri wa kwenda na kurudi Mahakamani, vitisho, pamoja na kukata tamaa kutokana na kesi kuchukuwa miaka mingi kabla ya kumalizika.

Mhe. Mwenyekiti, na kwa kuwa**,** kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi, kwamba baadhi ya vyombo vilivyopewa dhamana ya kushughulikia kesi hizi vimekosa uadilifu katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo, hali

inayopelekea wananchi kutokuwa na imani na vyombo hivyo na kupelekea kushindwa kutoa ushirikiano.

Mhe. Mwenyekiti, hivyo basi mimi Asha Abdalla Mussa, Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, Zanzibar, Jimbo la Kiwengwa, chini ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2016, naliomba Baraza hili Tukufu, kwa kutumia Mamlaka iliyo nayo, liridhie na kupitisha maazimio yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, azimio la kwanza katika Bajeti ya mwaka 2017/2018, Serikali iliweke suala la kupambanana na kutokomeza vitendo vya udhalilishaji wa wanawake na watoto kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ili kuweka mazingira mazuri ya kupambana na vitendo hivi vya udhalilishaji, ikiwemo kuviwezesha vituo vya mkono kwa mkono kufanya kazi zake kitaalamu na kwa uhakika pamoja na kuviwezesha vituo hivyo kufanya kazi kwa masaa 24 ili kushughulikia kesi wakati wote zinapojitokeza.

Mhe. Mwenyekiti, azimio la pili Serikali katika Bajeti ya mwaka 2017/2018 iweke utaratibu maalum wa kupunguza vifungu vya fedha kwa kila Bajeti ya Wizara ili kuweza kupata fedha za ununuzi wa mashine ya DNA**.** *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, azimio la tatu ili kuipatia jamii uelewa wa matatizo haya, Serikali iandae siku maalum ya kupinga udhalilishaji wa wanawake na watoto Kitaifa, ambayo itaadhimishwa kwa kutoa mafunzo mbali mbali yanayohusiana na kupiga vita udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nne Serikali, ndani ya mwaka mmoja, ilete katika Baraza la Wawakilishi, Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, Namba 7, ya mwaka 2004, ili kuongeza mamlaka ya Mahakama za Mkoa kutoa adhabu zaidi ya miaka saba 7, na kufanya marekebisho ya kifungu namba 150(1**),** ili kuingiza makosa ya kujaamiiana kuwa miongoni mwa makosa yasiyopatiwa dhamana.

Mhe. Mwenyekiti, tano pamoja na marekebisho hayo, Serikali iweke utaratibu wa kisheria wa kuwachukulia hatua kali wahusika wa kesi ambao watachukuwa hatua ya kusuluhishana katika ngazi ya kijamii na kufuta kesi za udhalilishaji na wale watakaokataa bila ya sababu za msingi, kutoa ushahidi na watakaovuruga ushahidi wa kesi hizo.

Mhe. Mwenyekiti, sita Serikali, iunde Tume ambayo pamoja na kufuatilia mambo ya jumla yanayosababisha kuongezeka kwa kesi za udhalilishaji lakini pia ifanye utafiti wa kina ili kujua sababu zinazosababisha idadi ya kesi

zinazoripotiwa kwa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka yaani (DPP) kuwa ni kidogo ukilinganisha na idadi ya kesi zinazoripotiwa na wananchi katika vituo mbali mbali. Aidha, Tume hiyo ifanye uchunguzi ili kubaini wale ambao wamekuwa wakikiuka maadili ya kazi zao na kusababisha kesi hizi kuongezeka siku hadi siku na kupendekeza adhabu kali za kisheria na kinidhamu zichukuliwe dhidi yao, na ripoti ya Tume iwasilishwe ndani ya Baraza kwa ajili ya kujadiliwa.

Mhe. Mwenyekiti**,** saba bila ya kuathiri uhuru wa Mahakama, uandaliwe utaratibu wa kuharakisha muda wa kusikiliza na kutoa hukumu katika kesi za udhalilishaji ili haki itendeke kwa wakati.

Mhe. Mwenyekiti**,** nane Kamati husika ya Baraza la Wawkilishi ijumuishe katika ripoti yake ya kila mwaka, namna inavyosaidia katika kupambana na tatizo hili la udhalilishaji wa watoto na wanawake nchini.

Mhe. Mwenyekiti, tisa Serikali kupitia Wizara husika, ilete mbele ya Baraza, ripoti ya namna inavyolishughulikia tatizo hili katika awamu *(periodic reports)* ili wajumbe wa Baraza wapate fursa ya kusaidia fikra na mikakati ya kupambana na tatizo hili.

Mhe. Mwenyekiti**,** kumi Serikali iandae utaratibu maalum wa kuzifuatilia na kuzisimamia nyumba binafsi za kulelela watoto, ili kuhakikisha kwamba watoto wanalindwa na kuwa katika mazingira salama.

Mhe. Mwenyekiti, kumi na moja Serikali iwe na program maalum kwa ajili ya kuwapatia elimu mahakimu na wahusika wengine, elimu ambayo itawashajihisha na kuwapa muamko wa kuweza kuzipa kipaumbele kesi hizi wakati zinapofika mbele ya Mahakama na vyombo vengine.

Mhe. Mwenyekiti, kumi na mbili Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wakiwa kama Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi za Mikoa na Wilaya, waongeze kasi ya namna ya kupambana na vitendo hivi vya udhalilishaji katika maeneo yao.

Mhe. Mwenyekiti azimio la mwisho uwepo utaratibu maalum kupitia kwa masheha kuweza kupeana taarifa juu ya wahusika wa matukio ya udhalilishaji, ambao wanahama kutoka shehia moja kwenda nyengine, ili kuweza kuchukua tahadhari juu ya watu hao, kabla hawajafanya vitendo vya udhalilishaji dhidi ya watoto na wanawake.

Mhe. Mwenyekiti**,** naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Jimbo la Kiwengwa kwa hoja yako na naona hoja imeungwa mkono naomba niwahoji. Waheshimiwa mjadala unaendelea mchangiaji wa mwanzo naomba nimwite Mhe. Bahati Khamis Kombo, akifuatiwa na Mhe. Ali Suleiman Shihata na Mhe. Salma Bilali ajitayarishe.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante saana Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia hoja hii ya mjumbe mwenzetu kwa upande wa wanawake tunasema UWAWAZA.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze pongezi nyingi sana mtoa hoja kwa kuona kwamba ana uchungu mkubwa sana wa kitendo cha udhalilishaji na ubakaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, hoja hii imekuja wakati muwafaka kwasababu mwezi huu tarehe 8 ndio mwezi wa Siku ya Wanawake Duniani *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, namuunga mkono mjumbe mwenzetu kutetea haki zetu, kutetea haki za watoto wetu kwa sababu vitendo vya udhalilishaji vimetugusa sisi wanawake na wanawake ndio tunathirika zaidi ndani ya vitendo hivi.

Mhe. Mwenyekiti, kumezuka mtindo hata walimu wa Madrassa kuwadhalilisha watoto na wengine kuwalawiti wanaume wakati ni wanafunzi wao naiomba Serikali wale walimu ambao wanafanya vitendo hivi viovu wachukuliwe hatua kali na ionekane kwamba hatua zile ni fundisho kwa wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nawaomba polisi, nawaomba madaktari na pia naiomba mahkama zinapopelekwa vitendo hivi basi vichunguzwe kwa umakini sana na pia zisiwekwe wakati mrefu wa kutolewa hukumu kwasababu tumeona kwamba vikiwekwa vitendo hivi hukumu ikiwa kwa siku nyingi basi vitendo vile vinaamuliwa kwamba ushahidi haukupatikana na wakati mwengine ushahidi uko sahihi lakini mwenye kufanya vitendo vile tayari keshatoa rushwa na tayari kesi ile imeshafutwa. Mhe. Mwenyekiti, tumechoka kudhalilishwa na tumechoka kudhalilishiwa watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, imejitokeza kuwa zinapotokea kesi kama hizi kuna baadhi ya kinamama au kibaba kukubali kupewa fidia juu ya watoto wao au wao wenyewe kinamama binafsi ili kesi zile zisiendelee. Tunawaomba wanawake wenzetu hili wasilikubali na sisi tuko tayari kwa hali na mali kama UWAWAZA kulisimamia na kuwasimamia wao ili wapate haki yao iwe sawa kama wanawake wengine.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea hivi sasa kumejitokeza sisi wenyewe kinamama tuna hofu kubwa hata kwa waume zetu na pia kwa wazazi wetu na hata kwa ndugu zetu tunaowaacha nyumbani kukaa na watoto wetu, kutokana na hali hii iliyojitokeza ambao ni tishio kwa nchi nzima juu ya udhalilishaji na ubakaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea vile vile ni juzi tu wakati tuko *Z Ocean* kimetokea kitendo hiki ambacho kuwa watoto walidhalilishwa kwa kupigwa na tukaamua UWAWAZa twende usiku ule ule tukiongozana na mwenyekiti wetu kwenda kuhakikisha tukio lile kweli limetokea au laa. Tulipokwenda ni kweli tukio lile limetokea na sisi kama UWAWAZA tumekaa na mwenyekiti wetu na kulipiga vita kiasi cha kutosha tatizo lile na kumtaka mwalimu mwenye kufanya kitendo kile basi aweze kuhukumiwa. Tunaiomba serikali iendelee na iendelee tena zaidi kupiga vita udhalilishaji na ubakaji wa watoto.

Mhe. Mwenyekiti, wanawake hatuna raha, kuna baadhi ya wanawake wengine wana miradi tafauti, wengine wanakweda shamba kulima, wengine wanaokota makozi na wengine wanakwenda pwani kwa ajili ya kuchukua samaki kuja kuuza, lakini sasa hivi baadhi ya wanawake wakimuona mwanamme yuko mbele yao tayari roho ishawashituka anaona anakuja kubakwa tumechoka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wanawake wenzangu UWAWAZA tunawaomba wanawake wenzetu wote wasikubali kufanyiwa udhalilishaji juu ya jambo hili. Lakini pia tunaiomba serikali sisi wanawake kwamba ituridhie na itukubalie tuunde tume maalum sisi kwetu ili tuweze kushirikiana na Mahakama kuzitafutia ushahidi kesi hizi za udhalilishaji na ubakaji.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hayo machache naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Baraza lako hili tukufu kuchangia hoja hii au azimio hili muhimu juu ya kuhakikisha kwamba watoto na wanawake wako salama katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, suala hili kwa bahati nzuri liko katika wizara ninayoishughulikia mimi au ninayoifanyia kazi kwa kipindi hiki cha Baraza. Kwanza nampongeza Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto, nimekuja mapema sana nimemkuta yumo ndani peke yake, nathibitisha katika kutoa kauli hii katika moyo wangu kwamba anajali na anajua nini kinachotafutwa kwa usalama wa vijana wetu. Lakini upande wa pili

mimi hupenda kusema kweli, nasikitika na watendaji wa wizara hii, hadi sasa hivi namuona mnyonge Mhe. Waziri yuko peke yake wakati jukumu hili awe na wasaidizi wake kule juu wamsaidie yanayozungumzwa hapa. Kwa hivyo, ndio yale niliyosema katika taarifa yangu iliyopita kwamba bado hatujajielewa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nampongeza Mwenyekiti wa UWAWAZA, nawapongeza Wajumbe wa UWAWAZA wote, nampongeza mtoa hoja hii Mhe. Asha Abdalla Mussa baada ya semina waliyoipata na baada ya matatizo mengi waliyoyapata ya unyanyasaji waliona pana haja walete azimio katika Baraza hili. Kwa hivyo, jambo hili Mheshimiwa mimi nawapongeza kwa moyo wangu wote, mimi husema siku zote mlezi mzuri ni mwanamke maana yake anajali watoto, anajali mume, anajali wazee wote wanaomkabili kuhakikisha kwamba yeye ndiye mlezi. Mimi husema ulezi kazi ndio kama huu tuliokuwanao.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ya kusema ninayo mengi lakini nitasema kwa ufupi sana. Tuna vita vikubwa katika nchi yetu na vita hivi sawa sawa na madawa ya kulevya. Kama tunavyomuona Rais John Joseph Pombe Magufuli alivyopania na Rais wetu wa Zanzibar anapiga vita unyanyasaji huu, kila siku anaseama mpaka anataka kulia. Kwa hiyo, umefika wakati Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Madiwani, Wabunge, Masheha na wananchi wote raia wema wa nchi hii tumuunge mkono Rais wetu kupiga vita suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, kadiri tunavyokwenda siku hadi siku ukikaa siku moja au mbili utasikia mawio leo hapala fulani kabakwa mtoto, fulani kamtorosha mtoto, sijui tuna hulka gani Mwenyezi Mungu atunusuru hata sasa hivi mtu mwanamme anathubutu kuingilia wanyama jamani dunia hii tunakwenda wapi. Mimi nimuombe sana mtoa hoja hii pamoja na wizara yetu inayohusika lazima tukae tufikirie tunakokwenda. Lakini pana kitu ambacho kinasaidia ili kupatikana haki. Mimi nisiingilie Mahakama wala sina uwezo, lakini kwa kuwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nina ushauri tu. Hoja imesema na mimi katika taarifa yangu niliyoileta hapa ya wanawake na watoto ilisema vile vile, pana haja ya sheria yetu kubadilishwa au kufanyiwa marekebisho. Mahakama ya Mkoa imepewa mwisho miaka saba kumuadhibu, mtu ameshamuharibu mtoto wa watu wakati mimi nakumbuka nyuma tunakotoka wakati yupo Mwanasheria Marehemu Iddi Pandu Hassan tuliweka sheria mtu miaka 30 aadhibiwe na kuendelea. Kwa hivyo, mimi naunga mkono kwamba sheria hii ibadilike kifungu cha 7 kibadilike ili Mahakama ya Mkoa ipewe uwezo kutoka miaka saba mpaka wafike miaka 30 au 40 ua hata miaka 50 huko sio vibaya mana huyo tena mpaka afe huko huko.

Jengine kuna kifungu cha 150(1) cha makosa kifutwe kibadilishwe ili kuondoa kinga ya kupata dhamana. Mheshimiwa mhalifu yeyote ndio maana mimi nasema hivi, mbakaji yeyote sawa sawa na jasusi sijui niseme mtu gani hata hafahamiki. Naomba kwa dhati kabisa huyu ni mhalifu nambari moja kwa hivyo kama vitani kakamatwa teka usimuamini na huyu ukimpa dhamana kenda kufanya anayotaka yeye.

Mhe. Mwenyekiti, lakini jengine ili kuliondoa hili tumesema sisi katika kamati yetu wajumbe wengi wamechangia hapa mashine ya *DNA* itasaidia kupunguza hili wimbi kubwa la Mahakama yetu kupata shida. Kwa sababu chombo hiki mtu yeyote kitamuelekeza tu, fulani kafanya kosa kwa kosa fulani hana pa kupenya.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, tuna Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Masheha, kuna wananchi wema, naomba Wakuu wa Mikoa na Wilaya wao ni Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama umefika wakati sasa hivi wajipange kuhakikisha kwamba nafasi ya mhalifu yeyote haipatikani kuachiwa, akamatwe apelekwe kunakohusika ili mambo haya yaondoke.

Mhe. Mwenyekiti, ningetoa pendekezo jengine au rai au ushauri. Vijana wengi wanahama katika eneo moja kwenda kwengine, hawa watakuwa wauza unga wengine au wavuta bangi, lakini pia hawa wanaobaka watoto wamo humu, akishaharibu mtaa fulani anakwenda kwengine. Ningeomba masheha wetu wawaangalie kahamia mtu katoka Nachingwea mfano au katoka Mahonda kaja Kijito Upele kwangu huyu atizamwe je, huku Mahonda alikotokea mpaka Kijito Upele aende kwa sheha hana kasoro yoyote huyu? Pia itatuokoa. Kwa hivyo, hili liangaliwe uhamaji wa ovyo una hatari katika maeneo yetu.

Mheshimiwa kidogo namalizia. Kwa kumalizia muda hakuna ningeomba hili suala ambalo tulilitoa zaidi. Mheshimiwa haya yote yanatokea katika sehemu zetu za madrasa sio wote lakini walimu wa madrasa wengi wahalifu. Narudia tena sio wote, maana anayemharibu mtoto yeyote mhalifu. Kwa hivyo, hawa ningeomba pawe na sheria au taratibu za kufanyiwa ukaguzi wa tabia zao, kwa sababu mtu analilia mimi nataka kusomesha hapa chuo hiki siku nyengine hao ndio wanaoharibu watoto wetu na ndio wengi, wanawachukua watoto wanakwendazao kwenye dufu huko ikifika saa tisa za usiku wanawambia leo msirudi bakini hapa hapa wanafanya mambo yao. Kwa hivyo, watoto wa kiume wanaharibiwa na wanawake pia.

Mhe. mwenyekiti, mimi nawapongeza tena UWAWAZA, nampongeza Mwenyekiti wa UWAWAZA, nawapongeza UWAWAZA wote lakini

ninaloomba ili tuhakikishe linaondoka hili tumuunge mkono Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kauli moja, liwe azimio letu tunaondoka hapa Barazani Mheshimiwa tukafanye kazi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo kwa heshima kabisa naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.

Mhe. Salma Mussa Bilal: Mhe. Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kunipa fursa hii jioni hii ya leo kuwa mtu wa tatu wa kuchangia hoja hii. Kwanza kabisa na mimi nimpongeze kwa dhati kabisa mjumbe kwa kuleta hoja yake hii ya kutoa maazimio kuhusiana na uimarishaji wa mfumo mzima wa kisheria unaohusiana na uendeshaji wa kesi za udhalilishaji wa wanawake na watoto.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitakuwa sina mchango mkubwa kwa sababu hili suala tumekuwa tukilisema sana. Juzi tu kwenye ripoti za kamati tulilichangia vizuri sana lakini kwa kuwa leo mjumbe mwenzetu amelileta hili inabidi na sisi tuweze kulitilia mkazo.

Mhe. Mwenyekiti, suala la udhalilishaji ni suala ambalo limeathiri sana jamii yetu na linaendelea kutuathiri siku hadi siku. Kesi za udhalilishaji imekuwa sasa hivi kama wimbo wa taifa kila siku asubuhi tukifungua redio udhalilishaji kadhalilishwa huyu, kadhalilishwa huyu. Halafu pia hukumu zinazotolewa nazo pia zinavunja moyo kwa kweli. Udhalilishaji umekuwa ukiongezeka siku hadi siku mjini na mashamba na kila likisemewa, likizungumziwa inaonekana kama kwamba wanatiwa kasi wale wadhalilishaji. Kwa hivyo, naomba nimuunge mkono kwa dhati kabisa mtoa hoja hii kwa sababu ni suala ambalo linatuumiza sana katika jamii yetu.

Mhe. Mwenyekiti, mtoa hoja hapa ameleta jadweli linaloonesha jinsi gani makosa yaliyoripotiwa Vituo vya Polisi vya Mikoa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, inaonekana kwamba kuna kesi 2,346 zimeripotiwa lakini inasema hoja hii kwamba ni kesi 105 tu ambazo zimeripotiwa kwenye mahakama kwa Unguja na Pemba, lakini matukio yamekuwa mengi. Mhe. Mwenyekiti, hii inasikitisha mno kwamba kesi ni nyingi lakini uripoti wake uko mdogo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba tuungane wananchi sote wema kuutoa ushahidi katika kesi hizi ili ushahidi uweze kupatikana na wahalifu waweze kuchukuliwa hatua kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niunge mkono maazimio ya Mheshimiwa mtoa hoja kwamba katika maazimio yake nambari mbili (2) kuhusu upatikanaji wa hii

mashine ya *DNA*. Naomba niunge mkono kabisa kwa sababu Mwenyekiti tulipokuwa tuna tatizo hapa la meli serikali ilikubali moja kwa moja wizara zote zikatwe bajeti zao ili iweze kupatikana meli ili kupunguza kasi ya ajali za baharini. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, na hili janga la udhalilishaji nalo limekuwa kubwa mno katika nchi yetu.

Kwa hivyo, mimi naunga mkono moja kwa moja kwamba hili suala la kukatwa bajeti za wizara ili iweze kupatikana hii mashine mimi naunga mkono. Kwa sababu siku zimekuwa nyingi yaani tangu kipindi cha Baraza lililopita tulikuwa tunaomba, naomba jamani wizara au serikali ifanye jitihada za makusudi ili kuweza kuipata hii mashine ambayo itasaidia kutoa ushahidi na wale wadhalilishaji wahusika waweze kupatiwa adhabu zinazostahiki. Lakini nasikitika kwamba baadhi ya viongozi wanasema kwamba hii mashine haina umuhimu, hilo siungani nalo. Mimi naungana na Mheshimiwa mtoa hoja kwamba hii mashine ina umuhimu wake na bajeti inayokuja naomba serikali ilitilie mkazo suala hili na bajeti zikatwe ili iweze kupatikana mashine hii kama serikali haina uwezo wa kununua mashine hii.

Mhe. Mwenyekiti, pia nasema labda kumekuwa na kasoro katika hii sheria yetu ya hukumu za makosa haya. Mheshimiwa mtoa hoja hapa yeye alisema ameonesha kwamba Mahakama za Mkoa mwisho wake ni miaka saba. Kwa kweli hukumu hizi na kutokana na uzito wa masuala haya haikidhi haja hata kidogo, naomba sana serikali ilete mabadiliko ya sheria hii ili makosa haya yaweze kupatiwa hukumu stahiki. Muda huu wa miaka hii ambayo wanahukumiwa unakuwa ni mdogo sana kwa sababu kuna baadhi ya hao watuhumiwa mtu anaweza kufanya kosa moja, la pili, la tatu, la nne anafanya hili anatolewa anakwenda kufanya hili kabla ya kesi ile haijahukumiwa; anakwenda kufanya tena na tena baadae anakuja na hukumu ya miaka saba kwa kweli inasikitisha sana. Inasikitisha kama walivyokwisha kutangulia wenzangu watu hawa wanatakiwa kwanza kabla ya hukumu wahasiwe, hukumu ya kwanza ni kuhasiwa kwa sababu wakihasiwa halafu ikija na hukumu sidhani kama atarudia kufanya tena suala hili. Kwa hivyo, mimi mawazo yangu kwanza watu hawa wahasiwe ili wapunguzwe kasi baadae ndio wahukumiwe kama miaka kumi, ishirini, kama kifungo cha maisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nadhani kama nilivyosema kwamba haya masuala tumeshayazungumza sana na yanatuuma sana, yanaumiza sana. Kwa hiyo, naendelea kumshukuru mtoa hoja na mimi namuunga mkono kwa asilimia mia moja. Lakini pia nawaomba Wajumbe wenzangu na Wazanzibari wote tumuunge mkono ili kulipiga vita suala hili lisiendelee, limeumiza na tumeshachoka Mheshimiwa alietangulia alisema na tumechoka na tumechoka

kweli tukiondoka majumbani tuna wasiwasi tuna watoto wadogo wanakwenda chuoni tuna wasi wasi tuna watoto wanakwenda skuli tuna wasiwasi, tumechoka nalo hili suala kwa kweli kila likizungumzwa linazidi.

Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Salma Mussa Bilali kwa mchango wako. Lakini Waheshimiwa Wajumbe niwakumbushe dakika zetu za kuchangia ni 10 kwa kila mmoja. Kwa hiyo, tunaposimama tujue tuna dakika 10 nilitaka niwakumbushe hilo. Sasa namuomba Mhe. Suleiman Sarahan Said.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi lakini naomba uangalie saa kidogo kwa sababu zimeshakwenda vibaya hapo kidogo ukija kuchukulia dakika zimeshatembea sana. Lakini najua wewe mtaalamu na una uwezo wa kunisaidia.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa hili jambo sio geni kwetu ni kusisitiza tu na kuweza kuwaambia kweli kulikazia kamba kutokana na hali halisi ilivyo. Mhe. Mwenyekiti, unajua jambo hili lilipoanza huko mwazo lilikuwa linaenda la kibinaadamu la bahati mbaya. Lakini serikali ilipotoa kauli ya kuwa itapambana na watu hawa wale watu kama wamefunguliwa nyuki kwamba wanapambana na serikali.

Lakini serikali bado makucha yake hajatanua, sasa wale watu wanatanua makucha kuiangalia serikali itatanua vipi makucha yake. Kwa hivyo, hawa watu wanashindana na serikali kwa sababu si vizuri wala si vyema hili si jambo la wanawake na watoto hili ni jambo la jamii mimi nina mtoto wa kike, mimi nina mtoto wa kiume kama alivyokuwa mama watoto ana mtoto wa kike ana mtoto wa kiume hawezi kuzaa mwanamke peke yake. Kwa hivyo, si jambo la wanawake na watoto ni jambo letu sisi sote.

Mimi nataka nikwambie Mhe. Mwenyekiti, mwanaume ndie anaeumia zaidi akifanyiwa kitendo hichi kuliko mwanamke mtoto wake wa kike akifanyiwa mtoto wake wa kiume akifanyiwa yule mwanamke akizaa mwanamme anasema kazaa "simba" leo unamkuta mtoto anatia kidole hivi hatari baba hatizami analia mwenyewe. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, nataka uliangalie hilo kwamba hii si kauli ya mama na mtoto ni kauli yetu sote.

Jambo la pili Mhe. Mwenyekiti, hizi kesi nazo mashaka yake ni ufatiliaji. Ufatiliaji Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi watu wanaofanyiwa vitendo hivi

kwanza huwa masikini na kitendo hichi kina kuwa kama cha mwizi hakufanyii mbele za watu lazima akafanye siri. Sasa hapa kama hapajapatikana ushahidi ule ushahidi wa kitaalamu kama wa kutumia na kupima vitu ambavyo kamuachia mtu yule basi ushahidi hatupatokana maisha ambacho hapa kinajulikana chombo cha *DNA* ndio kinaweza kikaangalia yale mabaki aliomwachia kwamba huyu nani. Lakini vyengine kwa kumuangalia tu kwamba alipita wapi alikuwa saa ngapi itakuwa haifai. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, ningeshauri kitafutwe chombo ambacho kitasaidia sana ushahidi. Mhe. Mwenyekiti, hili jambo limeshakuwa kubwa sana kwetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze kwamba kwa hatua ambayo iliyopo sasa hivi ni kweli tujikazeni sana wazee sana serikali sana. Mhe. Mwenyekiti, vichocheo vimezidi sana vinasaba vya *TV*, *Video*, simu hizi za *WhatsApp* na mambo mengine uzungu uliotujaa akija mama mtoto umbusu, akija baba watoto umbusu, Mhe. Mwenyekiti, tunawapa watu wengi fikira mbaya za watoto kwa watoto. Sasa mambo haya zamani yalikuwa yanafanyika kwa kujificha siku hizi eti ndio uzungu mnabusiana kila pahali mashaka yanaongezeka.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, haya matatizo yanaongezeka na watoto kama madada na makaka kuwachukuwa ndugu zao wadogo wadogo wakifatana nao katika maeneo ya starehe nayo yanaongezeka sasa ni vitu ambavyo vinachangia sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niangalie na mashule pamoja na vyuo. Sisi wakati tunasoma vyuoni wakati madrasa wakati huo wanaume kwake wanawake kwao hatuchanganywi, kila sababu zipo mwanamke na mwanaume kuwachanganya wana sababu nyingi na hapo zamani ulikuwa ukisikia kwamba mashule pia yalikuwa wanayasema watu kwamba hii ni shule ya kike hii ya Kiume, lakini kwa ufupi yale madarasa yanajaribiwa kugaiwa sio wapumbavu hawa wameshaona kuna dalili fulani ya kumuweka mtoto wa kiume na mwanamke. Sasa hilo nilikuwa naliangalia zaidi pia tulionae.

Lakini na hii hali ya kusitiriana mara nyingi sana Mheshimiwa Mwalimu wa Chuo, shekhe nani akiteleza katika mambo haya Mhe. Mwenyekiti wazee ndio wanaokalia kifua na wakamtisha mama au baba mzazi wakamwambia ukilitoa hili basi yanakuwa haya. Sasa yule baba kwa sababu tayari kama Mwalimu Nyerere alivyosema "Ukishaonja nyama ya mtu atakula nyama ya mtu siku zote" akishaonja kitendo kile yule Mheshimiwa kila siku atafanya kile kile kwa sababu tayari akili yake imeshafyatuka na masuala yake. Kwa hivyo, Mheshimiwa hilo ambalo nasema.

Mhe. Mwenyekiti, wakati umeshafika hakuna tena cha kufichana Mheshimiwa sasa elimu lazima itolewe kila pahala kuanzia majumbani, vyuoni, mashuleni lazima tuweke bayana, tuwaambie wanafunzi wetu, tuwaambie wazee wetu, tuwaambie watoto wetu kwamba sasa dunia imechafuka ukiitwa na mtu usiende sasa hivi heshima haiko tena mimi namwambie mwanangu hata ukimuona mtu usimpokee nenda mbio, akikuta mtu ndani usiende akikupa mtu pesa usipokee ni vitisho vyote. Zamani tulikuwa tunawaambia kwamba akitokea mtu nenda ukampokee. Leo utaweza kumpokea kumpelekea kwake utatoka si unakwenda mwenyewe hiyo itakuwa hadithi ya Shekhe Paka na tasbihi ya dagaa.

Mhe. Mwenyekiti, lazima tuangalie kwamba sasa dunia imeharibika ni mambo mazito ambayo kwa kweli yameanza kutupeleka pabaya. Lakini mimi ningeshauri katika hali ambayo bado hivyo vyombo vyetu havijapatikana basi ziundwe kamati ambazo zitasiadia kule kwenye Masheha kwenye mabalozi ule wakati muafaka ambao kitendo kile kitafanyika kuliko kumuachia mzee peke yake akaenda Polisi akafanya mambo yote inaonekana kama kasutwa na jamii na mwisho anavunjika moyo. Sasa ningeshauri kwamba tungetengeneza mabaraza kule kwenye Usheha muda ule ule tukaona kuna ukweli kuna uongo na kuna jambo gani na nguvu za pale zikatoka za Baraza au za Kamati kwenda kulisimamia lile jambo, kuliko kumuachia mzee mwenyewe akahangaika nalo.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nizungumze tunazungumza Wanawake na watoto, Mheshimiwa sasa hivi wako akina mama nao wanachukuwa watoto wadogo wa kiume. Hawa watoto nao wazee wao wanalia hivyo hivyo, anamzaa watoto wake nataka amfanyie harusi amfanye mambo yote mtoto anahama kwao anahamia kwa huyo "papa" hampati mzazi wake tena. Hawa mama wapo na wanafanya na hakuna sheria hata moja inayowalinda hawa, kwa sababu hawa kwenye wanaume si kunyanyasa. Kwa hivyo, na hawa Mhe. Waziri nao watie katika hilo daraja lao kwamba nao wanaume wananyanyasika.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, unyanyasaji sasa hivi umeenea kila pahala hao hao akina mama "mapapa" wanawachukuwa watoto wadogo wanawaowa wao wenyewe wananza kuoenesha vitendo vibaya. Sasa Mhe. Mwenyekiti nashauri sana tuangalie hii jamii imeshaharibika *total* hakuna mwanamke hakuna mwanamme hakuna mdogo hakuna mkubwa Mheshimiwa sasa hii imekuwa vita vya samaki tunalana wenyewe kwa wenyewe ni *total* sasa hivi tuangalie kwa hali na mali hali halisi.

Lakini ningesema tena usajili ya vyuo vya Quran vifanyiwe usajili sio kila mtu achukuwe bakora yake na kofia na kilemba akae mkwaju wake anasomesha na

hii afisi iwe inakaaguliwa ana wanafunzi wangapi anawapa elimu vipi na darasa lake linaonekana vipi, tumeiacha hii tumeiweka pembeni mtu akiona hana kazi anaona na mimi nitafute nafasi anachukuwa mkwaju na kilemba nakaa pale anaanza kusema watoto leteni sasa hapo anaekuja anabaka tu akibaka kachukuwa.

Waheshimiwa hii lazima nayo ifanyiwe kazi tukiteleza tunaanza na hapo kwa sababu hadhari ni bora kuliko kutibu hii kesi zamani zilikuwa za wandawazimu tulikuwa tunajua kwamba yule ni mwanadawazimu. Lakini sasa hakuna mwandawazimu tena mpaka wenye akili zao hii dhahama imeshaanguka hili neneo hakuna tena.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumze kwamba uzalilishaji unauma zaidi ni udhalilishaji wa watoto wachanga maana yake unamfikiriaje mtoto wa miaka miwili mitatu unamfanya jambo mpaka unamua. Hivyo, ukimuua unamtizameje yule mtoto hebu tulitizame hili jambo. Sasa Mheshimiwa hivi vitu vinauma ubakaji upo kila aina au lakini ule wa watoto wachanga umezidi sana. Sasa ningeshari sana mtoto mchanga atakuja kutoa ushahidi gani hakuna ushahidi.

Sasa ningeishauri serikali kuhakikisha kwamba tunatafuta kifaa cha haraka sana ili kuliondoa hili suala. Mheshimiwa pamoja na kwamba bado nina maongezi lakini nimeshakuona unavyonitizama basi mimi sina haja ya kugombana na wewe niunge mkono hoja nashukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mtumwa Penya Yussuf: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti na mimi kwa kunipa nafasi hii.
Kwanza na mimi nimpongeze kwa dhati Mjumbe mwenzetu ambaye aliewasilisha hoja hii. Kwa kweli hii hoja ni hoja nzito na ni hoja ngumu sana. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli suala la udhalilishaji kwa watoto na kina mama kila siku hili suala linaongezeka siku hadi siku na vitendo hivi ingawaje Mjumbe mwenzangu kina mama nao pia wanahusika kufanya udhalilishaji, lakini hususan hasa wanaofanya matendo haya ni kina baba. Inashangaza na ina uma sana sijui baba yule anakuwa kuwa na anakuwa na hamu ya kiasi gani hata akamchukuwe mtoto mdogo wa miaka miwili au mitatu.

Kwa kweli ni suala zito tena zito sana maana shari ujifikirie lile suala linataka sharti uwe na ile shughuli yenyewe na hamu yenyewe na kumuona yule mtu wenyewe, mtoto mdogo kweli anafikiri vipi wewe mtu mzima baba mkubwa kwenda kumkatamata mtoto wa kike au wa kiume ukamfanyia tendo lile kweli raha iko wapi, jamani hili tatizo yule anakuwa sio binaadamu ni mnyama.

Binaadamu wa kweli hawezi kufanya tendo kama lile kwa sababu unajigeuza wewe ni binaadamu unakuwa kama jogoo, jogoo hata kifaranga anakifatia mbio sasa ndio binaadamu. Sasa ndio binadamu kweli yule ndio binaadamu ule ni unyama tunaoufanya kwa kweli hili suala ni zito.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye Vituo vya Polisi na baadhi ya Polisi haya maswala nasema wanayachangia. Kwa sababu mimi nina ushahidi tosha mtoto wa miaka 7 kadhalilishwa mtoto wa kike kafanyiwa vibaya sana na ushahidi wote ulikuwepo. Lakini askari wanawatisha mzazi yule kwa kuwa myonge hawezi kuzungumza kenda kubalishiwa kesi baada yake kesi imemzunguka anaamua kule kituoni asiende mtaa nyumba yake mwenyewe mtu inamshida kukaa kwa kweli hizi za uzalilishaji. Kwa kweli tunakwenda wapi na tutafika wapi.

Niombe sana vituo vya Polisi Vituo vya Polisi kesi hii inapokuja tujitahidi sana tubadilikeni kwa sababu leo limemfika mtoto wa mwenzio kesho litamfika mtoto wako utakubali. Lazima tulishughulikie hili suala na askari yoyote ataekwenda kinyume atakaefanya taratibu nyengine basi ashughulikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, lakini haya mambo ya kesi hizi kwenda Mahakamani kwa kweli kesi zinachukuwa muda mrefu mzazi utakumkuta kila siku anaambiwa nenda Mahakamani masikini ya Mungu mzazi yule yake asubuhi inamshinda kila siku atakuwa na nauli ya kupanda gari kwenda na kurudi, kesi inachukua muda mrefu mzazi mwenyewe mpaka aende kondeni arudi ashughulikie watoto leo unamwambie nenda rudi nenda rudi hili suala jamani anapokamatwa mtu anofanya kesi hizi hukumu yake itolewe haraka isichukuwe muda mrefu.

Kwa nini mwizi wa kuku mwizi wa ndizi siku mbili anahukumiwa inakuwa ile kesi ina urahisi gani ya kuwa mtu aliyemdhalilisha mtoto mdogo kesi ichukuwe miaka mpaka unasahau, enhe! mpaka unasahau kesi hiyo inakwenda mzazi nenda rudi wanakatika tamaa wazazi wanashindwa kufatilia inabidi wabakie nyumbani kesi ile inamalizika kiyenyeji hivyo hivyo.

Lakini pia nije kwa familia maswala haya yanapotekeza mitaani utakuta pengine kafanya mtoto wa mjomba mtoto wa shangazi wazazi wenzangu niwaombeni sana tuwache kumalizana wenyewe nyumbani. Kwa sababu yule mtoto tayari yeye keshadhalilika kesha umia kiakili lakini pia kiashaumia kimwili unatamkuta mtoto pengine kukaa kitako hakai kutoka nje wenzie wakitoka waanza kumwambia maneno yanayokuwa siyo. Wewe mama mzazi au baba mzazi mnakaa nyumbani familia mnaihukumu kesi ile ndani kienyeji enyeji usiseme tuyamaliza mnayamaliza nyumbani wazazi wenzangu

hatuwatendei haki watoto wetu, tubadilike tuhakikishe kesi zinakwenda kunakohusika.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, pale Hospitali ya Mnazi Mmoja kwenye kituo pale cha mkono kwa mkono unafika pale saa nne asubuhi vitoto unavikuta vimewekwa pale wanataka kushughulikiwa na pale kinachotakiwa ushahidi upatikane. Saa nne daktari anaeshughukika pale pengine hajafika unakuta mpaka mtu anaona bora niende nikamsafishe mwanangu mtu inafika saa tano anakwenda kumsafisha mtoto wake ushahidi unaambiwa haupatikani na kile kitengo nacho kifunguliwe mapema, ili wanapokwenda pale wakutikane wapo *time* zote hawa watoto waweze kushughulikiwa .

Mhe. Mwenyekiti, jengine nishauri wazazi wenzangu jamani turudisheni malezi ya kizamani. Zamani watoto walikuwa hawalelewi na mtu mmoja jamii yote mtaa mzima tulikuwa tukilea mtoto mmoja. Lakini leo kila mmoja na mwanawe hivi kweli kila mmoja na mwanawe unaweza kumlea mtoto wako, mtoto wako hata akikutikana na jambo unashindwa kuja kuambiwa mzazi mwenyewe unakuwa mkali unapanda juu hatima yake yanatufika haya yanayotufika.

Tubadilikeni watoto ni wetu sote mtoto halelewi na mmoja tuwalee kwa pamoja ili tupunguze haya na ukimbaini yoyote ana tendo hili basi tushirikiane tupeane taarifa hakuna la kufichana. Kwa sababu hili hali inaendelea na watoto wetu kwa kweli tutamaliziwa tutakuwa hata wale watoto wa kiume tena mwisho habari hakuna watoto wetu watakosa hata wachumba wa kuwaoa hamna kwa kazi hii tunayokwenda nayo. Kwa kweli tubadilikeni jamani.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, mimi kuna suala linaniuma sana wiki moja tu iliyopita mtoto wa kiume mgonjwa wa akili kakamatwa kabakwa na si chini ya watu watatu. Nalisema hili mmoja naambiwa kakamatwa na nasemaje waliobakia watafutwe wakamatwe na hili suala lishughulikiwe na nisema nitakwendanao sambamba tuhakikishe hili linafika mwisho. Kwa sababu haya matendo yamezoeleka na yanaendelea kila baada ya wiki utaambiwa mtoto kabakwa na mbakaji hapatikani baada ya wiki kabakwa mbakaji hapatikani. Sasa huyu nasema aliepatikana ashughulikiwe.

Lakini mwisho Mhe. Mwenyekiti, natoa maoni yangu hawa wataokamatwa mtu keshakamatwa na kesi hii mwezangu kasema wahasiwe hebu kila kituo cha Polisi na kuwekwe spana ya umeme, kile kinachofanya aringie, kile anachoringia anachomharibia mtoto wa mwenziwe ukifika mbaneni kwa ile spana ya umme ndio. Kwa sababu haiwezekani kuwa leo mtu abaka anapekwa

ndani siku mbili ya tatu akirudi anafanya lile kwa sababu zipi afanye lile ina maana kuna raha huko ndani anakopelekwa, hawapati shida ndio sababu yenyewe. Lakini ingelikuwa kule ndani akifika anapata shida *wallah* yangekwisha yangemalizika lakini hafanywi chochote tengenezeni spana ya umeme kila kituo cha polisi anafika abanwe kwa spana yake ya umeme siku ya pili akitoka yule akimuhadithia mwenziwe hafanyi tena wala yeye harudi tena lile tendo kwa sababu na yeye ile raha ataiona ya kumfanyia mtoto wa mwenziwe lile tendo.

Kwa hayo machache Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hii hoja jamani tushirikiane wanaume muwaambie wanaume wenzenu waachane na vitendo hivi hatari tutauwana sote. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli siku ya leo ni siku muhimu sana kwa Wazanzibari pamoja na sisi ambao tuliopewa sauti ya kutoa sauti zetu mbele ya Mwenyezi Mungu.

Niseme hivyo, kwa kuanza kusema *Inna Lillah Wainna Ilaihy Rajiun.* Mhe. Mwenyekiti, huu ni msiba mkubwa ambao tokea asubuhi leo tulikuwa tunashuhudia kutokana na vitu ambavyo sio utamaduni wetu sisi Wazanzibari, na kwa kweli inasikitisha sana kwamba maporomoko ya maadili yameanza kutupotea.

Mhe. Mwenyekiti, kubwa ni ombi tu kwa hivi vyombo vinavyohusika, kwamba mitihani hii itamfika kila mtu, naona jambo kama hili sio la kuliweka na kulifanyia mzaha, fimbo ya Mwenyezi Mungu haina sauti.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi niombe suala hili la udhalilishaji lina upana mkubwa sana na ina maana nyingi sana, na inagusa kila sehemu ambayo sisi binadamu hatupendi yafanyike. Mhe. Mwenyekiti, toeka asubuhi makatazo kama haya kama sisi Waislamu yamo kwenye Misahafu na kwa waliokuwa sio Waislamu yamo hata kwenye Biblia, hakuna sehemu inayosema vitu kama hivi. Sote siku zote tunapiga kelele kwa kuamriwa kitu kimeharamishwa.

Lakini mimi nichukuwe nafasi hii Mhe. Mwenyekiti, kuwaomba viongozi Masheikh, kwa sababu maporomoko ya maadili tumeshuhudia baadhi ya walimu wa vyuoni kufanya vitu hivi ambavyo kwa kweli inasikitisha. Mimi ushauri wangu kwa serikali ni kwamba umefika wakati iwe tunajiuliza taasisi hizi zote zimepewa majukumu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tujiulize haya majukumu wakati mwengine sioni kama kuna ugumu wa kuyatekelezwa, ni imani yangu kwamba katika mazingira tuliyokuwanayo na udogo ambao

tunajuana, mimi naamini kama tutakuwa watendaji wakweli serikalini na taasisi zote, basi naamini kwamba mambo haya hayana mjadala na nina imani kwamba yanaweza kuondoka kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. Lakini penye nia pana njia, lazima kuwepo na nia.

Kwa hivyo, mimi niombe kwamba serikali yetu vitu hivi ambavyo tuliokuwa tumekubaliana na tukapitisha azimio toka asubuhi mpaka hivi sasa basi sote tuunge mkono, tuwe mabalozi wa kwanza kwa Mwenyezi Mungu, na kujisafisha nyoyo zetu kwa kuweka maslahi ya watoto wetu na vijana wetu na maslahi mbele.

Mhe. Mwenyekiti, katika mazingira kama haya tumeshuhudia mengi, ukisema udhalilishaji kuna mengi, kuna dada zetu wanapigwa, kuna ndugu zetu ambao Mwenyezi Mungu amewaletea mtihani walemavu hufungiwa ndani ya majumba yao miaka mitano au sita pasipo na hatia ni mtihani wa Mwenyezi Mungu. Kwa hivyo, ni mambo mengi sana. Kwa hivyo, mimi niombe kwamba tukubali sote hili jambo ni la kulisimamia, na mimi naamini kwamba uwezo huo tunao na sote tunajua.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo tulililokuwa nalo sisi baadhi ya watendaji, sio kila anayepepesuka ni mlevi, panapokuwa na kikao. Mimi nitataja vitu vitatu ambavyo ushahidi huo mimi ninao. Walikamatwa vijana kwa madawa ya kulevya *red handed* uwanja wa ndege pale, wakati wa awamu ya Dk. Salmin Amour, vyombo vikafanyakazi wakapelekwa. Aliyekuwa Mwanasheria Mkuu kwa wakati ule akawaruhusu wale kuwakimbiza na wakakimbia Canada. Na walipewa *information* kabla siku moja ili waondoke na wakaondoka na lile jambo likaja pale likaonekana kama ni sembe, unga wa ngano. Sasa ninachotaka kusema kwamba ni lazima tuwe wa kweli, hizi taasisi zimo ndani ya serikali, sasa kama taasisi zimo ndani ya serikali sisi tunapitisha azimio, kwa hivyo taasisi hizi ni lazima ziwe zinafanyakazi. Hilo la kwanza.

La pili, Mhe. Mwenyekiti, wakati mwekezaji kutoka Venter Kiwengwa, ndugu zetu au wenzetu Wataliana. Mhe. Makamu wa Pili wa Rais Mzee wetu, baba yangu mzee Balozi Seif Ali Iddi aliitisha kikao ofisini kwake jioni saa 8:00 kwamba bwana hawa wameshakimbiza karibu bilioni 6 za wakulima. Kwa hivyo, ukatoka ushauri wazuiliwe, kwa sababu kuna madai ya serikali na kuna madai ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, katika kikao kile mjumbe mmoja aliwakimbiza jioni wale watega uchumi wa Kiwengwa pale, waliondoka jioni yake, katoka mtu hasa katoa *information*. Sasa ni lazima tuwe waangalifu kwamba hawa tunawaita

tuwe tunawaelewa na kama kuna taarifa iwe *very sensitive*. Kwa hivyo, walikimbizwa, na mimi nikampigia simu balozi usiku, nikamwambia Balozi mmefanya kikao jioni wale jamaa wameshakimbizwa, na aliyewakimbiza ni aliyeteuliwa na Rais na alikuwa Kamishna ni mmoja katika Makamishna.

Mhe. Mwenyekiti, isitoshe aliyekuwa Waziri Kiongozi Mhe. Shamsi Vuai Nahodha pale Baraza la Wawakilishi, aliitisha kikao saa saba kulikuwa na sehemu ambayo watu walikuwa na mpango wa suala zima la madawa ya kulevya, kikafanyika kikao wakawekwa watendaji kazi ile ikafanywe, watu walipotoka tu ikatoka *information* kwamba bwana wee tayari ngoma imesharipuka, wakakimbizwa. Nikamwambia Nahodha mimi Waziri Kiongozi mstaafu bwana wee mmeitisha kikao dakika kumi ngoma iko nje hiyo. Sasa Mhe. Mwenyekiti, tutazunguka sote lakini katika vitu kama hivi ni lazima tuwe wakweli na tutizame tatizo liko wapi.

Halafu jambo la pili ni kuhusu zana za kufanyia kazi. Katika vitu kama hivi vya udhalilishaji na haya madawa ya kulevya yanaendana na matokeo kama haya. Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, juzi mimi nilikuwa Mchangani mtoto wa miaka miwili *Wallah Laadhim* inasikitisha, kwa sababu wakati mwengine watoto wetu ni wa kimaskini, uwezo wao ni mdogo, hawana nauli hata ya kufika sehemu ya kupata sheria sasa inakuwa ni ngumu sana, na mambo mengi yanawatokea watu waliokuwa hawana uwezo. Mimi naona kuna haja hizi *system* nzima kukawa na bajeti, uwezo na nyenzo za kufanyia kazi. Kwa sababu sasa hivi ukitokea ubadhirifu wowote mfano shamba ile ikiripotiwa tu, basi inakuwa vigumu. Tunao vijana na watendaji wazuri, lakini utakuta gari haina mafuta, bajeti haipo. Sasa yule mtu anapata kukimbizwa, wewe huku unatafuta gari. Kwa hivyo, ni lazima tujipange na katika kujipanga basi vitu kama hivi vinahitajika, yaani nyenzo.

Kwa hivyo, mimi niombe hili jambo zima linagusa hasa katika mambo yetu ya Muungano, Wizara ya Mambo ya Ndani, ambapo ningewaomba wahusika wakakaa na kuona bajeti kwa sababu hii bajeti ipo kubwa na tunapata misaada, lakini lazima tuji- *organize*. Leo tutapiga kelele lakini ukanda huu mzima wa baharini kule hatuna boti za kisasa, je tunajiandaa vipi katika kukilinda kisiwa chetu. Sasa vitu vyote hivi vinataka nyenzo za kufanyia kazi. Kukitokea ubadhirifu kunahitajika nyenzo za kufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika miaka mitatu iliyopita, ipo *Hansard* hapa tulizungumza hili suala la *DNA*, ambapo wakati ule ilikuwa inazungumzwa milioni 800. Mhe. Mwenyekiti, twendeni kwenye *Hansard*, tukasema jamani tunaijua serikali yetu hohe hahe tunakwenda na tunachokipata, mimi

ninamshukuru sana Mhe. Rais Dk. Shein na uongozi mzima wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, wamefanya kila jitihada. Lakini wakati mwengine ni lazima tukae tusaidiane maarifa. Sasa *DNA* wakati ule, leo nafikiri *it about nine hundred million* (900,000,000) *that time if I don't mistake* ilikuwa *four hundred million* (400,000,000) milioni. Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa mtu wa kwanza kujitolea katika kuona kwamba watoto wetu Wazanzibari namna gani ya kutafuta msaada huu. Yaani hakuna mtu aliyekuwa na habari, aliyekuja akazungumza mpaka leo, na leo pengine bei mara mbili. Sasa Mhe. Mwenyekiti, hii nchi...

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, naomba malizia muda wako umekwisha.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Mhe. Mwenyetiki, hii nchi ni yetu sisi sote, tujiulize ni lazima kwanza tuwe na uchungu wa kusaidia serikali yetu. Kwa hivyo, mimi niiombe serikali ikae kitako itizame na tutaunga mkono sote hakuna mmoja atakae kataa katika suala ambalo ni kinyume na maadili yetu. Lakini tumefika na mimi nakushukuru na naishukuru serikali tujipange, ninasema tukijipanga mambo haya tunajuana sote. Leo mheshimiwa ana Recruzer tatu, ana milioni mia tatu anaendesha gari, hana leseni, hana TRA, wala hana chochote. We have to be serious Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Raza.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja zote hizo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mohammedraza kwa mchango wako. Sasa namuita Mhe. Zulfa Mmaka, akifuatiwa na Mhe. Mussa Foum Mussa na Mhe. Tatu na yeye ajitayarishe.

Mhe. Zulfa Mmaka Omar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii na mimi leo kuweza kuchangia. Mhe. Mwenyekiti, mambo mengi yamesemwa lakini na mimi nataka niseme kidogo ili tuonekane kwamba wanawake tumekubali mara hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza Rais wetu. Nampongeza sana Mhe. Rais kwa kuona kwamba ipo haja maalum ya kutufungulia Mahakama yetu ya Watoto, Mhe. Rais tunakupongeza kwa hili na tunakuambia kwamba usife moyo sisi vijana tuko pamoja na wewe kwa suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, katika hizi mahakama mimi nimuombe tena Mhe. Rais ile Mahakama ya Watoto tayari amefungua. Lakini ukiwaangalie hawa ambao wanafanya makosa ya udhalilishaji wengi sana sio watoto, utamkuta mtu wa miaka 40 na 37 ndio wanaofanya matendo haya. Kwa hivyo, mimi ningemuomba Mhe. Rais kwa jicho la imani, kwa kuwapenda watoto wake, kwa kuwapenda wananchi wake basi afunguwe mahakama maalum ambayo itasimamia kesi hizi za udhalilishaji. Mhe. Mwenyekiti, ikiwa haitowezekana hiyo mahakama maalum, basi kesi hizi zipangiwe siku yake maalum ya kusikilizwa.

Mhe. Mwenyekiti, tukiangalia kwa upande wa *DPP*. Mhe. Mwenyekiti, upande wa DPP tunahisi kwamba wana makesi mengi sana ambayo wanayalimbikiza, basi ichukuliwe juhudi kwamba kesi hizi ziundiwe chombo maalum ambacho kitakuwa kinazifuatilia na kutoa hukumu zake.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika hukumu ambazo zimewekwa katika kesi hizi. Mhe. Mwenyekiti, hukumu hizi ni ndogo sana, mtu anamdhalilisha mtoto halafu kwenda na kurudi tunasikia kwenye maredio mtu kafungwa miaka 7. Miaka saba kufungwa ni kitu gani, kwa kweli ni kidogo sana tena sana. Kwa hivyo, tunaomba kwamba sheria hii iletwe katika Baraza hili ili tuibadilishe, hii sheria imeshapitwa na wakati, na hiki kifungo au adhabu hii ndogo ndio inayowasababishia wale ambao wanafanya vitendo vile kuona kwamba jambo hili haliko *serious* wacha tufanye, tutakwenda tu miaka 7 tukirudi tunakuja kufanyakazi zetu. Kwa hivyo, tunaomba kwamba sheria hii iletwe hapa Barazani, sisi tuko tayari kuibadilisha, hata kama tutaambiwa siku tatu tusitoke humu tuwe tunabadilisha sheria hiyo, basi sisi tuko tayari.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naiomba na hii wizara nayo iwe iko tayari kusimamia mambo ya udhalilishaji, kwa sababu bila ya wao basi watu wengine hawawezi kufanya kazi zao vizuri, lakini kama wao watakuwa wanatoka asubuhi wafanyakazi wale au wanasheria wa wizara hii wanakwenda katika mahakama zetu, na kuuliza vipi leo katika kesi zilizopangwa kesi za udhalilishaji ni ngapi. Kwa kweli hata kama zitakuwa hamna basi watakuwa wana hofu, watakuwa wanajua kwamba sisi tunakwenda kuchukua ripoti, lakini kila siku tukienda kama ripoti hazipo, basi watakuwa na wao mahakamani wataona aibu. Ni lazima itakuwa kesi hizi kwa siku wanazipanga mbili au tatu, zikishakupangwa wanauliza vipi adhabu gani zimetolewa, zikishakutolewa wizara hii na wao wanatoa zile taarifa katika vyombo vya habari. Lakini tukisema kwamba wizara hii inasubiri tu ofisini iletewe hizi habari, kwa kweli tutaendelea kulala.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende katika Kituo cha Mkono kwa Mkono. Mhe. Mwenyekiti, watu wetu ambao wamepangiwa katika baadhi ya vituo vya mkono kwa mkono hawako tayari. Kwa sababu anaweza akaenda mtoto pale anamtaka daktari, kwa kweli masaa manne au matano anatafutwa daktari mmoja anakosekana, na daktari yule atakapopatikana basi atakuja kufanya mambo yale rapu rapu amalize arudi nyumbani kwake. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, wale madaktari niseme kwamba hawako tayari wengine kusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, halafu madaktari wale wale wameshafanya vipimo vile, lakini tunawakuta kwamba madaktari wanaogopa kwenda mahakamani kutoa ushahidi. Hivi Mhe. Mwenyekiti, kesi bila ushahidi itakwenda vipi, haiwezi kwenda, daktari ndio mtu pekee wa kutoa ushahidi wa mwisho. Kwa hivyo, ukiwauliza wao wanakuambia kwamba maswali tunayokwenda kuulizwa mahakamani ni mazito, hamna swali zito ambalo utaulizwa. Wewe mtu mzima daktari umeaminiwa na umesoma kitu gani kitakushinda kujibu juu ya masuala ya afya, hakuna. Kwa hivyo, tuwaombe hawa madaktari wasiogope kwenda mahakamani kutoa ushahidi kwao wao hata Mwenyezi Mungu atakwenda kuwalipa kwa kupigania suala hili la udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza hapo niende kwenye hizi dhamana. Mhe. Mwenyekiti, tumesema kwamba kwa sasa hivi kwa vile hizi sheria bado hatujazibadilisha, hizi dhamana hebu zifungwe tuangalie itakuwaje. Mtu akienda na kesi hii hata kama ndio anafuatiliwa ushahidi wake basi dhamana yake aambiwe kwamba imefungwa.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mbaba mmoja mtu wa Kaskazini Pemba ana kesi nne za ubakaji, mbaba huyo mbona hana kesi nyengine za kufuga kuku, bado uambiwe kwamba ushahidi bado haujatimia, kesi nne iwe anazuliwa yeye tu Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli sio kweli. Tuwe tayari dhamana zao zifungwe, zikishafungwa watajua aah! hivi sasa serikali tayari imeshazitilia mkazo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, niende upande wa udhalilishaji wa watoto wa kiume. Kwa kweli sasa hivi hili ni tatizo. Katika maskuli yetu kwa mfano Pemba mtoto akiambiwa kapasi upande wa Wete unaogopa kumpeleka, Mhe. Mwenyekiti, huko kuna wimbi kubwa la watoto wakiume ambao tayari wameshaharibiwa. Kwa hivyo, niwaombe sana wanachi, watoto wale wanafanyiwa vitendo vile bila ya kujijua, tuwaache watoto wale wasome. Wale wote ambao wanafanya vitendo vile basi tuwaambie kwamba warudi kwa Mwenyezi Mungu, wale watoto nao wana haki ya kuishi, kama wao ambavyo wanaishi na sasa hivi wamepata nguvu za kufanya vitendo hivi vya udhalilishaji ambavyo sisi leo hapa tumesimama kwa ajili ya kuvipigia kelele.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nahisi mambo mengi yameshazungumzwa. Lakini katika hizi adhabu, unajua mambo mengine Mhe. Mwenyekiti, ni dhambi kuyafanya, lakini laiti kama ingekuwa sio dhambi basi ningesema kwamba kuwepo hasa watu maalum pale polisi, akiletwa mtu kafanya kosa la udhalilishaji mtoto mmoja, basi watokee vijana 7 na yeye wamshughulikie, mimi naamini kwamba hii itakuwa ni adhabu kubwa. Kwa sababu anajua kwamba nikienda na kesi moja, basi kuna vijana 7 mimi watanishughulikia, halafu akitoka pale wacha apewe dhamana vijana washafanya kazi zao vijana 7, naamini na yeye atashindwa kutoka nje. Kwa sababu na wale watoto wanaofanyanyia vitendo hivi na wao tunawauwa.

Mhe. Mwenyekiti, utamkuta mtoto wa miaka minne kafanyiwa, kweli mtoto huyu akija akiwa mtu mzima atazaa, hawezi kwa sababu wengine wanawavunja uzazi. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, kama wameamua kuwaharibu watoto, mimi naiomba sana serikali adhabu hii kwa nini isiwekwe, ingawa ni dhambi na tunaogopa dhambi, lakini Mwenyezi Mungu alijua mwanzo ndio akatuwekea hizi adhabu nyengine zisiwekwe, lakini adhabu hii Mhe. Mwenyekiti, ingekuwa inafaa sana. Kama haifai adhabu hii ni dhambi, kuuwa ni vibaya sana, basi naiomba sana serikali mtu akienda kwamba kamdhalilisha mtoto, basi kile ambacho kamfanyia kile kiungo chake ambacho katumia kufanya kitu hiki, Mhe. Mwenyekiti, kikatwe. Kikishakukatwa basi naamini mimi litakuwa lile suala la kujifanya kwamba yeye anaringa na kuwaharibu watoto wetu huko nje litakuwa limemalizika. Kwa hivyo, mimi naomba hii adhabu ya kukatwa hichi kitu ambacho wanaringia itumike, kikatwa hakifai. Nikimaliza hapo Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Zulfa Mmaka. Sasa nimwite Mhe. Mussa, akifuatiwa na Mhe. Tatu Makame Ussi na Mhe. Viwe Khamis ajitayarishe.

Mhe. Mussa Foum Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakupongeza na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii, na mimi vile vile nimpongeze mtoa hoja Mhe. Asha Abdalla Mussa Muwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa, hoja imekuja kwa wakati muafaka na sote ipo haja ya kuchangia hoja hii au kuiunga mkono.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachangia kidogo kwa sababu mambo mengi wenzangu wameshayachangia lakini nataka niseme kwamba udhalilishaji umekuwa mkubwa sana hapa nchini kwetu, lakini mimi upande mmoja nasema kwamba kuna na sababu zinazochangia, sababu kubwa inayochangia katika

mambo haya ni kuvunjika kwa maadili maadili yetu tumeyaacha ambayo haya yalikuwa yanachangia katika kuyapunguza mambo kama haya. Ninavyofahamu mimi zamani watoto wa kike walikuwa hawana urafiki na watoto wa kiume, na watoto wa kike hasa watoto wakiwa wari walikuwa hawajipambi. Lakini leo utamkuta mtoto mwari kajipamba kuliko huyo mama yake sasa kuna mambo yanachangia. Zamani watoto wa kike wanaambiwa msicheze na watoto wa kiume wana mafunza lakini pale ilikuwa wazee wana ghadhuwatulfikra wameiweka ile ghadhuwatulfikra pale inalinda jamii, kumbe wanaambiwa msicheze na watoto wa kiume wana mafunzo kumbe ni zile mimba za watoto.

Sasa leo hii tumeona hakuna lolote watoto wanapata mimba bado wadogo na yale maadili yetu tumeyavunja na sisi baadae tunachangia, kwa mfano leo tutakaa hapa tunalaumu upande mmoja polisi kwa mfano mtoto wangu mimi kapewa mimba na mtoto fulani, lakini yule mtoto inawezekana tuko katika kijiji kimoja au jamii moja ndugu. Leo mimi mzee nitajikaza pale nakwenda polisi kushtaki lakini siku ya pili watanijia wazee wa kijiji ili tuende polisi tukafanye suluhu, leo matokeo yenyewe tunakwenda polisi suluhu itakayotokea kule tunayoifanya kwamba wale watoto waozeshane ili lile suala limalizike tunafanya nini tunayachangia haya mambo, kwa sababu baada ya kutoa adhabu leo tunampeleka yule kijana ende akafaidi zaidi.

Pale ingelitolewa adhabu yule mtu wa nyuma aliyekuweko nyuma na yeye angelijua nikifanya kitendo hiki nachezea miaka mitano au sita pale angelikuwa na heshima nzuri, lakini leo tunajikaza tunakwenda kufanya ile siku ya pili kijiji kile kile yanatokea mengine sasa haya mambo tunayachangia. Sasa mimi nasema hebu turudini jamii ijirekebishe juu ya mambo haya leo tutalaumu polisi, tutalaumu Mkurugenzi wa Mashitaka, tutalaumu madaktari lakini sasa sisi kama jamii mbona hatujilaumu kwanza tujisahihisheni na sisi leo Mhe. Waziri anayehusiana na masuala ya wanawake bila ya shaka na yeye anapata wazee kwamba zile kesi alizopelekewa yaani wafanye mazunguzo zisipelekwe Mahakamani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba kwanza hii hoja lazima tuiunge mkono kwa sababu hali si nzuri sisi waislam lakini mambo yaliopo nchini petu haya tunayofanya ya udhalilishaji makubwa sijui tutakwenda kusema nini kwa Mungu, mimi siungi mkono kwamba kuwe na mambo mtu akifika pale aumizwe hii siungi mkono. Isipokuwa kuwe na sheria lakini hizo sheria tusimamie ili sheria ifuate mkondo wake kiukweli tusiwe wanafiki. Hili suala la ukaribu undugu ujamaa hili halitotufikisha pahali pazuri siku zote tutalaumiana hapa tutasema ibadilishwe sheria, leo wewe umetakiwa uende ukakae ushahidi

tu basi utasema sitaki kwenda kukaa ushahidi kwamba hutaki fulani apate adhabu mahakamani sasa haya mambo yatafika wapi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naiunga mkono hii hoja na naomba Wajumbe watakaoichangia vile vile waiunge mkono, lakini vile vile nasema kwamba na sisi jamii tubadilike pindipo hatutobadilika tutatunga sheria hapa kila siku tutabadilisha hii na hii lakini ikiwa hatutobadilika basi mambo hayatokuwa mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo na mimi naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa nafasi ya kuweza kuichangia hoja hii iliyowasilishwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa, na mimi nasimama hapa kuichangia hoja hii kwa sababu ni mwanamke imenigusa, ni mzazi nimezaa nina watoto nina kila hali ya kuichangia hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianze kwa masikitiko sana kwa jinsi watoto wetu wanavyodhalilishwa na watoto wetu hawa wanadhalilishwa na akina baba, mimi huwa najiuliza hawa akina baba wanaonaje hawa watoto wadogo kuwadhalilisha kuwavunjia utu wao walionao, kwa sababu kijana mdogo unamfanyia vitendo vya udhalilishaji inakuwaje jambo hili jamani hebu tujiulize kulikoni.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hoja yangu kwanza itakuja kwenye makosa yaliyoripotiwa katika vituo vya Polisi katika mikoa ya Zanzibar. Mimi kwanza nina wasiwasi na hizi kesi zilizoletwa hapa. Kwa sababu ukiamka asubuhi utasikia wenzetu wa habari na nawashukuru watu wa vyombo vya habari na zaidi watu wa mawio jinsi wanavyofuatilia kesi hizi za udhalilishaji. Lakini la kushangaza kesi hizi zilizoletwa hapa naona ni kidogo. Lakini hata hivyo inakuwaje kama hawa watu walioachiwa huru hapa Mahakamani najiuliza walikuwa hakuna ushahidi au wameachiwa huru kwa sababu gani, lakini je hawa waliowaachia huru hawaoni kuwaachia huru ni kuendeleza hili suala zima la udhalilishaji.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye kesi zinaopelekwa Polisi, kwanza niwaase Mapolisi wasiendelee kusuluhisha kesi wakawaita wenye kesi wakawaambia wasuluhishe kwa sababu wote ni ndugu hii ndio inayosababisha kuendelea kwa vitendo vya udhalilishaji. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, kesi hizi zinaposuluhishwa Polisi hata wale wafanyakazi wetu wa Wizara ya Ustawi wa

Jamii na wanawake ambao wanasimamia kesi hizi basi zinawavunja moyo kutokana na kuwa kesi haziendi inavyopaswa. Kunakuwa na mlundikano wa kesi wao wanafanya jitihada ya kusimamia kesi hizi kwa hivyo jitihada zao wafanyakazi hawa inaonekana hazithaminiwi, kwa hivyo nawaasa tena polisi kuacha kufanya vitendo hivyo.

Lakini vile vile ukienda upande wa Mahakama Mhe. Mwenyekiti, hiyo kesi ikipelekwa Mahakamani sie tunailaumu jamii kwamba hawatoi ushahidi, hivyo Mhe. Mwenyekiti mimi nitakwenda Mahakamani siku ya kwanza, nitakwenda siku ya pili nitaambiwa kesi haina ushahidi, mimi mtu ninayetoka kijijini kweli kesi iliyokuwa haimalizi kuna nini mbona kesi ya mwizi wa ndizi na muhogo inamalizika.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, mimi niende kwetu sisi wazazi na jamii kwa jumla, wenzangu wamezungumzia suala la maadili, wenzangu wamezungumzia suala la malezi jamani ni kweli na mimi naunga mkono wenzangu ili turudi katika malezi ya zamani. Kwa sababu hili nalo linachangia kwa kiasi fulani, wewe ukimuona mtoto wa mwenzio hata kafanya nini basi wewe unakuwa humuulizi unasema namuogopa mzazi wake jamani sivyo tulivyolelewa sisi turudini katika malezi ya zamani ili kuondosha suala hili la udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, sasa niwatake Masheha watu wetu wakishafanya hichi kitendo cha udhalilishaji wanakimbia katika shehia wanazokaa wanakimbilia shehia nyengine. Sasa kutokana na hilo tuwatake masheha kufanya kazi zao za usheha ndani ya nyumba kumi kwa sababu wajue wageni walioingia. Mimi nina ushahidi hapa ninapokaa kuna mtoto alifanyiwa vitendo vya udhalilishaji usiku dakika hiyo hiyo aliyefanya kitendo kile hakuonekana na mpaka leo hakukamatwa na yule mtoto yupo yuko ndani maskini anajisikia unyonge yeye na wazazi wake. Sasa nina hakika mfanyaji kitendo kile kwa usiku ule hakuweza kusafiri lakini hadi leo hakukamatwa na mtoto yuko ndani yeye na wazazi wake wanadhalilika.

Mhe. Mwenyekiti, nasema tena Masheha jamii, Polisi, vyombo vya Mahakama tushirikiane katika kulitokomeza suala hili, lakini vile vile niiombe Serikali kununua kile kipimo cha *DNA* kwa sababu kukosekana kwa kipimo hichi imekuwa ndio sababu ya udhalilishaji kuongezeka, kwa sababu kesi zinapopelekwa utasikia hatuna ushahdi mpaka mtu apimwe kwa kipimo cha *DNA*. Sasa naiomba Serikali inunue kipimo hichi kwa sababu hizi kesi ziliopo zipungue tumechoka wanawake kudhalilishwa, tumechoka kudhalilishiwa watoto wetu, watoto wetu hawana raha, hawana furaha lakini na sisi wazazi pia tumechoka. Siku hizi ukitaka kutoka asubuhi una wasiwasi kumuacha mtoto

ndani ya nyumba, una wasiwasi kumtuma mtoto dukani alimradi kila unapokwenda huna raha huna furaha.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo naomba tufanye mashirikiano ya kuondosha udhalilishaji huu. Baada ya maelezo haya Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja asilimia mia moja. (Makofi)

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunpa nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii ya Mheshimiwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi, hoja ya udhalilishaji wa kijinsia hapa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo la udhalilishaji Zanzibar limekuwa likiendelea siku hadi siku hivi karibuni kulikuwa kuna kipindi cha maswali hapa Barazani tulimsikia Mhe. Waziri alilijibu suala lile akasema kama kuna watu ambao kuwa ni mashahidi wanakwenda Mahakamani na watu wale wanakuwa wanapatiwa nauli shilingi mia nane. Mimi hili silikubali kama lipo kwa sababu kama lipo watu hawa wanaobakiwa watoto wao wanaodhalilishiwa watoto wao pamoja na mashahidi wasingelishindwa na nauli ya kwenda Mahakamani na kuweza kukaa ushahidi kwa wale watoto ambao kuwa wamebakwa au wamedhalilishwa.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe Serikali katika kipindi chake hichi cha bajeti inayokuja wahakikishe fungu la nauli kwa mashahidi limeingizwa ili kuondosha kero ambazo zinawakabili wananchi wetu wakati wanapokwenda kwenye kesi hizi za udhalilishaji, tukiangalia wananchi wetu wengi ni masikini.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye vyombo vya sheria Polisi, Mahakama, DPP na Vituo vya Mkono kwa mkono hawa Mhe. Mwenyekiti, kama watataka kushirikiana kwa pamoja basi tatizo hili la udhalilishaji hapa Zanzibar litaondoka. Mhe. Mwenyekiti, kuna rushwa nyingi ambazo zinatumika kwenye vyombo hivi vinavyohusika na Mahakama Polisi, pamoja na hivi Vituo vya Mkono kwa Mkono. Hivi kweli Daktari unataka ushahidi gani mtoto ameshabakwa kama hajaingiliwa hata siku moja basi unamjua unataka ushahidi gani wee kama huyu mtoto kabakwa, Madaktari wanakubali kuchukua rushwa ili kesi zile zisiendelee lakini mimi nasema kama kuna dokta ambae kuwa alishiriki asiweze kutoa mashirikiano basi Mwenyezi Mungu amlipe na yeye mtoto wake.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi Zanzibar kuna vyuo vingi vya madrasa hivi vyuo hivi wengine huwa wanaviweka kwa malengo yao makusudi tuna watoto wetu sasa hivi wanabakwa kwa kupitia kwenye vyuo vya madrasa, walimu wale wa

madrasa bado wapo na wanaendelea kuwepo na vyuo vile vinaendelea kuwepo. Serikali au Ofisi ya Mufti wakigundua kuna chuo ambacho kuwa kina mwalimu amebaka basi chuo kile au madrasa ile ifungwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niende kwenye jamii wazee, wazee waache kukaa kusuluhishana wenyewe kwa wenyewe mitaani kutokana na kusuluhishana wenyewe mitaani ndipo ongezeko hili kubwa la udhalilishaji linaongezeka hapa Zanzibar. Tuache muhali muhali siku zote haujengi unabomoa. Mhe. Mwenyekiti, juzi tu tuliambiwa kamaa kuna meli ambazo zitanunuliwa na Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar, niiombe Serikali katika meli hizo mbili ambazo watazinunua Serikali basi meli moja waiwache wanunue kipimo cha *DNA* muda umefika. Kasoro hizi zote zilizopo ni kuwa hapana kipimo cha *DNA* ndio kisingizio chao walichokiweka hapa Zanzibar na watoto wetu na vijana wetu kila siku wanazidi kudhalilika. Natilia mkazo Serikali kwa bajeti hii wanunue kipimo cha *DNA* ili tuweze kuondosha tatizo hili la udhalilishaji, sisi wanawake wa Zanzibar tumechoka na udhalilishaji wa kijinsia, tumechoka baada ya muda fulani tutakuwa sisi hapa Zanzibar hatuna watoto wa kiume, hatuna watoto wanawake, watoto wote watakuwa wameharibiwa. Serikali ituone kama tushachoka wanawake wa Zanzibar. Vyombo vya Mahakama vichukue maamuzi. Tunaiomba serikali watuletee.

Mhe. Mwenyekiti, sasa hivi kuna baadhi ya watu wanataka utajiri sasa wanapokwenda wanaamini sana imani za kishirikina wanakwenda kwa waganga, wakishakwenda huko wanaambiwa kama unataka utajiri tembea na mtoto wako. Wewe unakwenda unambaka mtoto wako eti kwa sababu unataka utajiri hivi utajiri unapatikana kwa kumbaka mtoto wako? Waache waganga kutoa imani hizi za kishirikina na kuweza kuwalaghai watu kwa sababu ya kuwa watawapa utajiri hakuna mtu mwenye uwezo wa kumpa mtu utajiri mwenye uwezo ni Mwenyezi Mungu peke yake.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika azimio langu mimi mwenyewe nililoliona sheria zote zinazohusiana na udhalilishaji ziletwe mbele ya Baraza hili tukufu kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho, ili kuziba mianya ambayo hufanya wadhalilishaji kuwa huru. Sheria zote ziletwe ndani ya Baraza la Wawakilishi, sheria hizi ambazo zinawafanya wadhalilishaji hawa kuwa huru. Muda umefika na tena umefika wa kuwa wadhalilishaji hao wasipewe dhamana. Mtu anambaka mtoto anafungwa miaka saba, miaka saba nasikia kwa sheria asubuhi ni siku moja na jioni ni siku moja unakaa mle ndani miaka mitatu na nusu.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie muda wako umekwisha.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Mhe. Mwenyekiti ahsante namalizia. Kwa hayo machache niliyochangia naunga mkono hoja hii ya Mhe. Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa asilimia mia moja na serikali wanatusikia wayafanyie kazi, la si hivyo tutaandamana Zanzibar nzima wanawake.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Viwe Abdalla sasa namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi akifuatiwa na Mhe. Mgeni Hassan Juma, Mwenyekiti wa UWAWAZA na Naibu Spika na kama muda utaruhusu kuna Waheshimiwa wameomba dakika tano tano naweza nikawapa, lakini wale ambao nitakuwa sijawataja nawaomba sana waandike michango yao kwa maandishi., Kwa sababu wachangiaji ni wengi na hoja naona imemgusa kila mtu humu ndani mpaka mawaziri wote wanataka kuchangia. Kwa hivyo, nawaomba sana waandike kwa maandishi kutokana na muda. Hivyo namuomba Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, pili naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu lakini naomba vile vile nimpongeze sana Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa hoja yake binafsi aliyoileta muhimu sana kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nataka niseme tu kwamba kama kuna kiongozi ambaye ameguswa sana na jambo hili ni Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein. Na katika kuguswa kwake tulichukua siku nzima kulijadili jambo hili kwa undani kabisa na hatimaye akaunda Kamati ya Mawaziri ikiongozwa na Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na baadhi ya mawaziri wamo na watendaji ili kulisimamia kwa kina jambo hili. Kwa hivyo, nataka niseme tu kwamba kwa upande wa serikali imechukua juhudi hizo na haya mapendekezo ambayo yametolewa hapa kamati itayasikia na itayachukua na kwenda kuyafanyia kazi ili kuongeza nguvu ya yale ambayo yameamuliwa kwenye serikali.

La pili Mhe. Mwenyekiti, nataka niseme jambo hili ni jambo zito na wala tusilifanyie mas-hara, ni jambo zito kwa mambo matatu. Kwanza kama waumini tumeacha kumuogopa Mwenyezi Mungu, huo ndio msingi wa kwanza kabisa wa tatizo hili kwamba watu tumefika pahala Mwenyezi Mungu hatumchi tena hatumuogopi. Vitendo hivi kama vilifanyika huko zamani ilikuwa kwa siri sana leo linaonekana ni jambo la kawaida. Lakini unakuta wengine ni viongozi kabisa ndio wanashabikia na ndio wanaoongoza katika jambo hili. Viongozi wa dini wako katika jambo hili na viongozi wengine wa taasisi wako katika jambo hili. Kwa hivyo, suala la kumuogopa Mwenyezi

Mungu hili lazima tukubali kwamba ni tatizo kubwa la msingi tunahitaji kama viongozi, kama wazazi, kama wazee kujielekeza kwamba tumeacha mkono wa kumuogopa Mwenyezi Mungu hili litatugharimu.

La pili kubwa wenzetu ambao zamani walikuwa na wao wakiona jambo hili ni kosa leo ni halali kwao na wanakukosesha hata msaada kama hukubaliani na wao kubadilisha sera yako kwamba kulifanya jambo ni la kawaida, la kwamba mwanamke na mwanamme wanaweza kuingiliana na mwanamke na mwanamme wanaweza kuingiliana ni jambo la kawaida kwao na wanalihalalisha mpaka mahakamani. Kwa hivyo, ni jambo ambalo sio dogo, yale maeneo ambayo yanajikinga na jambo hili yanavamiwa nayo kwa nguvu na wakaona pahala peke yake pa kuvamia ni wapi ni kwa watoto wadogo hawajui chochote masikini za Mungu na bahati mbaya kuna tatizo la umasikini katika maeneo yetu wanatumia nafasi ya umasikini tuliyonayo. Kwa hivyo, athari yake ni kubwa sana.

Sasa tunayo mapendekezo ya kuunda kamati ya sheria, lakini sheria bila ya sisi wenyewe kusimamia kidete haitofanya kazi. *DNA Machine* iweko hapa itakuwa ipo haitofanya kazi ile mashine kama haijapelekewa taarifa, kama haijapelekewa na mtu aweze kutoa ushahidi. Lakini kuna mambo ya kawaida tunaweza kuyafanya wenyewe hatuyafanyi na Rais amelisema hili la kufanya kazi kimazowea. Wazee wa zamani walikuwa hawana muhali, leo muhali ndio unaotawala kwa kila jambo. Watu wanavunja sheria lakini kwa sababu ni ndugu yako, ni jamaa yako unafanya muhali, huu muhali ndio uliotu-*cost* mpaka hapa tulipo. Tumeacha mambo ya Mwenyezi Mungu tunaweka muhali mbele ya safari. Kwa hivyo imefika pahala humuogopi Mwenyezi Mungu, muhali mbele na mataifa haya yanavyotuvamia tatizo limekuwa kubwa mno. Tunahitaji kukaa kitako kama viongozi na tuanze sisi wenyewe katika nyumba zetu. Rahisi kumuoneshea mtu kidole jitizame wewe mwenyewe kwanza.

Wakati mmoja niko Makka pale nilikuwa nawaoneshea watu fulani kidole nasema wakati wa Mtume *(S.A.W)* alikuwa akikaa na wafuasi wake mbona leo wakubwa wa Wafalme wanakaa mbali. Yule Sheikh akanambia yule kule anasema wewe tizama vidole vitatu vinakuuliza mke wako anasali, wanao wanasali na kadhalika. Jibu la kwako kwanza kabla hujamnyooshea kidole mwenzako. Tujibu na sisi ya kwetu, tujibu katika majumba yetu, tujibu katika majimbo yetu, tujibu katika shehia zetu halafu twende katika ngazi ya kitaifa hapo ndio tutaweza kupambana na hivi vita. Kama hatujaenda kwenye *grass roots* ku-*deal* nayo hatutofika pahala, tutazungumza kwa jumla, tutapiga kelele, lakini ukitoka katika nyumba yako kuna tatizo, ukitoka katika shehia yako kuna tatizo, ukitoka katika jimbo lako kuna tatizo, ukitoka katika wilaya yako kuna

tatizo, ukitoka katika mkoa wako kuna tatizo na taifa litakuwa katika hatari vile vile.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, *plea* yangu ya kwanza ni kwamba tulione jambo lenyewe ni kubwa sio dogo wala sio suala la kupiga kelele tukamaliza, wala si suala la sheria peke yake. Sheria zipo lakini hazifanyi kazi kama sisi hatutaki sheria hizo zifanye kazi zana zitakuwepo hazitofanya kazi kama zana hizo hatutaki sisi zifanye kazi, *DNA* itakuwepo na kadhalika. Pale Bara ipo *DNA* haijapunguza uzito wa jambo lenyewe, sisemi isiwepo, lakini nasema tusichukulie tu kwamba imeshapatikana *DNA* ndio tumetatua tatizo aa, tatizo bado lipo tunahitaji kuli-*address* tatizo lenyewe. Sheria itapitishwa hapa anaekosa aadhibiwe hivi na hivi, lakini kama tunarudisha muhali hatutompeleka kutoa ushahidi maana hatoadhibiwa mpaka afikishwe Mahakamani ushahidi utolewe.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kama hutaki kwenda kutoa ushahidi mahakamani inakuwa tatizo liko pale pale pamoja na kwamba sheria ni kali na pengine ikiwa kali zaidi utasema aah! mwenzangu atakwenda kufungwa maisha hapati dhamana ndio siendi kabisa. Kwa hivyo, lazima tukubali kwamba hili ni tatizo letu tulichukue, tupambane nalo ni la kwetu sote. Lakini nasema kwa upande wa serikali tumechukua juhudi hizo namshukuru sana Rais wetu amejitahidi sana kuliona jambo hili ni tatizo kubwa, ameli-*address* katika Baraza hili kila *forum* anayopata anajitahidi kuli-*address* amekaa na sisi na amezungumza na sisi anasema *major* hizi tuchukue, lakini bila ya ushirikiano wa wananchi, bila ya ushirikiano na taasisi hatuwezi kufika pahala. Na nawaomba viongozi wote wa kisiasa, wa kidini lazima hili tuchukue ni *challenge* sisi ni *mas-uul* mbele ya Mwenyezi Mungu, tukisahau hilo tutapata matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana naomba kuunga mkono hii hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Zaina Abdalla Salum: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipatia fursa hii adhimu jioni hii ya leo kuweza kuchangia na mimi hii hoja ya mjumbe ambayo ni ya maadhimio kuhusiana na udhalilishaji wa kijinsia.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze mjumbe huyu ambaye aliyekuwa ameipanga vizuri hoja yake na akaiwasilisha vizuri, kwani tumeona kwamba katuwakilisha sisi wana UWAWAZA katika Baraza hili la Tisa la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kusema kwamba suala la udhalilishaji kwa kweli hivi sasa katika hii nchi yetu ya Zanzibar imekuwa tendo la tishio linalotishia katika jamii yetu. Tukiangalia katika jamii yetu imekumbwa na janga hili kubwa sana, kwa sababu tatizo hili linafanyika maskulini, majumbani mwetu, linafanyika na sehemu nyengine mbali mbali kama kwenye vyuo vya madrasa. Kwa hivyo suala hili kwa kweli linahitajika kutoa elimu kubwa kwa jamii japo kuwa na haya mambo wanafanya ma-baba zetu au waume zetu ndani ya majumba yetu. Ukiangalia kama hivi kuna taarifa fupi tu hivi juzi ilitokea kuwa mtu mwenye ulemavu wa viungo alidhalilishwa na baba yake na pia akawa anapita akimkashifu nadhani katika vyombo vya habari viliripotiwa. Kwa hivyo, naomba kwamba wizara husika ishirikiane vizuri na hivi vyombo vya sheria ili kuhakikisha kwamba mambo haya yanawekwa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tukubaliane tu kuwa sheria zetu kweli zina mapungufu hasa katika suala la ushahidi. Lakini nataka kusema kwamba japokuwa zina mapungufu hayo yaliyokuwa ndani ya sheria zetu, pia vyombo vya ulinzi vinachangia suala hili hasa Vituo vya Polisi kwa sababu tumeona katika jadweli hili ni kesi nyingi ambazo zilizoripotiwa katika Vituo vya Polisi na tukiangalia Mkono kwa Mkono vilivyokwenda kupatiwa ushahidi ni kidogo. Sasa kesi hizi nyengine zinaishia majumbani, zinaishia mitaani hili suala kwa kweli ndio maana linazidi kuchangia na linazidi kuendelea sana katika jamii yetu. Namuomba Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora azidi kulifanyia kazi suala hili tuone kwamba jamii inakaa katika hali iliyokuwa nzuri.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wangu naishauri Wizara husika ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto ishirikiane kikamilifu na ihakikishe kwamba sheria hizi zote zinapitishwa ndani ya Baraza la Wawakilishi hili tukufu ili kuleta maslahi kwa jamii na Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa muda umekwisha kwa mchango huu naunga mkono kwa asilimia mia moja hoja hii ya Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti…

MUONGOZO

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nilileta maombi…

Mhe. Mwenyekiti: Kwa kifungu gani cha kanuni.

Mhe. Simai Mohammed Said: Kanuni ya 40, 73 na kanuni ya 165 na sheria ya fursa za mwakilishi. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai sijakuruhusu useme, umetaja Kanuni ya 40 inasemaje ili ujenge hoja yako? Mhe. Simai naomba ukae. Tuendelee Mheshimiwa.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mheshimiwa Kanuni ya 40 inasema…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Simai naomba ukae.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante.

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nichukue fursa hii adhimu kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi hii. Lakini nitangulize kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye ametupa uwezo wa kusimama hapa mbele ya Baraza letu tukufu kwa kuweza kuchangia hoja hii muhimu ambayo imeletwa na Mhe. Asha Abdalla Mussa, Mwakilishi wa Jimbo la Kiwengwa.

Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii adhimu kwanza ya kipekee kabisa kumpongeza sana Mhe. Asha kwa umahiri na umakini wake ambao ameutumia katika kusimamia suala zima la udhalilishaji wa wanawake na watoto. Suala hili Mheshimiwa ni suala ambalo kila mtu hapa au watu wengi hapa Zanzibar tunalizungumza, suala la udhalilishaji na namna linavyokua kila siku limekuwa ni kero kubwa katika kero ambazo tumeshafikia wakati tunaona kwamba kero hili haiwezi kutatulika. Namshukuru sana na nampongeza Mhe. Asha kwa sababu ameileta hapa ndani ya Baraza tutafute mbinu na njia ambazo zitasaidia katika kuhakikisha kero hii ambayo tunahisi haiwezi kuondoka tukae pamoja kwa mashirikiano yetu tuweze kusaidiana kuondosha kero hii ya udhalilishaji.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Asha ametupa takwimu ambazo zinaonesha kuwa kesi nyingi zinaripotiwa lakini kesi nyingi zinapeperuka katika hewa hazijuulikani zinakwenda wapi. Ni kesi chache sana ambazo zinapata hukumu. Tumeambiwa kwamba katika jadweli hii ambayo ameitoa Mhe. Asha ni kwamba idadi ya kesi zilizoripotiwa ni 2,346 lakini zilizochukuliwa na upepelezi ni 1,944, zilizokwenda katika Mahakama ni kesi 142 na kesi zilizopata hukumu (hatia) ni kesi 13. Lakini ukitizama ile *trend* ya zile kesi unaona kwamba kuna kama kesi 1,500 Mhe. Mwenyekiti ziko hewani hazijuulikani ziko wapi?

Mhe. Mwenyekiti, hili ni tatizo, hili ni tatizo na kama hatujatafuta njia yakulitatua tatizo hili tutaendelea kuwa walalamikaji. Mheshimiwa haipendezi nchi nzima iwe watu wote walalamikaji. Mheshimiwa nachukua fursa hii adhimu kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Nasema hivyo kwa sababu ameshafanya jitihada kubwa sana, ameongeza mshahara mzuri kwa Mahakimu wetu, lakini vile vile nakumbuka vizuri sana Mheshimiwa kulikuwa na siku maalum ambayo ni kuadhimisha siku ya udhalilishaji wa wanawake na watoto Mhe. Rais alitangaza rasmi kwa kipindi cha miaka mitatu kama sikosei na alitoa kazi zifanywe na ndio maana zikaundwa kamati Mheshimiwa ndani ya kamati hizi kuna watu mahiri watu ambao watu wanafanya kazi na kweli suala hili linawauma. Lakini panatakiwa ushirikiano mkubwa bila ushirikiano suala hili bado litaendelea kuwepo. *(Makofi)*

Tusiachie Waheshimiwa serikali peke yake, tusiachie Mahkama peke yake, tusiachie polisi peke yake, tusiachie Wizara ya Wanawake peke yake suala hili sote tuhakikishe tunavaa njuga kuhakikisha suala hili linaondoka. Mimi niwapongeze sana waheshimiwa wote waliochangia hapa watachangia kwa kuzungumza lakini vile vile watachangia kwa maandishi kwa sababu suala hili tunafahamu kwamba kila mmoja lazima aonyeshe *concern* yake.

Mimi naanza kwa kusema hivi Mheshimiwa baada ya kutoa pongezi zangu, kwanza Mhe. Mwenyekiti nashauri hawa vitangi nasema vitangi kwa sababu ndio jina la mwanzo ambalo tulitumia baada ya kuwanza kujitokeza wadhalilishaji ambao wakapewa hukumu hawa vitangi lazima ifike wakati wajulikane. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna mataifa huko *Europe* tatizo lilikuwa hili hili la watoto kudhalilishwa na wanawake na wananchi wakakataa wakasema kwamba hatutaki tena kufata sheria kwa sababu hawa watu wanaumiza sana watoto wetu, wakaanzisha mbinu za kuwatambulisha watu hawa wadhalilishaji na ilikuwa mbinu yenyewe wakaita *name the shame men* watajeni wanaotutia aibu, udhalilishaji ni aibu ya taifa sio tu wale wanaofanya kile kitendo. Mtu yeyote akipata taarifa ya udhalilishaji anahisi kwamba Serikali yetu na sisi wenyewe wananchi tuko regerege kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti ningeiomba sana Serikali na ningemuomba Mheshimiwa akija hapa kufanya majumuisho suala la kuanza kuwataja, kuwataja hadharani wadhalilishaji wote ni suala muhimu sana. *(Makofi)*

Lakini jengine Mheshimiwa ningeiomba sana Serikali katika mahkama zetu kuzipa uwezo mahkama zetu hasa kwenye masuala ya *technology* wakaweza

kuweka taarifa vizuri za wadhalilishaji wote ili kwamba mtu anafanya kitendo kile mwanzo lakini mara ya pili anafanya tena hajulikani kama yule alifanya Makunduchi anakuja tena mjini kwa sababu hatuna mfumo wa kuweka *data* vizuri katika mahkama zetu. Kwa hivyo, wale wanaendelea wakitoka hapa wanakwenda hapa wakitoka hapa wanakwenda hapa wenzangu waliotangulia wamesema vizuri kabisa tuna masheha lakini masheha hawana hata takwimu za vyuo ambazo madrasa zimo katika shehia zao tuwaombe masheha hiyo kazi ni yao.

Lakini wawe na taarifa za walimu na taarifa zenyewe kwamba taarifa wapi amefanya kazi kabla ili wajuwe ni wepi ambao wanaweza kufanya vitendo vile vya udhalilishaji na kuwaondoa haraka katika jamii au kuwaripoti katika tuwaripoti polisi. Mheshimiwa hivyo mambo kama hayo wenzetu wanayafanya.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo amelizungumza mheshimiwa aliyetoa hoja suala la *DNA* ningeiomba sana Serikali yangu. Mheshimiwa naliomba hili kwa sababu kipindi kilichopita katika Baraza la Nane nilileta hoja mimi mwenyewe binafsi kuhusiana na udhalilishaji wa wanawake na watoto na nikaiomba Serikali kwamba hii *machine* ya *DNA* ni muhimu lakini imekuwa bado haijuakubalika Serikalini, haijakubalika kwa sababu ambazo inasema kwamba haiwezi kutoa ushahidi na ushahidi wake utakuwa ni ule kama mgonjwa labda kama mtu ambaye amepata mimba basi tena ataafute nasaba za yule ambaye amemtia mimba nalo hilo si dogo.

Waheshimiwa wenzetu wako Tanzania bara iko *machine* hii na tunapopata matatizo inabidi tuyapeleke kule na kule inachukua kama miezi sita miezi saba ukweli tunakuwa hatuupati wa kesi zile. Mheshimiwa naiomba sana Serikali ione hili jambo la kuwa na *DNA machine* ni muhimu. Nimeuliza wataalamu wanaohusiana na masuala ya kesi hizi za jinai na wakanambia huwezi kupata ushahidi wa kutosha hasa wa kisayansi kama huna *machine* hii sasa leo tukisema kwamba hii mashine haina umuhimu naomba hilo jambo tuwache kulisema. Hii *machine* ni muhimu na tunaona nchi za wenzetu wanazitumia katika kukamata mambo mbali mbali yanayohusiana na udhalilishaji, ujambazi mambo chungu nzima.

Mheshimiwa naiomba tena Serikali na ninaomba Serikali ikubali katika maazimio haya azimio hili la kuwa na *machine* ya DNA wenzangu wamesema na mimi nakazia hapo.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kulisema jengine ambalo ni muhimu sana wajumbe wengi wamezungumzia

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba umalizie

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Ahsante Mhe. Mwenyekiti namalizia kuwa na mahkama maalum kwa ajili ya udhalilishaji. Mhe. Mwenyekiti na mimi hilo nalikubali lakini vile vile kupanga kuwe na siku maalum au majaji maalum ambao watakuwa wanashughukia kesi za udhalilishaji ningeomba sana ningeomba sana nashauri Serikali katika hayo tufikirie ili tuweze kuhakikisha kesi hizo zinakenda haraka.

Lakini mwisho Mheshimiwa saa nyengine mahkama zetu hazina usiri Mhe. Mwenyekiti tuhakikishe kwamba kwa sababu ya kesi hizi zilivyo tuhakikishe kwamba Mahkama zetu ziwe na usiri ili wale wanaokwenda kutoa ushahidi wajisikie wako huru kutoa ushahidi.

Baada ya kusema hayo machache Mhe. Mwenyekiti nakushukuru sana na mengi ya kusema lakini mengi yamesemwa na wengine niwapongeze sana wanawake wote wa Baraza hili niwapongeze kwa sababu ile azma ya kuwa na umoja wa wawakilishi wanawake inatimia. Ahsante sana nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti utaratibu, Mhe. Mwenyekit utaratibu Mhe. Mwenyekiti nasimama kwa...

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mwenyekiti sasa naomba waheshimiwa wajumbe Mhe. Simai kuhusu utaratibu nimekuona na uendelee kukaa Mhe. Simai *(Makofi)*

Waheshimiwa Wajumbe kwanza niwapongeze sana kwa kujua Kanuni lakini pia hii kanuni inatuhusu sote nikiwepo mimi hapa kwenye kiti pamoja na wajumbe wote mlokuwemo humu hii ni Kanuni yetu. Lakini niseme kwamba hii kanuni kwa vile ni yetu sote na mimi pia nina maamuzi katika hii Kkanuni unilisema Mmheshimiwa kuhusu utaratibu nimekuelewa lakini mpaka nikuruhusu useme kama sijakupa ruhusa, kama sijakupa ruhusa basi Mhe. Simai usisimame ukasema. Kwa hivyo naomba pia hii Kanuni utizame katika kifungu cha 61. *(Makofi)*

Hii kanuni 61 mtizame ule utulivu pia unatakiwa ndani ya Baraza kifungu 61 katika kanuni hii mnayoitumia nyinyi na mimi naitumia kwa hivyo kinataka pia

utulivu ndani ya Baraza kwa hivyo tutulie pale unapohisi hujatendewa haki nikikuruhusu utasema na kifungu ukitaje hii mara ya pili karibu ya tatu unasimama kwa hivyo kwa leo sikuruhusu tena. *(Makofi)*

Waheshimiwa naomba tuendelee sasa namuomba kwa sababu hii hoja nahisi au ndivyo ilivyo imegusa na Wizara mbili. Wizara ya Katiba na Sheria na pia Wizara ya Wanawake kwa hiyo tukianza hivi huyu kasimama kuhusu utaratibu sifikiri hata hawa mawaziri wanaweza wakasema chochote kuhusiana na hii hoja kwa hiyo, tuwape nafasi hawa wajumbe waliomba dakika tano tano ili nipate niwape nafasi na hawa mawaziri wa wizara hizi mbili waseme chochote halafu tumpishe mtoa hoja nadhani tumeelewana Waheshimiwa Wawakilishi.*(Makofi)*

Waheshimiwa tunaendelea namuomba Mhe. Amina Iddi Mabrouk akifuatiwa na Dk. Sira kwa dakika tano na Mhe. Shadya pia dakika tano ikiwezekana hata tatu pia naomba muende haraka haraka ili tuwapishe wale mawaziri.

Mhe. Amina Iddi Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti..

Utaratibu

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Alwardy: Mhe. Mwenyekiti, utaratibu sisi tumeleta mwanzo.

Mhe: Mwenyekiti: Mhe. Simai naomba utoke nje. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Nitoke nje vipi?

Mhe. Mwenyekiti: Utoke nje. Tunaendela Mhe. Amina dakika tano ikiwezekana hata tatu.

Mhe. Amina Iddi Mbarouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi kwa kunijalia na kuniwezesha kusimama hapa mbele ya baraza lako tukufu nikiwa mzima na afya njema.

Lakini pia nichukue nafasi hii adhimu na ya dhati kabisa kukupongeza wewe Mwenyekiti kwa umahiri wako, kwa ujasiri wako, kwa kujiamini na kwa kutumia kanuni vizuri hongera sana hii inamaanisha kwamba akina mama tunaweza bila kuwezeshwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niungane na wenzangu wote ambao wamechangia hoja hii lakini pongezi za dhati kabisa nitoe kwa Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa ujasiri wake na umahiri wake wa kuleta hoja hii muhimu sana kwa Taifa letu na kwa watoto wetu.

Mhe. Mwenyekiti, janga hili ni la kitaaifa naamini kwamba janga hili linatugusa sote katika Baraza la hili lako tukufu lakini pia linawagusa walio nje. Mhe. Mwenyekiti, watoto wetu ni uhai wa Taifa letu lakini watoto wetu ni vijana wa Taifa la leo na la baadaye, lakini pia watoto wetu ni hatma ya baadaye ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, janga hili la udhalilishaji watoto kwa kweli linakidhiri katika nchi yetu na nina amini kwzamba Mhe. Mwenyekiti suala hili sasa limekuwa hatarishi kwa Taifa letu kwa hiyo, mimi niseme kwamba kabla mchango wangu naiunga mkono hoja hii ya Mhe. Asha Abdalla Mussa Mwakilishi wa Kiwengwa kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nianzie katika jamii yetu mimi Mhe. Mwenyekiti naamini kwamba pamoja na Serikali lakini na wananchi kwa ujumla na jamii kwa ujumla lazima tushirikiane katika kuhakikisha kwamba tunalipiga vita swala hili.

Mhe. Mwenyekiti, muhali niseme kwamba ndio umetufikisha hapa jamii yetu ina muhali sana Mhe. Mwenyekiti labda kabla sijaendelea nitoe mfano mmoja niseme kwamba Mhe. Mwenyekiti baadhi ya wananchi wanachangia asimilia kubwa kuongezeka kwa jambo hili, na sisi wazazi muhali wetu unatupeleka kuendelea katika suala hili. Kuna kesi moja Mhe. Mwenyekiti ilitokea hivi karibuni ya udhalilishaji wa mtoto.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mtoto fulani alifanyiwa jambo hili na kati ya mmoja wa mwanafamilia lakini badala yake kikaitishwa kikao tu cha familia na yule mtu aliyemfanyia kitendo kile mtoto akakiri kwamba kafanya na akatoa fidia ya kumpa kidani tu mzazi, ili kesi asiipekele mbele.

Mhe. Mwenyekiti, kidani kitamfanya nini mtoto wakati mtu yule mwenye akili timamu ameshampotezea uzima mtoto yule jibaba mtu mzima mwenye akili timamu ameshamdhalilisha mtoto ameshamharibu mtoto lakini mtoto yule amemfanya kuwa hata akili kuchanganyikiwa kwa suala lile. Inasikitisha sana inauma sana kwa kweli kama tutasimama sote wanawake humu ndani kulizungumzia suala hili inauma sana, inasikitisha sana.

Mhe. Mwenyekiti, naona unataka kunipiga muda lakini niendelee katika *point* ambayo nilikusudia.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika swala letu la sheria yetu

Mhe: Mwenyekiti: Mheshimiwa umeniomba uendelee lakini nakuomba umalizie

Mhe. Amina Iddi Mbarouk: Namalizia Mhe. Mwenyekiti, Mheshimiwa sheria yetu tuliyokuwa nayo sasa hivi nambari 7 ya 2004 haikidhi haja haijaweka kiwango cha chini cha adhabu kwa mtu ambaye anafanya kosa lile na inapelekea hakimu anapohukumu kosa like anapojisikia tu ikiwa miezi mitatu, ikiwa miaka mitatu, ikiwa miaka minne.

Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti, mtoto ushamfanyia kadhia ile unamfunga mtu pengine ana miaka arubaini miaka mitatu au saba mtu yule anapotoka anakuwa mzima anaendelea kufanya mambo yale kwa kweli inauma. Niombe Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilete sheria tuifanyie marekebisho *at least* iwe kiwango cha chini miaka thelathini na cha juu mtu afungwe maisha, lakini sio miaka saba Mhe. Mwenyekiti hii ni sawasawa na mtu kwenda kutembea tu kupumzika kule gerezani akitoka anaendelea kufanya mambo yake kama kawaida wakati mtoto yule ameshamuharibia maisha yake.

Mhe. Mwenyekiti, inauma sisi Waheshimiwa wanawake inatuuma pengine kuliko wanaume sisi ndio wazazi niombe Mhe. Mwenyekiti Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ilituletee haraka sana tuifanyie marekebisho sheria. *(Makofi)*

Mhe: Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Amina

Utaratibu

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy: kuhusu utaratibu kifungu cha 63 kanuni ya 63(45) maelezo binafsi ya mjumbe kanuni ya 45 Mhe. Mwenyekiti kwa kweli hujatundea haki kumtoa Mhe. Simai siyo hajafanya makosa la pili Mhe. Naibu Spika bosi wako kavunja wakati na kanuni hujaitumia kavuka wakati ulouweka na *stilll* umemuonea huruma, Mhe. Simai ana haki ya kuinuka kwa mujibu wa kanuni yetu kuinuka na *still* umemtoa kwa kupigiwa zogo na wajumbe.

Mhe: Mwenyekiti: Mhe. Nadir nimepokea kuhusu utaratibu wako na kama nilivyosema saa zile hii kanuni inatugusa sote, siwezi kumuona mtu anafanya fujo anakwenda huku na huku akaliondoshea Baraza ile umakini wake akaendelea kukaa kule. Kama ni hoja hiyo waheshimiwa nilitoa taarifa hapa wachangiaji wengi na muda wetu ni mdogo kwa hiyo naomba waheshimiwa wote wachangie kwa maandishi wale ambao sijawapa nafasi hapa wapeleke kule kwa mtoa hoja. Hicho ndicho nilokisimamia na ndicho nilokisema na Mhe. Simai nilikuwa najua ataka kusema nini kanambia anataka dakika tano nimpe kama ulitaka ujue kama sababu hiyo..

Sasa dakika tano za kuchangia peleka kwa maandishi si Kanuni inasema hivyo hukupata muda hapa basi peleka kwa maandishi.na nimetoa hilo agizo. Kwa hivyo, kuhusu huo utaratibu wako sikufanya makosa kumtoa Mhe. Simai Mohammed Said kwa sababu Kanuni ya 61(e) ipo inazungumza mtu akiwa anafanya fujo kama mimi niliyekalia kiti hapa ninao uwezo wa kumtoa ili Baraza liendelee na shughuli zake. Ahsante.

Mhe. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiye na Wizara Maalum): UWAWAZA Oyee! Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi ili niweze kusema machache kwa muda mfupi lakini nataka niseme yale ambayo hayakusemwa.

Mhe. Mwenyekiti, kusema la haki leo hii wanawake wa Baraza hili wamekasirika na mimi nikiwa mmoja wao, niwe mkweli wa nafsi yangu. Lakini juu ya kukasirika kwangu bado nitakuwa na machache kujaribu kuwawaidhi wenzangu ili tuone jinsi gani mambo haya yataweza kwenda kwa utaratibu unaotakiwa.

Mhe. Mwenyekiti, tumezungumza kanuni, zimezungumzwa sheria, yamezungumzwa mengi hapa; tumelaumiana, tumenyoosheana vidole, lakini hayo yote tunayafanya haya kwa uchungu lakini sio kwamba yatatusaidia sana. Kitakachoweza kutusaidia sisi sote katika kuiendesha nchi yetu hii Baraza la Wawakilishi, Mawaziri, Vyombo vya Sheria tukiwa kitu kimoja hili litakwenda. Lakini tukianza kunyoosheana vidole huyu anafanya, huyu hafanyi, tuhuma ni nyingi. Mimi sina uhakika kama yaliyosemwa yote tunaweza tukaambiwa leteni uthibitisho tukasema kwamba hili tumeliona hili tumelifanya, yanasemwa na yasemwayo yapo na kama yasingekuwepo hili jambo lingekuwa halipo sasa. Kwa sababu kusema kumesemwa sana lakini mambo ndio kwanza mkoko ualike mauwa, kana kwamba kuna udhaifu pahala fulani. Sitaki niseme nani mdhaifu kwa sababu nina imani kwamba hakuna anayetaka hili jambo liendelee.

Mimi sifikiri Polisi si binadamu, mimi sifikiri kama watu wa mahakama kweli wanalitaka. Hivi ingekuwa Polisi, mtu wa Mahakama na wale wote ambao tunanyoosheana vidole tumefanywa sisi au tumefanyiwa watoto wetu tungekubali? Tusingekubali. Sisemi kwamba mambo yako sawa lakini nafikiri tuwe tayari kurekebisha kwa sababu hili jambo linaonekana kwamba linaota mizizi badala yake ina maana papo pahala ambapo hapapo sawa. Ni wajibu wetu kutafuta pale palipoharibika tupatengeneze ili tupate ufanisi wa jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka niseme kwamba tumepewa maazimio tuyatekeleze na kwa matumaini yao walioleta hii hoja ambayo sidhani kama Mhe. Asha Abdalla Mussa kaileta kwa niaba ya Kiwengwa, kaileta kwa niaba ya wanawake wote wa nchi hii. Ni matumaini yetu kwamba haya yakiwa yatatekelezwa basi labda asaa kheri mambo yanaweza yakabadilika. Kwa hiyo, mimi ninachoweza kusema kwamba tumeziona hoja, tumeyaona maazimio nakubaliana nayo kwa asilimia mia moja. Sisi ni wajibu wetu kuhakikisha kwamba tunayapitia, tunayaangalia linalowezekana kufanywa leo lifanywe leo, linalohitaji muda labda na utafiti lifanyiwe utafiti, linalohitaji kununua maana yake kununua *DNA Machine* sio chombo chepesi.

Serikali tutafanya iwezekanavyo Mwenyezi Mungu akipenda hiki chombo kitakuwepo kwenye nchi hii, siwezi kusema ni lini lakini nataka kusema kwamba sidhani kama serikali haiyaoni haya, wanachokisema kweli *DNA Machine* inahitajika. Lakini kwa kesi hizi nyingine mimi sioni kwa nini hata hiyo *DNA Machine* hapa ina haja gani, mtu kakamatwa *red handed* kila kitu kiko pale kilichofanya. Lakini *DNA Machine* pale panapotaka ndipo inapotumika, pale panapo jambo ambalo kwa njia nyengine yoyote haliwezekani pale inatumika. Hata kwa huo udhalilishaji pia inatumika.

Sasa niwaombe ndugu zangu Wawakilishi kwamba tumeyasikia, tunaelewa na tutayafanyia kazi nakushukuru. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kusema machache katika hoja hii.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba nianze kumtanguliza Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema ambaye naye anaendelea kutupa pumzi zake na magharibi haya tukafika hapa tukiwa katika hali ya uzima na afya njema.

Mhe. Mwenyekiti, naomba shukurani za pekee zimwendee Mhe. Asha Abdalla Mussa wa Jimbo la Kiwengwa kwa kuona iko haja ikiwa yeye ni mwanamke ambaye wanawake sote naweza kusema kwamba jambo hili linatuuma na linatuumiza sana. Lakini nami niungane na Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi aliyesema kwamba katika suala hili la udhalilishaji hakuna mtu linalomuuma zaidi kama Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Namuunga mkono na Mhe. Mwenyekiti, wengi tutakuwa mashuhuda Mhe. Rais wakati anafungua Mahakama ya Watoto Mahonda katika hotuba yake alilizungumza suala hili kwa njia ya huzuni na akasema anakaribia kutaka kulia kwa suala hili linavyomuumiza.

Mhe. Mwenyekiti, nikija kwenye mchango wangu kwa ruhusa yako naomba uniruhusu kidogo ninukuu mtoa mada huyu kwa kusema kuwa: "Kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wananchi kwamba baadhi ya vyombo vilivyopewa dhamana ya kushughulikia kesi hizi vimekosa uadilifu katika kutekeleza majukumu yao". Na mimi Mheshimiwa simpingi kwa hili lakini nasema kwamba kuna baadhi ya watendaji bado hawajawa tayari katika kutoa msaada kwa suala hili. Nasema hivyo kwa sababu gani Mhe. Mwenyekiti? Nikiwa kama Naibu Waziri wa Wizara ya Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto nilifanya ziara kisiwani Pema na nikaweza kutembelea sehemu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kubwa naomba kwanza nitoe wito kwa sehemu zilizosemwa matokeo yangu nimeona naanza na ndugu zetu masheha. Masheha tunaamini kwamba wao ni chombo cha serikali lakini mwananchi yeyote anayepatwa na kadhia kwanza anaripoti kwa sheha ndio akafuata taratibu nyengine. Lakini baadhi napenda kurudia tena Mhe. Mwenyekiti baadhi ya masheha hawatekelezi sheria ipasavyo, anakwenda mama mtu na suala lake hili yuko tayari sheha kulisuluhisha suala lile kule kule bila ya kufika juu. Kwa hivyo, tunaomba kwanza masheha suala hili waachane nalo mtu anapokwenda wamuelekeze katika vyombo vya sheria ili sheria nayo ichukue nafasi yake.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile nasikitishwa na masheha, naomba kidogo uniruhusu nitoe historia fupi ndogo. Hivi karibuni kuna mtoto mlemavu mama yake anatoka mtoto yumo ndani, alikwenda kijana akapita ndani mule lakini kwa bahati nzuri naweza kusema kwamba kijana yule hakuwahi kumdhuru mtoto yule. Mtoto yule alipokuja mama yake akamueleza ile habari, mama moja kwa moja akatoka akenda Kituo cha Polisi akapewa barua ampe sheha ili sheha amtake yule kijana aripoti Polisi, kwa bahati barua ile kwa sheha ilikaa ndani haikushughulikiwa. Kijana yule siku ya tatu yake alikwenda tena kule nyumbani akavunja ukuta akaingia ndani na siku ile alifanikiwa kufanya tendo

lake lile. Inasikitisha tunasema kama sheha angewahi kuipeleka ile barua kwa yule kijana akaitwa nafikiria mlemavu yule angewahi kukingwa kabla ya kufikwa na lile dhara.

Vile vile naomba nichukue nafasi hii pia kuzungumza suala zima kuhusu wenzetu Polisi. Wenzangu wengi wamezungumza kuhusu Polisi, kuna mtindo kwamba kinamama wanapofika Polisi baadhi ya askari wanawalazimisha wazee wale suala lile kumaliziwa pale polisi. Sio jambo zuri, Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto inasema Polisi yeyote tutakayekuwa na ushahidi wa kutosha kwamba mama yule amekwenda na kesi wakaifanya ikamaliza pale pale basi kesi ile tutamfungulia askari yule.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea nilikwenda kwenye Kituo cha Mkono kwa Mkono na nikapewa idadi ya madaktari ambao wamesomeshwa suala zima la kuhudumia watoto hao na idadi yao ni 25. Lakini jambo la kusikitisha katika madaktari wale wanaofanya kazi ile ni madaktari watatu, wewe ukienda na mtoto wako ukiwakosa pale utahangaika naye utarudi naye nyumbani. Nitoe wito kwa madaktari hawa jamani hili janga ni letu sote kama si wewe ndugu yako, kama si ndugu yako mwanao, tushirikianeni tuunganishe nguvu zetu ili tuweze kuliondosha suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, waheshimiwa wengi wamezungumzia hapa kuhusu wizara husika isilale, naomba kuwahakikishia Waheshimiwa Wawakilishi kwamba Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto haijalala wala haina usingizi kwa jambo hilo. Kutwa tunapanga mikakati ili kuona hili jambo linamaliza na kuondoka kabisa katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naona unanitizama. Mheshimiwa wengi baadhi ya Waheshimiwa Wawakilishi wamezungumzia kuhusu suala la *DNA*. Mimi niseme tu kwamba *DNA* ni chombo ambacho nacho kitafanyia kazi na binadamu na binadamu tuna mapungufu yetu, kubwa Mhe. Mwenyekiti sisi wenyewe kubadilika kusema na nafsi zetu, turudi kwa Mola wetu, tubadilikeni nafsi zetu tuseme nazo ndugu zangu wanaume. Kila siku najiuliza swali hivi hawa wanaume wana kitu gani katika kichwa chao kinachowatuma.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru naunga mkono hoja. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru sana kwa nafasi uliyonipa nitajitahidi nitumie dakika tano. Kwanza nimshukuru sana mtoa hoja, Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa kuleta hoja hii muhimu sana katika Baraza letu hili

tukufu. La pili, nikushukuru na wewe Mwenyekiti kwa jinsi unavyoliendesha Baraza letu.

Mhe. Mwenyekiti, na Waheshimiwa Wajumbe nataka nikuhakikishieni kwamba kama kuna jambo ambalo linamgusa sana na linamkera Rais wetu ni jambo hili la udhalilishaji wa watoto na wanawake. Hivi karibuni tulikuwa na Wiki ya Sheria, katika wiki ya sheria ile katika kila eneo tulilokwenda kufungua Mahakama kule Mahonda na pale tulipofanya wiki ya sheria Baraza la Wawakilishi la zamani basi Rais amelikemea jambo hili kwa nguvu zake zote, linamkera, linamuudhi na nina hakika linawaudhi watu wote kama lilivyowaudhi Waheshimiwa humu ndani. Lakini nitaanza na kihadithi kidogo, katika hizo dakika tano naomba uniongeze dakika moja kwa hii hadithi tu.

Mimi nilipata ziara kwenda nchi za Kiarabu, katika nchi za Kiarabu ukifuatana na wakubwa mnaalikwa *banquet.* Sasa ukifika kule unapiga mlo lakini mlo wa kule kwanza unaletewa vitu vidogo vidogo vitafunio, visambusa, vibajia. Sasa nilikaa na mwenzangu tukaanza kufanya ile kazi mpaka tushashiba kwa kula vile vitafunio tu, ukaanza kuja wali na vitu vyengine vizito, nikasema hawakunambia mapema kwa nini hawa, mimi haya mambo ya bajia na sambusa nisile nikangojea huu wali kwa sababu mimi nilikuwa nasubiri wali tu. Sasa na waheshimiwa hawa ingekuwa laitani wangepata nafasi pengine niliipata nafasi ya kuzungumza mimi mwanzo basi yaliyozungumzwa mengi wasingezungumza leo kwa sababu majawabu yako tayari na hatua zishaanza kuchukuliwa.

Mhe. Mwenyekiti, hivi ninavyozungumza mimi taasisi zile zote za Polisi, Mahakama, *DPP* na Ofisi yetu ya Mwanasheria Mkuu tumeshakaa tumelipanga vizuri hili, tumeshakutana na maamuzi yametoka. Hivi ninavyokwambia Mhe. Mwenyekiti na kwa taarifa ya Wajumbe jana tarehe 1 Machi, 2017 watu 55 wamepelekwa mahakamani na hawakupewa dhamana hawatoki. Siku mbili hizi hizi mtasikia tena wengine wanapelekwa kama 30 au 40 na hao vile vile wakifika kule hakuna kupewa dhamana watatiwa mahabusu pale. *(Makofi)*

Sheria hii hivi sasa kuna sheria ambayo inarekebishwa, kweli imeipa uwezo Mahakama za Mkoa kufunga mpaka miaka saba. Sheria ile tayari imesharekebishwa miaka 14 lakini sheria hii mbali ya kuwa imependekezwa miaka 14 sasa hivi italetwa hapa Barazani Waheshimiwa tutakuja kuichangia mkisema miaka 24, 34, 40 sisi ndio wenye maamuzi ya kutunga sheria hizo tutakuja kuileta hapa na tutaamua. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuhakikishie sana kwamba *DPP* mpaka hivi sasa wafanyakazi wake wako ofisini wanafanya kazi kwa ajili ya kuhakikisha wanaharakisha hayo. Juhudi zinafanywa na serikali hii namshukuru sana Mhe Mwanasheria Mkuu anafanya kazi nzuri sana, *DPP* anafanya kazi nzuri na amechoka kulaumiwa kwa sababu ya makosa ambayo sio yake. Tatizo la kesi hizi huwezi kuzipeleka mahakamani kama hazina ushahidi, sasa alikosa ushahidi lakini sasa hivi tumeshaamua vyombo hivi vishakutana Mahakama, Polisi, *DPP* kwa kushirikiana na wizara yetu chini ya ushauri wa Mwanasheria Mkuu, mambo yote yamekaa sawa na mambo yameaza jana tumeanza kuchukua hatua.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani itoshe kwa kutoa taarifa hiyo kwanza na *Inshaallah* usiwe na wasi wasi mambo yanakwenda vizuri. Sasa hivi waliokuwa likizo nao tutawaita ili kuharakisha kesi hizi ziende haraka. *(Makofi)*

Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda nichukue nafasi hii kumshukuru Mweyezi Mungu kwa hili jambo ambalo limefanyika siku ya leo na mimi nitapata faraja na kuweza kulala usingizi leo. Kwa kweli suala hili mimi limenitia moyo sana na nipende kumshukuru Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuongeza nguvu katika wizara yangu. Sasa hivi nina Naibu Waziri kama alivyosema kazi anazofanya anajitahidi na pia tumeongezewa mshauri ambaye alikuwa ni mstaafu Waziri wa Kazi ambaye ana uzoefu na anajua kabisa masuala yaliyokuwepo ndani ya wizara, Mhe Zainab Omar Mohammed.

Pia niseme kwamba haya yote waliyozungumza wenzangu nayaunga mkono na naomba tuendelee kusikamana katika jinsi hii. Bahati nzuri kamati hii ni kamati ambayo imesimamia masuala ya wizara yangu, ninashukuru sana kwamba wamezingatia mengi pamoja na yale yaliyokwishawasilishwa huku lakini kwa kazi waliyoifanya napenda kusema kwamba, Mwenyezi Mungu aendelee kuwabariki kwa sababu katika wizara kuna mambo mengi sana yaliyokuwa yamefanywa na kamati nyingi, ambazo kuwa zimeundwa kama alivyosema Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora pale na kamati za kutoka kwenye shehia, Kamati za Waratibu wWnawake, kuna Kamati za Masheha, kuna Kamati za Wakristo, Kamati za Wanawake mbali mbali, *NGO's*, wote wanafanya kazi moja ya kutaka kuhakikisha kwamba suala hili linakwisha.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kinachotokea hapa niseme kwamba nawashukuru sana UWAWAZA na namshukuru sana Mheshimiwa ambaye mara nyingi nikienda kwenye UWAWAZA nakuta kuna mwanamme mmoja mashuhuri sana wa

kufundisha UWAWAZA, naomba Mwenyezi Mungu ambariki sitaki nimtaje, lakini ni mtendaji mzuri sana aliyeko kwenye Baraza la Wawakilishi ambaye mara nyingi anakuwa anawafundisha na amewafumbua macho.

Sasa kama kuna suala la mwanamme tumpongeze ni katibu aliyekaa pale, Ndugu Mussa Kombo Bakari, amewafungua sana macho UWAWAZA na amekuwa akielimisha sheria, akitumia kanuni, zile kanuni tulizokuwa tunavutiana hapa kupigana mabuti na sisi sasa hivi tunaweza kupiga mabuti makubwa makubwa, hivyo kila mmoja anajua. Kwa hivyo, suala hilo la kutishana kwamba akisimama akitoa kanuni unatetemeka halipo tena.

Mhe. Mwenyekiti, nipende kusema tu kwamba kwa kweli *NGO's* zinafanya kazi na mambo mengi yanafanya kazi na tupende kumpongeza Mhe. Rais katika ile sheria iliyokuwa ya miaka 100 iliyotungwa India, ambayo tumekuwa tukiitumia Tanzania sasa hivi imefuatwa na tumeanza na sheria mpya ambayo itakuwa na ushahidi mkubwa wa kutosha. Hata huyu mtoto mlemavu na yeye atafatiliwa Pemba akasikilizwe, kwa sababu kwa kumtaja na kumjua yule mtu kuna namna atakayowekwa mbele ya yule mtu akionesha dalili ya kwamba anamuogopa basi sheria itachukua mkondo wake. Na hawa akina baba wote wanaosema watoto wanakwenda nao watachukuliwa hatua zao, sasa hivi kuna *operation* ya kukamata hawa wabakaji, walawiti na wanaofanya shughuli zetu kama inavyofanyika kwa madawa ya kulevya Tanzania Bara.

Mhe. Mwenyekiti, tulikuwa tumeamua kuanza rasmi tarehe 1, bahati nzuri kama mlivyokwishapewa taarifa pale kwamba tayari watu 55 wako ndani, watano wameachiwa kwa sababu wako chini ya miaka 18 lakini na bado tunaendelea kuwasaka na tutawasaka kwa sababu tuna-*evidence* kutoka kwa wanafunzi maskuli mbali mbali. Pia kuna *NGO's* zimepita maskuli na kutoa taarifa ya kutosha kwamba watoto wote wanaokwenda kununua vitu madukani wamebakwa na watu wanaouza maduka, wanaouza matunda, walimu wao wenyewe, wazazi wao *list* zote tunazo kama walivyokuwa na madawa ya kulevya na sisi hizo *list* tunazo. Kwa hivyo, sasa hivi hakuna kulaza damu, na kama kuna watu basi wajisalimishe mapema kabla hatujawashughulikia tutawaaibisha safari hii, hatulazi damu.

Mhe. Mwenyekiti, napenda niseme kwamba naishukuru kamati na haya yote pamoja na yale ambayo tumeyaandaa kama wizara tutakwenda kuyafanyia kazi. Nawashukuruni sana na Mwenyezi Mungu awabariki kwamba hili suala limetosha, limetoshaa, kaeni mkao wa kukamatwa na nyinyi wanaume tumechoka. (*Makofi*)

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa juhudi anazozichukua kwa kuanzisha Mahakama ya Kesi za Watoto.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimpongeze Mwenyekiti wa UWAWAZA kwa kuongeza kikosi kazi cha Umoja wa Wawakilishi Wanawake na kusimamia kwa kasi juu ya vitendo vya udhalilishaji vinavyojitokeza siku hadi siku. Pia niipongeze Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kwa juhudi wanazozichukua kwa kuhakikisha kwamba vitendo hivi vinaondoka.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwashukuru sana Ofisi ya Spika pamoja na watendaji wake wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kunipa mashirikiano mpaka hoja yangu hii kuweza kuileta Barazani. Vile vile niwashukuru sana wajumbe wote waliochangia hoja hii kwa michango yao mizuri na yenye manufaa kwa taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatambue wajumbe wote waliochangia na kuwataja kwa majina. Katika hoja yangu hii nimepata wachangiaji 48. Mhe. Mwenyekiti, wajumbe waliochangia moja kwa moja ni wajumbe 18 na waliochangia kwa maandishi ni wajumbe 30.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwataje kwa majina waliochangia moja kwa moja ni:

1. Mhe. Bahati Khamis Kombo
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Salma Mussa Bilal
4. Mhe. Suleiman Sarahan Said
5. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
6. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
7. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali
8. Mhe. Mussa Foum Mussa
9. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
10. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
11. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
12. Mhe. Zaina Abdalla Salum
13. Mhe. Mgeni Hassan Juma
14. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
15. Mhe. Dkt. Sira Ubwa Mamboya (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)

16. Mhe. Naibu Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto
17. Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora
18. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto

Mhe. Mwenyekiti, pia naomba niwataje waliochangia kwa maandishi kama ifuatavyo:

1. Mhe. Mohammed Mgaza Jecha
2. Mhe. Rashid Makame Shamsi
3. Mhe. Khadija Omar Kibano
4. Mhe. Suleiman Makame Ali
5. Mhe. Sada Ramadhan Mwendwa
6. Mhe. Ali Mussa Ali
7. Mhe. Yussuf Hassan Iddi
8. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
19. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
9. Mhe. Said Omar Said
10. Mhe. Juma Ali Khatib (Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum)
11. Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
12. Mhe. Simai Mohammed Said
13. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
14. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora
15. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo
16. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
17. Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
18. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
19. Mhe. Shehe Hamad Mattar
20. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
21. Mhe. Hidaya Ali Makame
22. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
23. Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji
24. Mhe. Miraji Khamis Mussa
25. Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali
26. Mhe. Shaib Ali Shaib
27. Mhe. Ali Khamis Bakar
28. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
29. Mhe. Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira

Mhe. Mwenyekiti, wajumbe wamechangia kwa hisia kubwa kuonesha kuwa suala hili limetosha, lakini Mhe. Mwenyekiti kutokana na muda niwaombe wajumbe kwamba michango yao nimeithamini na kamati inayohusika ipo pamoja na wizara husika imesikia, naamini…

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Asha

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Naam!

Mhe. Mwenyekiti: Naomba utoe hoja.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Mhe. Mwenyekiti, niwashukuru sana wajumbe wote waliochangia kwa haya machache naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, hoja imetolewa, naomba niwahoji wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mkono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe na mimi niwapongeze wote waliochangia hoja hizi tokea asubuhi, lakini pia nimpongeze mtoa hoja Mhe. Asha Abdalla Mussa kwa kazi yake mahiri. Sasa kabla ya hapo naomba niikumbushe serikali kwa kutumia Kanuni ya 58(9) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, hoja zilizotolewa leo zote zinahitaji taarifa ya utekelezaji kwa kipindi cha miezi mitatu. Kwa hivyo, naiomba serikali panapo majaaliwa hoja hizi na taarifa zake basi kipindi cha miezi mitatu tukijaaliwa zilete yale maazimio yaliyoletwa katika hoja hizi na zipatiwe majibu. Nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa utulivu wenu, naomba niakhirishe kikao hiki mpaka kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 1:49 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 03/03/2017 saa 3:00 asubuhi)